*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini Saba – Tarehe 5 Juni, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoangalia ratiba yetu, zile siku 26 za kujadili Wizara moja moja zimemalizika jana, tulimaliza na Wizara ya Fedha. Sasa ile ndiyo tulikuwa tunajadili sekta moja moja na kama nilivyokuwa nimewaambia siku moja, kwamba hatuwezi kufanya maamuzi ya dhahiri katika zile sekta moja moja, kwa sababu kutatokea na mabadiliko mengi.

Kwa hiyo, kuanzia leo tarehe 5 Juni, 2014, mpaka tarehe 11 Juni, 2014 Kamati yetu ya Bajeti na Serikali, wataendelea kujadiliana kwa undani zaidi kuhusu maeneo yale ambayo sisi tulifikiria kwamba ni muhimu zaidi yapewe uzito wa pekee. Kama vile tulivyosema, Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi ya Teknolojia na mengine ambayo wataona yanafaa. *(Makofi)*

Yaani pointi hapa ni kwamba, si kwamba kuna fedha zinazotoka mahali pengine, hapana, ni hizo hizo humu ndani tuangalie ni vitu gani tunaweza kuviondoa tukaviingiza katika mambo yale ambayo ni muhimu, si kwamba kuna fedha nyingine zitakazotokea.

Kwa hiyo, kazi ambayo itakuwa inafanyika, kuanzia siku ya leo mpaka tarehe 11 Juni, 2014 kwa Bajeti ya *Committee* na Serikali na kwa kiwango fulani Wenyeviti watahusika, kushirikiana pamoja na *Budget Committee* kuona kwamba tunashirikiana vizuri.

Kwa maana hiyo ni kwamba katika kipindi hiki tofauti na miaka mingine, toka mwaka jana, Bunge linashiriki kunadika ile Bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo itakayosaidia Waziri wa Fedha siku ya tarehe 12 kusoma kitu ambacho sisi kwa namna moja au nyingine tumeshiriki. Kwa hiyo, nilipenda kuwakumbushahiyo

kwamba tutakuwa tunafanya shughuli zile ambazo mlipata *addendum* ya agenda. Tutakuwa na Uchaguzi, tutakuwa na Maazimio katika siku tano, kwa sisi ambao tutakaokuwa tunakaa Bungeni. Kwa hiyo, naomba ushiriki wenu uwe wa hali ya juu katika mazingira haya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninachowaombeni muweze kufanya kazi hiyo na kama mtakavyojua, Jumamosi, mmoja wa vijana wetu anafunga pingu ya maisha, Mheshimiwa Nassari atafunga Jumamosi harusi yake. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri na siku hiyo, ratiba yetu inaruhusu, sisi hatutakuwa na kazi siku ya Jumamosi. Kwa hiyo, nadhani itakuwa ni siku nzuri ya huyo mtoto wetu, siku hiyo ya Jumamosi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, leo ni siku ya Alhamisi, kipindi cha kwanza huwa tunaanza na maswali ya Waziri Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa bahati isiyokuwa ya kawaida pia kiongozi wa Kambi ya upinzani naye hayupo, kwa hiyo, hakuna cha kuwakilisha mwenzake. Katibu! *(Makofi)*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Highness Samson Kiwia.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa niweze kumwuliza Maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mgogoro wa kiutawala katika Manispaa ya Ilemela, uliosababishwa na *Mayor*, kufukuza madiwani watatu wa CHADEMA. Kwa sasa umechukua takribani mwaka mmoja na miezi sita, bila ofisi yako kulipatia ufumbuzi tatizo hili ambalo kimsingi linakwamisha Maendeleo ya Halmashauri ya Ilemela. Lakini pia linachochea mazingira ya kutokuwepo na mazingira ya amani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini, kimsingi kigezo alichotumia *Mayor* kuwafukuza hawa madiwani watatu wa CHADEMA, kimsingi hakikidhi haja na hakikuzingatia Kanuni wala Sheria tunazotumia katika Manispaa yetu ya Ilemela kwa kusema kwamba Madiwani hawa watatu hawakushiriki vikao vitatu mfululizo vya kawaida.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uchaguzi wa *Mayor* ulifanyika tarehe 9 Novemba, 2012, na tarehe 10 Desemba, 2012, *Mayor* aliandika barua ya kuwafukuza hao madiwani watatu, mwezi mmoja baada ya Uchaguzi wa *Mayor* tu. Katika hali ya kawaida, hakuna namna unaweza ukapata vikao vitatu vya mfululizo ndani ya mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, kimsingi, suala hili liko wazi sana na kimsingi utaona kwamba, mara nyingi nimewasilisha kwako vielelezo mbalimbali, lakini pia limeshazungumzwa ndani na nje ya Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara ya mwisho ulikiri hapa Bungeni kwamba, ni kweli uliona kwamba, hapakuwa na sababu za msingi za kufukuzwa hao Madiwani watatu na ukasema kwamba, ulifanya uamuzi wa kuwarejesha. Lakini kuna pingamizi limetoka mkoani Mwanza la kupinga maamuzi yako.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, na ukasema basi unahitaji muda wa…

**SPIKA:** Isiwe kesi, yawe maswali.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Kwa hiyo,Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda ambao suala hili limeshughulikiwa umeshakuwa mrefu sana, na kimsingi, haki ambayo inacheleweshwa kwa makusudi ni sawasawa na haki iliyopotea. Naomba kupata kauli ya Waziri Mkuu leo juu ya muafaka wa madiwani watatu hao waliofukuzwa kimkakati na kusababisha Kata tatu zaidi ya mwaka na miezi sasa kukosa uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Unaomba Kauli ya Waziri Mkuu au utataoa shilingi. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi sana, bahati mbaya tuliamka na mambo fulani fulani, nimechelewa kidogo kwenye simu huko.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema kuhusu Mheshimiwa Kiwia ni kwamba, kwanza nataka nikutoe wasiwasi, hakuna kitu chochote cha makusudi kwa maana ya kuchelewesha. Ndiyo maana muda wote uliponiuliza nilikuwa najaribu kukupa maendeleo ya jambo hili.

Jambo hili lilietwa kwangu kwa njia hii ya kawaida, kwamba tunahitaji maamuzi ya Waziri mwenye dhamana, mimi nikapitia, wataalam wakanisaidia, nikarejesha kile nilichofikiria, lakini baadaye nikapata *counter request* kwamba hapana, nadhani maelezo uliyokuwa umepewa hayakuwa sahihi, kwa hiyo, nika-*demand* waniletee.

Wakaleta, nikajaribu tena kupata *opinion* nyingine ya ziada. Juzi tu hapa, ndiyo nimepata hayo maoni sasa ya TAMISEMI kwa mara ya mwisho. Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie tu kwamba, hakuna kitu chochote cha makusudi, lakini ni kweli limechelewa kidogo. Lakini sasa hivi tuna *finalize* ili niweze kutao sasa *position* ambayo mimi naamni kama Waziri mwenye dhamana, hii itakuwa ndiyo mwisho wa jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiwia, swali la nyongeza, naomba yawe mafupi jamani!

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kama nilivyotangulia kusema kwamba suala hili sasa limechukua mwaka mmoja na miezi sita, kata tatu, hazima uwakilishi wa Udiwani. Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa anatuambia kwamba sasa ndiyo amepokea taarifa, lakini taarifa ya awali aliyoitoa hapa Bungeni ya kupokea pingamizi ni zaidi ya miezi nane sasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwa niaba ya wananchi wa Ilemela, tuwatendee haki, ni lini utahitimisha na kuleta muafaka wa mgogoro huu mkubwa ambao unasababisha kurudi nyuma kwa Maendeleo ya manispaa ya Ilemela? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, tatizo unaposema ni lini maana yake unataka niseme tarehe, sasa tarehe siwezi kusema, lakini nimekuhakikishia tu kwamba jambo hili nimekwishalipata sasa hivi mimi ndiyo nafanya uamuzi wa mwisho baada ya ubishi wa muda mrefu.

Sasa nitakachoweza kukuahidi tu ni kwamba, jambo hili tutalipa umuhimu mkubwa, tutaharakisha mapema kadiri inavyowezekana tutarejesha majibu yetu mkoani na kwa ajili ya Jiji kujua *potions* ikoje.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa mimi fursa niweze kumwuliza Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba tumekuwa tukiendelea kushuhudia urasimu unaofanyika katika Idara nying nyingi kwenye Serikali, kitu ambacho kinapelekea kulipa taifa hasara.

Katika mantiki hii ningependa kuchukua mfano wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki, ambalo lilikuwa lipo Arusha na mpaka sasa hivi lipo Arusha, lakini Baraza hili lipo kule Arusha kuanzia mwaka 1997, mwaka 2003 walia-*apply* katika kutaka ardhi ili waweze kujenga *Head quarter* yao hapa Tanzania.

Kama nilivyosema kwamba kuna urasimu, mpaka mwaka huu walikuwa bado hawajapewa kibali, kitu ambacho kilipelekea wakae na kuamua kwamba watafute *altenative* kwenye nchi zingine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba uwepo wa Bodi hii, kwa maana ya *East African Business Council,* inatoa *opportunity* nyingi sana za kiuchumi, kwa sababu ina *multiply effect,* kwa maana inatoa ajira moja kwa moja, katika mahoteli, utalii na vitu vingine.

Nataka kujua ni kwa nini tunachukua muda mwingi sana takriban zaidi ya miaka 10 kuweza kutoa kibali au kuweza kutoa ardhi ambayo walikuwa wameiomba kule Lakilaki ili waweze kujenga *Headquarter* yao hapa. Badala yake walipo-*apply* nchi kama ya Rwanda, walichukuwa siku 21 tu na kupewa. Naomba kujua kwamba unatambua hasara inayotokana na kukosa *opportunity* hii na kupelekwa nchi nyingine, taifa lina-*incur? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijui kama, ni la kisekta zaidi, lakini jaribu.

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa *Ester, of course* swali alilouliza ni zuri, lakini kwa bahati mbaya siwezi kuwa na majibu ya jambo hilo. Mimi nimehangaika na maeneo mengi pale Arusha, nimehangaika juu ya Chuo cha Nelson Mandela, tukafanikiwa. Nimehangaika juu ya Chuo ambacho wanataka kujenga watu wa Aghakan, na tunakwenda vizuri. Nimehangaika na *East Africa Community Headquarters* na tukalimaliza vizuri. Sasa jambo hili, mimi ndiyo nalisikia kutoka kwako, kwa sababu sijawahi kulisikia, sasa pengine nikuahidi tu kwamba, maadamu umeli-*raise*, acha mimi niulize vyombo vinavyohusika ili niweze kujua tatizo liko wapi na kwa nini tumechelewa.

**SPIKA:** Haya jamani, swali la nyongeza amesema hajui, sasa utaongeza nini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Ninalo.

**SPIKA:** Anasesema hajui.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nina swali, niache ni *right* yangu.

**SPIKA:** Lingine umebadilisha!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ni hilo hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu umesema suala hili hulijui, nilitaka kujua, baada ya kufuatilia na ukalijua vizuri, utachukua hatua gani kwa viongozi ambao wamepelekea hiyo *opportunity* ikaondoka kwenda Rwanda?

**WAZIRI MKUU:** Sasa wewe tatizo, umeshaamua kwamba wameshakosea. Kwa hiyo, unataka mimi niseme nitachukua hatua gani! Nitachukua hatuakutegemea na aina ya maelezo yatakayokuwa yamepatikana. *(Makofi)*

Haiwezi kuwa kwa maana hiyo unayotaka wewe kuisema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mtu akisema hajui, sasa ukimwuliza tena…….

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:**Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwepo na wimbi kubwa la Askari Polisi baadhi, ambao siyo waaminifu, wale wanaotembea na pikipiki, wanaitwa bodaboda, wanaotembea na pikipiki wanaitwa tigo, huwa wanawanyanyasa vijana kwa kuwatusi, kuwapokonya pikipiki, na bahati mbaya zaidi wanawapiga faini ambazo hawapewi risiti ya aina yoyote.

Je, Serikali haioni kwamba tatizo hili ni baya kwa vijana ambao wanajiajiri wenyewe kutafuta riziki zao? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, jeshi la polisi ni kubwa, kwa hiyo, anachokisema Mheshimiwa Ngonyani, inawezekana kipo, lakini sana sana ninachoweza mimi kusema hapa ni kwamba, nitazungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nitamwelekeza achukue hatua stahiki kwenye maeneo yale ambayo wewe una maelezo thabiti juu ya nini kilichotokea. Kwa sababu kazi yetu sisi kama polisi, kwa kweli zaidi ni usalama wa raia wetu, lakini wakati ule ule tunalo jukumu la kuhakikisha vilevile kwamba, sheria zile zinazohusu majukumu yao, nazo wanazisimamia kwa uadilifu mkubwa kwa kadiri itakavyowezekana.

Endapo tutabaini kwamba kuna polisi wenye kasoro hizo, hatua stahiki zitachukuliwa, kama ambavyo tumekuwa tukifanya kila inapobainika. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:**Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru.

**SPIKA:** Sijakuita, Mheshimiwa Ngonyani.*(Kicheko)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:**Mheshimiwa Spika, ahsante.*( (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa majibu yako mazuri sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye jimbo langu la Korogwe Vijijini, kumekuwa na wimbi la Askali ambao wanawapokonya na majina ninayo. Wanawapokonya, kuwanyanyasa na ukizingatia sasa hivi mvua kubwa imenyesha, hakuna usafiri wa magari, vijana wanatumia pikipiki, lakini imefika hatua, kwamba askari hao wanawaambia kwamba mtaleta mpaka ndugu zenu hapa, mpaka kieleweke.Wakifika pale wanapewa elfu 5000, ha hawapewi listi, inaishia tumboni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, watu kama hawa nikikuletea majina utawafukuza leo hii? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tupe majina, lakini vilevile itabidi wafanya uchunguzi kidogo, kwa sababu, nafikiri Mheshimiwa Ngonyani unajua kwamba, vijana wetu wengi sana wanapoteza maisha kwa sababu ya hizi pikipiki na wengi sana wamekuwa na ulemavu kwa sababu ya hizi pikipiki.

Kwa hiyo, ni jambo ambalo lazima tuliangalie pande zote mbili. Inawezekana kweli polisi katika utekelezaji wanazidisha kidogo. Lakini lazima tujue kwamba pale ambapo ni kwa nia njema, labla kijana anaendesha mwendo kasi, hana leseni, hana kofia kichwani, pikipiki haina hiki, ni dhahiri lazima polisi atimize wajibu wake.

Shida hapa ni namna wanavyotekeleza, ndiyo maana nimesema Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mwenye sekta hii, tukipata majina, tukajua na matukio yenyewe yalivyo, nina hakika kabisa hatua stahiki zitachukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, na mimi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali kidogo. Nchi yoyote ambayo imeendelea, imewekeza katika suala la elimu. Kwa mfano Malaysia, imeendelea kwa kuwekeza katika elimu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi watoto wetu wanabeba vidumu vya maji na fagio, wenzetu jirani zetu Wakenya, watoto wanakwenda na *laptop* shuleni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuliambiwa *change* ya *Rader* itapunguza tatizo la madawati mashuleni, lakini mpaka leo hii tunashuhudia watoto wetu wanakaa chini na dawati moja wanakaa hata watoto watano.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kauli yako.

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri pengine suala la msingi hapa ni jitihada mabazo Serikali inafanya kuhusu elimu. Kweli Serikali imechukua maamuzi mengine makubwa mno, ambayo yamefanya suala hili la elimu limezaa changamoto nyingi sana, lakini kwangu mimi changamoto zote hizo ni jambo ambalo lazima twende nalo tukilikabili siku hadi siku.

Tumeongeza *enrollment* yetu kwa kiasi kukubwa sana, darasa la kwanza mpaka la saba. Matokeo yake ni kwamba limezaa sasa idadi kubwa ya mahitaji ya shule za sekondari, na hivyo hivyo kwenye *A-Level* na hivyo hivyo kwenye Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba changamoto zipi nyingi, ambazo lazima twende tuhangaike nazo, tuhakikishe tunazifikisha mahali pazuri. Rai yangu kwa Bunge ni kuendelea kusaidia Serikali hii.

Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, izidi kukua siku hadi siku, kwa sababu msingi wa yote haya ni *Budget Constraints*. Tukiwa na Bajeti nina hakika mambo mengi yatakwenda. Hivyo basi, mimi nakubaliana na wewe kwamba changamoto zipo, lakini hatujazipuuza, ndiyo maana tunahangaika sana na jambo hili. *(Makofi)*

Juzi hapa nimetoa maelekezo kwa ajili ya madawati kutaka mikoa ikae chini inaangalie kuwa na *program* ambayo itatusaidia kupunguza kwa kasi zaidi suala hili la upungufu wa madawati.

Hata hivyo, ukimaliza madawati, si mwisho, bado tuna kazi kubwa ya kujenga nyumba za walimu, tuna kazi kubwa vilevile ya *hostels*, tuna maabara. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tutambue tu kwamba ni kazi kubwa, lakini jukumu la Serikali ni kukabiliana na hizo changamoto zote ili tuweze kufikisha elimu iwe na ubora unaotakiwa.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikuulize swali la nyongeza, kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye mambo ya utandawazi, mambo ya sayansi na teknolojia. Huoni sasa umefika wakati wawanafunzi wetu ambao wanaanza darasa la kwanza mpakadarasa la saba wawe na *laptop* shuleni.

**BGT050614AM02ME**

**SPIKA:** *Okay*! Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala hapa kubwa ni moja tu. Unataka *laptop* kwa watoto wote wa shule, inawezekana? Kwa sababu kila kitu lazima uulize swali hilo.

Upande wa Serikali tulichofanya, tumefanya uamuzi wa kusaidia wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la saba, si kuwa na *laptop*, hapana, kuwa na kitu kinaitwa *tablets*. *Tablets* ni aina moja ya *computer* ndogo ambayo inamuwezesha mwanafunzi, badala ya kubeba vitabu hivi tunavyohangaika navyo unajaza vitabu vyote katika hicho kiji-*computer* kidogo.

Ni kitabu lakini katika mfumo wa leo wa dijitali. Sasa hii itatusaidia kuondoa kero ya vitabu lakini itamwezesha vile vile kuweza kukitumia chombo hicho vizuri.

Unapotoka kwenye hatua hiyo ukaenda sekondari ni lazima sasa uanze kutazama hatua nyingine ya juu zaidi, kadiri unavyokwenda juu l*aptop* itakuwa na maana sana. Sasa hivi tunahangaika na wanafunzi wa vyuo vikuu kila mmoja tuone namna ya kumuwezesha. Pole pole tutafika huko Maria Mheshimiwa Wangu. Lakini kwa sasa sisi tumelenga kwanza katika hatua hii ya *tablets* kwa ajili ya kuwawezesha kuwa na vitabu ndani ya mfumo wa dijitali.

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukitazama *Road Act* ya 1973 na *amendment* yake ya mwaka 1996, kwamba inatakiwa gari zote ziwe zinafanyiwa *inspection* ili kuweza kujua kiwango cha *emission* na uimara wake.

Ajali nyingi zinazotokea zinagharimu maisha ya Watanzania, lakini pia zinasababisha kuwa na *traffic jam* pale amboko gari zinapata *breakdown*.

Je, Serikali ina uamuzi gani wa haraka kuweza kutanzua hili kwa sababu ni gharama kubwa kiuchumi na kwa kijamii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana lazima uwe injinia.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kujibu tu swali la Mheshimiwa Mangungu kama ifuatavyo. Analolielezani kweli lakini kwa sehemu kubwa linatokana vile vile na mfumo au utaratibu wa sasa ambao unaruhusu magari, hasa *used* magari, magari yaliyokwisha kutumika kuweza kuingizwa nchini.

Kwa hiyo mengi unakuta ni yale ambayo yamechoka, au baada ya muda mfupi yanakuwa yamechoka, kwa hiyo yanasababisha kweli moshi mwingi, jambo ambalo kimazingira si zuri sana.

Lakini, mimi kwangu nilitaka niunganishe jambo hili na kile nilichokiona kwenye hotuba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi, ajali nchini. Ajali nyingi zinatokana vile vile na magari mengi ambayo ni mabovu, magari ambayo huduma yake ya kigereji bado haijawekewa utaratibu mzuri sana. Kwa hiyo mimi nadhani alichokisema Mheshimiwa Mangungu ni jambo kubwa na ni lazima tulipe nafasi kubwa. Nchi za wenzetu wanazo gereji maalum ambazo kila gari ni lazima lipite, nani mfumo wa *computer,* unaweza ukakuambia mapungufu yote yaliyoko kwenye gari, na unaambiwa nenda karekebishe baada ya kurekebisha ndipo uendelee. Huwezi ukaruhusu gari kupata bima mpaka kwanza imepita kwenye utaratibuwanamna hiyo.

Kwa hiyo pengine jambo hili ni suala tu la kuagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, pengine washirikiane na Wizara ya Uchukuzi, tuanze kuona jambo hili mapema na tuchukue hatua hizi haraka sana. Mtaona umuhimu wake mtakapoanza kutumia barabara kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo kasi, kwa sababu barabara zile zimepanga magari kwa mstari. Kwa hiyo, ukiwa na gari bovu utamgonga mwenzako.

Kwa hiyo iko haja sasa jambo hili kuliangalia vizuri, kuanza kuwa na utaratibu ambao utatuwezesha kuwa na vipimo hivyo, tutapunguza moshi, lakini kubwa tutakuwa na uhakika na ubora wa magari kabla halijaanza safari au kutembea barabarani.

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya matumaini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kipindi ya miaka ya themanini mpaka hivi sasa Serikali iliamua ku-*hire* makampuni ya nje kama *Jay* kule Japani kwa ajili ya kufanya *inspection* hizi kabla gari hazijakuja nchini. Ni lini Serikali itachukua uamuzi sasa wa magari haya yakaguliwe hapa nchini badala ya sasa tunapoteza zaidi ya Dola milioni kumi kwa mwaka kuwapa watu nje na tunatoa ajira kule badala ya kuleta ajira hizi nchini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Mangungu anachokisema ni kweli lakini lazima niongeze vile vile kwamba inategemea vile vile na uaminifu wa watengaji katika eneo hilo iwe ndani, iwe nje.

Kwa hiyo rai yake ni ya msingi na nafikiri hata Wizara inayohusika imeanza kuliangalia hilo. Tulikuwa tunafikiria TBS chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani tuanze kuangalia namna tunavyoweza kushughulikia jambo hili kutoka huku ndani, au kwa pande zote mbili ili tuweze kuwa na uhakika kwamba magari haya na vitu vingine, kabla havijaruhusiwa kuanza kufanya kazi hapa tuwe na uhakika kwamba mmepita katika hatua zote stahiki.

Kwa hiyo ni rai nzuri, nadhani Wizara zinazohusika zitakuwa zimesikia nilichokisema hapa.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda.

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu lenye sehemu a na b, kama ifuatavyo…

**SPIKA:** Hakuna cha a na b, ni swali moja tu.

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa waziri Mkuu, hivi karibuni zao la ufuta limekuwa ni miongoni mwa mazao ambayo yanategemewa sana katika kuinua uchumi wa

nchi na kuleta maisha bora kwa wananchi wa Tanzania hususan katika mikoa ya Mbeya, mkoa wa Lindi na mikoa mingine. Lakini katika msimu wa kilimo wa mwaka wa jana 2013, Serikali ilitoa maelekezo na bei elekezi ya zao la ufuta kwa kilo kuwa Shilingi elfu mbili na mia tano hadi elfu tatu na wakulima walipata fedha hiyo.

Lakini katika msimu wa mwaka huu tayari walanguzi ambao hawawatakii mema wakulima, wameanza kununua ufuta katika mikoa ya Lindi kwa bei ya Shilinigi elfu mbili mia mbili hadi elfu mbili mia tatu kwa kilo moja.

Je, Serikali iko tayari sasa kusimamia na kuhakikisha kwamba walanguzi hawa hawapati fursa na wananchi wanauza ufuta wao kwa bei ya kati ya Shilingi elfu mbili mia tano hadi elfu tatu kwa kilo moja?

**SPIKA:** Haya! Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mtanda ni kweli, lakini ni matokeo ya soko huru kwa upande mmoja na ndiyo maana tumekuwa na jitihada kubwa tu za kujaribu kuona mfumo wa stakabadhi ghalani kama suluhu ya jambo mhili. Lakini kwa bahati mbaya ni dhana ngumu, naona wengi wana-*resist* sana na Lindi ni moja kati ya eneo ambalo jambo hili limekuwa na kigugumizi kikubwa sana, na hasa rafiki yangu Mheshimiwa Bwege, yaani yeye hataki kabisa, piga geuza, anataka soko hili ndilo litambe, liendelee, sasa matokeo yake ni hayoi anayoyasema Mheshimiwa Mtanda.

Sasa, sina namna ya kuweza kuagiza wafanyabiashara hawa kwamba kuanzia leo wekeni shilingi hizi, kwa sababu wanakonunua sijui, maana mingine wanaweza kuwa wakaipata mitaani, mingine vijijini.

Kwa hiyo, ndiyo maana tulifikiri suluhu ya kweli ni hiyo. Lakini mimi naomba tu nichukue hili tatizo ulilolieleza, nitazungumza na Mkuu wa Mkoa, tutajaribu kuona namna ya kuweza kusaidia kuweza kumwezesha mkulima kupata bei ambayo ni nzuri katika mazingira ya mkoa wa Lindi.

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru Wana-Lindi kwa majibu mazuri na ninaamini utalifanyia kazi. Sasa swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sasa wakulima hawa, ili waweze kuondokana na mfumo huu ni vizuri sasa kuleta utaratibu wa viwanda vidogo vidogo vya kukamua mafuta ya ufuta ambayo hayana *cholesterol,* Serikali iko tayari sasa Wananchi wa Lindi, hususan wananchi wa Mchinga ambao umeme sasa hivi pale tunakaribia kuweka ili viwanda vidogo vidogo viweze kufanya kazi na wakamue ufuta wao?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni wazo zuri tu, lakini na mimi naomba niombe, sasa nataka nitoe changamoto hii kwa Halmashauri za Mkoa wa Lindi, kwa sababu mashine zile kwa ajili ya kukamua mafuta haya si mashine kubwa za ajabu, hapana. Ni mashine ndogo ndogo ambazo zinaweza kusaidia sana.

Kwa hiyo, naomba tu Halmashauri za Mkoa wa Lindi, kwa sababu zao la Ufuta Mkoa wa Lindi ni zao moja muhimu sana, ingawa nimeona sasa hivi hata Katavi na Rukwa na maeneo mengine hapa nchini kwa kweli limeanza kuwapa watu nafasi kubwa sana. Kwa hiyo, mimi

nakubaliana na wewe lakini nitakapozungumza na Mkuu wa Mkoa nitampa vile vile kazi ya kutazama uwezekano wa Halmashauri kwanza kufanya kazi hiyo, kwa sababu inawezekana kabisa katika ngazi za Halmashauri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee na Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, shule za Misingi nchi hii zina matatizo makubwa na hazieleweki ziko wapi na hili linaonekana tu kwenye vibao.

Kuna shule ukipita barabarani zimeandikwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nyingine zimeandikwa Mkoa fulani, nyingine zimeandikwa Serikali ya kijiji. Shule za Misingi hazina *Administration Block*, hazina bendera, watoto hawaelewi mambo haya, yaani kiasi kwamba hata akiulizwa swali kwenye mtihani hawezi kuandika jina la Wizara kwa sababu hata kibao cha shule yake kimekosewa na hili ni nchi nzima. Serikali inasema nini kuhusu mambo haya ya ajabu kwenye nchi yetu?

**SPIKA:** Na zenyewe ni shule za Msingi, hakuna shule za Misingi. Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkosamali mimi ananionea katika hili. Shule zote za Msingi ni shule ambazo chini ya Mfumo ulivyo sasa ziko katika Halmashauri zetu za Wilaya au Manispaa au kwenye maeneo yanayoitwa Halmashauri za Miji. Iko hivyo kwa sababu Sera ambayo ilikubalika hapa ni ile ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi. Shule hizi kwa sababu ziko kwenye ngazi za vijiji wamiliki wake itakuwa ni Halmashauri za Wilaya katika maeneo yanayohusika, ndio msingi wa jambo hili. *(Makofi)*

Wizara ya Elimu kama zilivyo Wizara nyingine zote, wataendelea kuwa ni Wizara ambazo zitakuwa zinashughulika na Sera, wanashughulika na mafunzo, wanashughulika na utafutaji wa fedha, na wanashughulika vile vile na ubora, kwa maana ya kuweka viwango kwa ajili ya waalimu wanaokwenda kufundisha katika shule hizo. Kwa hiyo ukikuta huo mkanganyiko huko ni suala tu la kuwaelimisha wanaohusika waweze kujua ni nini hasa kinatakiwa kiandikwe.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri Mkuu, lakini nina swali la nyongeza. Mambo haya wala si kuwaelimisha watu, Serikali inapaswa itoe mwongozo ili shule zote wajue wanaandika nini, haiwezekani Shule moja kwenye Wilaya hiyo hiyo, unatoka shule A hapa imeandikwa Mkoa wa Kigoma, Shule ya Msingi Kibondo, unakwenda mbele unakuta nyingine Serikali ya Kijiji. Hii ni mikanganyiko, watu hawaelewi waandike vitu gani, wala hawajijui wako wapi.

Shule hizi nimesema hawana pa kutunzia kumbukumbu, hawana bendera na vitu vingine vingi. Bendera hawajui hata wanunue wapi. Kuna watoto wanamaliza darasa la saba kwenye shule hizi hawajawahi kuona bendera za taifa. Kwa nini Serikali isiagize kwa kila mwalimu mkuu. Ni mambo ya kuagiza wala si kuelimisha, kwa nini Serikali usiagize?

Toa mwongozo watu hawa wajue, maana hawafahamu waliko. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya! Mheshimiwa Waziri Mkuu utaagiza mpaka kwako. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sasa Mkosamali, na wewe Diwani kwenye Halmashauri zako hizo, hilo nalo mnashindwa kweli kulieleza kwenye Halmashauri? Ee! maana Halmashauri ndiyo kazi yake hiyo. Lakini nakubali, tutaelekeza Mikoa na hasa Mkoa wa Kigoma, ili waweze kuhakikisha kwamba wanaliweka jambo hili vizuri. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa sababu kidogo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanza kutia *gambu***.** Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi nataka nijielekeza katika suala la utekelezaji wa Sera ya mali kale. Nazungumzia mali kale sizungumzii mali kauli. Sera ya mali kale; sera ambayo kwa kweli haijapewa kipaumbele cha kutosha na Serikali katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zina utajiri mkubwa wa mali kale, na mali kale ni moja ya eneo ambalo hutoa mchango mkubwa hususan ya kimaendeleo katika nchi, hususan katika nyanja za utalii, teknolojia, utafiti,lakini pia na elimu. Sasa, kwa sababu mali kale huwa inajumuisha utamaduni unaoshikika na usioshikika, unaohamishika na usiohamishika ambao mara nyingi unakuweko ama nchi kavu au baharini.

Lakini mbali ya hivyo ni kwamba kutokana na umuhimu wake mali kale na namna ambavyo una uwezo wa kuchangia pato la taifa, sasa mimi nataka kuelewa.

Je, Serikali yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, inachukua hatua gani za kimkakati kuhakikisha kwamba sasa eneo hili linatoa pato zuri kwa taifa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, labda nikiri tu kwamba Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, *kanibom* sana leo, mali kale, mali kale ni nini, mali nini tabu kweli. Sasa ninachoweza kusema tu ni kwamba, pengine ni suala tu la Wizara zile zinazohusika kupewa maelekezo.

Lakini mimi ninavyojua kwa kiasi kikubwa hatujapuuza eneo hilo. Ndiyo maana ukienda Zanzibar suala hilo tumelipa nafasi kubwa sana. *Actually* utalii mkubwa kwa Zanzibar kwa sehemu kubwa unatokana na sababu hizo.

Lakini mimi nakubaliana na wewe kabisa kwamba iko haja ya kuongeza uelewa kwenye eneo hili na hasa unapokuja kwenye maeneo ya Utamaduni ambao wengi hatujaupa nafasi kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi nakubaliana na wewe kabisa kwamba pengine ni nafasi nzuri Wizara ya utalii, Wizara Habari, Utamaduni na kadhalika, zijaribu kulifufua eneo hili, walipe nafasi kubwa, kwa sababu mchango wake si kwa maana hiyo tu kiuchumi, lakini kijamii zaidi nalo lina umuhimu wake wa kipekee sana. Kwa hiyo, mimi nadhani rai yako ni nzuri, pengine ni suala tu la kujipanga vizuri. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yako hiyo na maagizo ambayo umetoa kwa Wizara. Mali kale ni moja ya linaloendena vile vile na masuala ya utafiti, na mpaka sasa hivi nchi yetu bado haijawa na eneo au maabara ya kiutafiti katika suala zima la mali kale; lakini utakumbuka kwamba suala hili la mali kale ndilo ambalo vile vile linaitangaza nchi yetu kimataifa.

Kwa mfano labda nikupe, michoro ile ya miamba iliyoko Kondoa, Dodoma Vijijini, Singida vijijini, Iramba, Bukoba Vijijini, na hata kule Muleba kwa rafiki yangu kule. Lakini vile vile kama kile Kimondo ambacho kiko hapa Mbozi, lakini pia na zile nyayo za Zamadam ambazo ziko kule Olduvai.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na maagizo hayo, na hasa ukizingatia kwamba katika kipindi kilichopita waliwekewa lengo la kukusanya bilioni moja, na wameweza kulifikia lengo hilo. Hii inaonesha kwamba kwa kweli bado wana nafasi kubwa katika kuchangia katika pato la taifa. Nakubaliana na ushauri ambao umeutoa….

**SPIKA:** Haloo! Sasa mbona imekuwa hotuba nyingine?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika pamoja na Njombe, nilisahau, yako mambo ya Mali Kale…

**SPIKA:** Hiyo ni rushwa hiyo! Inaitwa rushwa ya maneno. *(Makoofi/Kicheko)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, sasa umenitoa kwenye *track* kidogo.

**SPIKA:** Hotuba! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nataka kujua, kwa sababu pato hili litasaidia taifa lakini vile vile linatakiwa lisaidie katika Halmashauri zetu.

Je, una tamko gani kwa Serikali au Wizara kuhusiana na mapato ambayo yanatokana na suala zima hili la Mali Kale kwa Halmashauri zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, wala si swali lako lakini ujibu tu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika, pengine Mheshimiwa Rajabu unataka mapato hayo tuyarudishe kwenye Halmashauri, kwa sababu kama ni mapato yako kwenye sehemu ya maduhuli ni lazima yatakuja kwenye Serikali Kuu na baadaye yatarudi kwenda kuimarisha mambo fulani Fulani katika Halmashauri. Lakini pengine tukiahirisha Bunge basi tunong'one nione hasa wazo lako lilikuwa ni nini katika eneo hili halafu tuone namna ya kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote walioomba kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu wamepewa nafasi. Nichukue nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ingawa leo maswali yenyewe yamekuwa *joggle joggle* tu, sera si sera, maswali si maswali, hayakukaa vizuri sana. *(Makofi)*

Hayakukaa vizuri sana kwa mujibu wa ile Kanuni yetu. Kwa sababu maswali ya Waziri Mkuu lazima yawe ya kisera zaidi kuliko *specific issues.* Najua kuna watu wanapenda kupinga kila kitu. Mimi nasema nakaa hapa natumia Kanuni, ndizo ninazozifuata na siyo kelele zenu.

Kwa hiyo nataka kabisa kabisa *next time* tunakuwa na maswali ambayo ni ya sera. Hapo mtapata majibu mazuri zaidi kuliko yale mnayomwuliza mambo mengine ambayo haayajui yeye mwenyewe.

Kwa hiyo, naomba msome Kanuni zetu, maana mkifanya hivi, nikiruhusu, wiki ijayo wengine watafanya vibaya zaidi. Ndiyo maana inabidi niwaambie ili mfanye vizuri zaidi kuliko mlivyofanya leo. *(Makofi)*

Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuweza kujibu maswali yote. Tunaendelea, Katibu!

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona katika kipindi hiki cha Maswali na Majibu tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Gosbert Blandes, atauliza swali la kwanza.

Na. 192

### Kuzigawa Kata za Kiriruma na Nyakahanga

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kupunguza ukubwa wa Kata na Vijiji, ili kuwapelekea wananchi Maendeleo haraka na Kata za Kiruruma na Nyakahanga ni kubwa sana na hivyo kuhitaji kuzigawanya haraka sana.

Je, ni lini Kata hizo zitagawanywa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama hivi ifuaatavyo:-

Mheshimiwa Spika utaratibu wa kugawa Kata unazingatia Kifungu cha Sheria Namba 29(3) cha Sheria za Serikali za Mitaa pamoja na (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Kifungu Namba 16(1) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura Namba 288. Utaratibu unaotumika ni kupiishwa maombi hayo katika Mikutano Mikuu ya Vijiji na baadaye maombi hayo kuwasilishwa katika Kamati za Maendeleo ya Kata.

Vilevile lazima maombi hayo yajadiliwe na kukubaliwa na Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Nyakahanga ina jumla ya watu 20,284 na Kata ya Kiruruma inakadiriwa kuwa na watu 34,945 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa maombi ya kuzigawa Kata hizo tayari yamewasilishwa kwa

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ili Baraza la Madiwani liweze kujadili pendekezo hilo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yakipitishwa na kujadiliwa katika Baraza la Madiwani, Kamati ya ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya mkoa *(RCC)* mihutasari ya vikao hivyo vya kisheria itawasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na uhakiki utafanyika kabla ya kuanzisha Kata hizo ili kujiridhisha kama maombihayoyamekidhi vigezo na taratibu zilizopo.

Aidha Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa atazigawa Kata hizo sambamba na maombi kutoka Halmashauri nyingine kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kufanyika.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ni kwamba katika majibu wa Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, atazigawa Kata hizo sambamba na maombi kutoka katika Halmashauri nyingine, kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kufanyanyika. Ninafahamu kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unafanyika mwaka huu mwezi Oktoba, 2014.

Je, ana maanisha kwamba Kata hizo atazigawa kabla ya mwezi Oktoba, 2014. Au katika Uchaguzi mwingine wa Serikali za Mitaa?

(b) Mheshimiwa Spika, nadhani ni kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Naibu Waziri hakupata taarifa sahihi. Ni kwamba tayari maombi haya yalishapelekwa katika Baraza la Madiwani, *DCC,* ilishajadili, *RCC,* imejadili na suala hili lishapelekwa mpaka TAMISEMI.

Sasa inawezekana Naibu Waziri haujapata taarifa kikamilifu. Ningelitaka kujua. Je, uko tayari kufuatilia taarifa hizi kikamilifu na ufanye uamuzi wa haraka kugawa Kata hizi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Blandes kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala kwamba majibu hayana uhakika. Lakini pia ameeleza kwamba tuanze na suala la kwanza kwamba. Nimeeleza kwamba kama taratibu zote zimekamilika sawa na Halmashauri nyingine ambazo zimeomba mabadiliko, au kugawiwa kwa vijiji au maeneo ya Kata. Maombi yote kwa sasa yako kwa Waziri mwenye dhamana.

Kwa maana hii sasa, kabla ya uchaguzi kufanyika. Chaguzi zijazo za Serikali za Mitaa majina haya yatakuwa yametoka ili kuyaingiza kwenye Mpango wa Serikali za Mitaa ujao, kwenye Chaguzi zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ambalo ni dogo. Ninamuomba baada ya kutoka hapa, tutawalisiana na Ofisi kuona Kata zako mbili mpya hizo ulizoziomba kama ziko pale kwenye Ofisi ya Waziri mwenye dhamana, ili tukupe mrejesho uweze kuweza kusubiri sasa maambuzi ya ofisi.

Lakini kama taratibu hizo bado hazijakamalika mpaka hapa kwetu, bado tutaendelea kuwasiliana na Mamlaka husika kwa maana ya mkoani, kama majina yameishafika mkoani. Kama hayafika, tutaiga tena simu Wilayani. Kuona kama Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya

yameishajadiliwa na taratibu zimekamilika, ili yaweze kuletwa kwa harakana yafike kwa Waziri mwenye dhamana tayari kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, tutaendelea kufuatilia ili kukupa taarifa halisi. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Naibu Waziri ameishasema kwamba Kata zote ambazo zina maombi yao tayari, zitatangazwa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, na mimi vilevile ningelipenda Mheshimiwa Naibu Waziri atupe uhakika kwamba Halmashauri ya Mji Mdogo wa Tunduma, ilipata Hati ya kuwa Mji kunako mwaka 2011. Hati kamili. Tulikata Kata 14, na mpaka sasa ni kwamba tumepewa Mkurugenzi na tukapewa na Halmashauri yote.

Lakini bado zile Kata 14 hazijafanyiwa kazi. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri atupe uhakika ya kwamba ni lini sasa zile Kata zetu zote 14 tulizoomba. Katika mji wa Tunduma ili uwe mji kamili. Lini mamlaka hiyo itaanza rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hilo swali lako ni *very specific,* ni lingine kabisa. Lakini Mheshimiwa Waziri kama unaliweza lijibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Silinde kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Mji wa Tunduma tuliishapeleka Mtendaji ili kuweza kuanza Mamlaka Halisi ya Mji Mdogo wa Tunduma. Lakini tatizo la pale, nikwamba kati ya Kata hizo mpaka sasa, tunaye Diwani mmoja tu wa kuchaguliwa kupitia katika chaguzi zilizopita. Kimsingi ili uanzishe mji ni lazima uwe na Madiwani wote katika Kata zote.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sasa, Kata hizi ambazo hazina Madiwani, zitaanza kuingia kwenye Mipango ya Uchaguzi ujao wakisha chaguliwa Madiwani. Zikishapata Madiwani, Mamlaka kamili inakuwa iko tayari, na vikao halisi vya kisheria vinaanza kuendeshwa na taratibu zote zitaendelea.

Kwa hiyo, kwa Kata zile ambazo hazina Madiwani, kuanza mchakato wake, baada ya kupewa ridhaa hiyo, ili sasa baada ya Uchaguzi, Madiwani hao wakishaingia, Mamlaka ikishakabidhiwa, taratibu zitaendelea kisheria. *(Makofi)*

**SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, tuendele na swali la Mheshimiwa Deusderius Mipata.

Na. 193

**Mgogoro wa Wananchi na Mwekezaji wa**

**Kampuni ya SAAFI Nkasi**

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa Vijiji vya Nkundi, Kalundi na Sintali vinavyopakana na shamba la mwekezaji wa Kampuni ya *SAAFI* wameomba Serikali kufanya mazungumzo na Mwekezaji huyu juu ya mgogoro wa ardhi unaowakosesha wana vijiji hao ardhi kwa matumizi yao:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ombi la wananchi hao?

(b) Kabla ya shamba la Nkundi kukabidhiwa kwa Mwekezaji wa sasa lilimilikiwa na Serikali na Wananchi kwa mahusiano mazuri na Serikali. Walipanda Miti ya mbao ambapo wanazuiwa kuivuna miti hiyo na mwekezaji wa sasa.

Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hawa waweze kuvuna miti yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shamba la Nkundi, lilibinafsishwa kwa Mwekezaji ambaye ni *Sumbawanga Agricultural and Animal Food Industries Company Limited*, mwaka 2003, kufuatia mpango wa Serikali wa kubinafsisha Mashirika ya Umma, Makampuni ya Mashamba yake.
Umiliki wa shamba la Nkundi kwa Kwampuni ya *SAAFI,* kwa maana ya *Sumbawanga Agricultural Animals Food Industries Company Limited,* ni halali, kwani taratibu zote za ubinafsishaji zilifuatwa hadi makabidhiano yake.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Nkundi, Kalundi na Sintali kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na vijiji vingine Chipu, Kasense, na Fyengelezya, katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, vinapakana na Shamba ambalo mwekezaji ni *SAAFI Company Limited.*

Ni kweli vijiji hivi viliomba viruhusiwa kutumia bwawa la maji ambalo, liko ndani ya shamba la Mwekezaji. Serikali ilifana mazungumzo na Mwekezaji na amekubali ardhi ambayo lilikojengwa Bwawa hilo, kabla ya shamba kubinafsishwa irejeshwe katika Serikali za Vijiji hivyo. Tayari eneo hilo limeishatengwa na kuwekekwa mipaka. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya shamba hilo kubinafsishwa, wananchi wa vijiji hivyo jirani walikuwa wanaruhusiwa na Serikali kulima katika shamba hilo lakini kwa masharti ya kutolima mazao ya kudumu, ikiwemo miti au kujenga nyumba za kudumu.

Kwa mantiki hiyo, Mwekezaji aliuziwa shamba pamoja na miti, iliyokuwemo katika Shanba hilo kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Hivyo basi Mwekezaji anamiliki shamba hilo kisheria. Maamuzi yoyote ya kutaka kuchukua sehemu ya ardhi hiyo ya Mwekezaji ni uvunjaji wa Sheria jambo ambalo linaweza kuitia hasara Serikali yetu.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mimi ninajua kwamba Mwekezaji huyu anamiliki eneo hilo kisheria.

*(Hapa Mheshimiwa Maragareth S. Sitta alikajisha baina ya Spika na Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margareth S. Sitta, ninakuomba tafadhali urudi ulikotoka.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimwia Spika, nina swali langu lililenga juu ya kuondoa mgogoro wa ukosefu wa ardhi, kwa wananchi wanaozunguka shamba hilo. Nikidhani kwamba wananchi wanapokuwa na mgogoro wa ukosefu wa ardhi, ni Serikali yao, ndiyo inayoweza kusuluhisha.

Nilitarajia kwamba Serikali ingeliweza kukutana na Mwekezaji huyo ikazungumza naye. Kwa sababu pia Mwekezaji huyu amekuwa na utayari wa kujenga mahusiano mazuri na majirani zake. Ndiyo maana wakati wa mgogoro unaoelezwa hapa wa bwawa la Maji, waliweza kukaa na kujadili na mgogoro ukaishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitarajia kwamba sehemu ambayo haitumiki, kutokana na mgogoro, wa ukosefu wa ardhi wa vijiji, pengine Serikali ingelizungumza naye, wakafikia muafaka fulani, ikiwezekana hata kulipa gharama fulani. Kwa sababu Serkali ni lazima iwahudumie wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamekuwepo na migogoro katika mashamba haya ya wawekezaji. Wapo wawekezaji ambao wanaomba mashamba ambayo hawayaendelezi, na wanayauza kwa Wawekezaji wengine. Hivi sasa ninavyo zungumza, kuna mgogoro wa mipaka kati ya Mwekezeaji aliyepo katika kijiji cha China, ambaye anaitwa Sumri, ambaye alinunua kwa Mwekezaji Hamad Slim. Sasa kuna mgogoro wa mipaka kati ya wananchi na Mwekezaji huyu. Mgogoro huu, kuanzia jana ulikuwa katika hali ngumu kidogo.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali iingilie kati, ili kuona haki inatendeka. Kama madai ya wananchi siyo sahihi, basi ione uwezekano wa kutatua mgogoro huo katika hali ambayo usije ukaleta adhari mbaya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa, ninakuomba uliza swali. Hiyo sasa imekuwa hotuba.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Je, Serikali iko tayari kuingilia kati na kuona haki inatendeka katika shambai hili lilliloko katika kijiji cha China?*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, maswali ya namna hiyo, kwa hali hiyo tutafanyia kazi maswali mawili tu kwa siku nzima.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Juu ya wananchi ambao wanakosa nafasi ya ardhi ya kulima kwa sababu ya Uwekezaji ule. Nilitaka nikujulishe ya kwamba. Mwekezaji yule ameridhia Wakulima kuingia kwenye shamba lake na kulima. Mpaka hapo taratibu zake za uwekezaji zitakapokamilika, kwa

masharti ambayo nimeyaeleza katika jibu la msingi kwamba hawaruhusiwi kulima mazao ya kudumu, kama vile kupanda miti na vinginevyo au kujenga nyumba za kudumu.

Kwa hiyo kwa kipindi hiki, kazi ambayo tumeishauri Halmashauri ni kwanza katika vijiji vilivyopo kufanya sensa ya matumizi bora ya ardhi, ili kuweza kubainisha maeneo ya kilimo na maeneo ya mifigo na makazi, ili kuwapa nafasi wananchi kujua ukubwa wa eneo lilipo kwa shughuli za kilimo ili kila mmoja apate eneo la kulima. Kwa hiyo, utaratibu huo tutaendelea kuusimamia na tutaendelea kumkumbusha Mkurugnzi akamilishe zoezi hilo huku wakipata nafasi ya kulima mazao yao kwa Mwekezaji ambaye yuko tayari na anaendelea kuwapa ushirikiano vijiji vyote vinavyozunguka eneo lile.

(b) Mheshimiwa Spika, swali la pili, linalohusu mgogoro wa Bwana Sumry na Bwana Hamad Slim, kuhusu mipaka ya maeneo ambayo wanayamiliki, hili nilitaka kukuhakikishia kuwa tutalifanyia kazi na tutakupatia taarifa ya namna ambavyo tumelishghulikia. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika ninashukuru, kwa kuwa katika Kata yangu ya Ndungu, kuna Mwekezaji ambaye ameshikilia zaidi ya asilimia kubwa ya ardhi na wala haitumii kikamilifu. Katika hali kama hii Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, amefika huko na kujionea mwenyewe hali mbaya iliyopo katika eneo hilo. Je, Serikali, leo hii inawaambia nini wananchi wangu wa Kata Ndungu, kwa sababu tatizo ni kubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hili ni swali jipya kabisa. Labda Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, atakuwa analijua.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli baada ya Mheshimiwa Anne Malecela Kilango, alipotoa maelezo ya shamba lililotelekezwa na Mwekezaji, nilichukua hatua ya kufika kule na kuona hali ilivyo. Ni kweli nilikuta ardhi iliyotelelekezwa pamoja na kwamba kuna mambo madogo madogo yanayofanyika.

Serikali inalifanyia kazi. Nilitoa ahadi kwa wananchi wa kule, kwamba hayo yote tutayafanyia kazi. Kazi hiyo inaendelea vizuri. Ninatoa matokeo ya kazi hiyo kwa Mheshimiwa Anne Kilango, na hata kwa wananchi ambao niliwaahidi nilipofanya ziara hiyo huko kwao. *(Makofi)*

Na. 194

**Waandishi wa Habari Kufanyakazi Katika Mazingira Magumu**

**MHE. MARYAM S. MSABAHA** aliuliza:-

Waandishi wa Habari hufanya kazi katika mazingira magumu sana na hatarishi na ya kuogopesha bila kuwa na Bima ya aina yoyote inayowakinga.

(a) Je, Serikali haitambui na kuthamini mchango wa Waandishi wa Habari katika kuhabarisha jamii?

(b) Je, kwa nini Waandishi wa Habari wengi hawana Bima?

(c) Je, kwa nini Waandishi wa Habari wanafanya kazi katika mazingira magumu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Msabaha, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mazingira ya utendaji kazi ya Wandishi wa Habari ni magumu na mengine ni hatarishi kama zilivyo kazi nyingine.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kudhamini mchango unaotolewa na Waadndishi wa habari nchini, katika kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha jamii. Mchango huu umesaaidia katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya taifa letu.

(b) Ni kweli waandishi wa habari walio wengi hawana Bima kwa sasa. Suala hili la Bima ni suala linalohusu maamuzi ya mtu binafsi, yaani Mwandishi wa Habari mwenyewe.

Nia ya Serikali katika Muswada mpya wa kusimamia Vyombo vya Habari unaotararajiwa kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, ni kuhakikisha kuwa inaweka sharti kwa Waajiri wote kuwawekea au kuwakatia Bima watumishi wao. Aidha, Waandishi wa Habari wa kujitegemea na wao pia watalazimika kujikatia Bima ya kufanya kazi katika mazingira hatarishi.

(c) Kazi ya Uandishi wa Habari ni kazi kama kazi nyingine zote, isipokuwa ni mgawanyo tu wa kazi na majukumu katika jamii yetu. Mwandishi wa Habari hana tofauti na Mwanajeshi, Daktari au Mwalimu.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Waandishi wa Habari kupitia kalamu zao na Kamera zao, wameweza kugundua matukio mbalimbali, yakiwemo maradhii ya watoto na kupata hata watoto wale kupelekwa India na wakarudi katika hali ya uhai.

Je, Ukiwa Naibu Waziri wa Habari, umetambua mchango wa Waandishi wale. Kama ulitambua mchango wa Waandishi wale ni Waandishi wangapi Habari ambao wamepata angalau tuzo?

(b) Kwa kuwa wenzetu katika nchi zao, wanadhamini sana Waandishi wa Habari. Hata Mwandishi wa Habari kukiwa na vita, kukiwa hakuna vita wanakuwa mara kwa mara wakihabarisha jamii.

Je, ni lini Serikali itawapatia Waandishi wa Habari Bima ya Afya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMDUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua sana mchango wa Waandishi wa Habari na inawadhamini sana. Kama nilivyojibu kwenye jibu la Msingi. Waandishi wa Habari kama alivyosema Mheshimiwa Maryam Msabaha, wametoa mchango mkubwa sana katika kuibua matukio mbalimbali kwa kutumia kalamu zao hasa wanapoandika *Investigative Stories.*

Sasa sikuelewa umesema ni Waandishi wa Habari wangapi wamepata tozo ama tuzo. Kama ni tozo hakuna Mwandishi ambaye amepata tozo.

**WABUNGE FULANI:** Amesema tuzo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNINA MICHEZO:** Ninashukuru, ni tuzo.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la tuzo nitalifuatilia (b) Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Bima ya Afya, kama nilivyosema ni kwamba hili ni suala kati ya Mwajiri na Mtumishi. Sisi tutakapokuja na ile Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari hapa.

Lengo letu ni kwamba kuwe na Bodi Maalum ambayo itakuwa inasimamia Tasnia ya Habari. Kama zilivyo Bodi za Wahasibu, na Bodi za Madaktari. Hapo ndiyo itasaidia sana Waandishi wa Habari kujua wapi wanawajibika kwenye Bodi zao. Huko sasa ni kazi ya Bodi ile kutoa maekezo kwa mwajiri ama mmiliki wa chombo cha Habari, kuhakikisha kwamba Waandishi wake wa Habari na wafanyakazi wengine kwenye ile *Media House* wanakuwa na Bima hizo.

**MHE. ZAINAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa suala la sheria ya vyombo vya habari na haki ya kupata habari imezungumzwa sana humu ndani na kwa kuwa swali la msingi limezungumzia suala la bima kwa wafanyakazi kwa maana ya waandishi wa habari. Je, haoni kwamba ni muhimu hiyo sheria ikaletwa na kipengele cha Bima kwa wafanyakazi au waandishi wa habari……

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba urudi ulikotoka! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Vullu endelea.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali haioni kwamba umuhimu wa kuileta hiyo sheria haraka sana na kipengele cha bima kikawekwa iwe ni sehemu ya sheria badala ya kutegemea hiyo bodi itakayoundwa maana bodi wanaweza wakakubali au wakawa hawaipi uzito wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, suala la kuletwa kwa sheria ya kusimamia vyombo vya habari hapa Bungeni limeshazungumzwa karibu mara nne au tano, wewe mwenyewe umetoa maelekezo, tuanchosubiri sasa ni utekelezaji tu kuletwa hapa Bungeni hiyo sheria na ninaamini sisi Wabunge ndiyo tutakaotunga hiyo sheria na tutakapotunga hiyo sheria basi kipengele cha bima tuone umuhimu wake. Mheshimiwa Vullu nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Bulaya.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya pande mbili kwamba waandishi wa habari hawatimizi wajibu wao kwa ku-*balance story*. Lakini pia upande mwingine upande mwingine kumekuwa na malalamiko sana kwa

upande wa Serikali kutotoa taarifa pindi waandishi wa habari wanapozitaka na hivyo kuchangia tatizo la kuto-*balance story*.

Sasa mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba anatoa tamko gani kwa Maafisa Habari wa Wizara ambao hawatoi ushirikiano kwa Waandishi wa Habari pindi wanapotaka habari nakuondoa kabisa tatizo la kuto-*balance story* na kuandikwa *story* za upande mmoja?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujbu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Bulaya ambaye bahati nzuri naye pia ni mwandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kati ya habari na hadithi, habari yoyote lazima iwe na *five W's and H,* kama haijakamilisha vigezo hivyo sita inakuwa ni hadithi na inakuwa siyo habari.

Kwa upande wa Serikali tumeshatoa maelekezo kwamba Maafisa Habari wote kupitia Idara ya Habari Maelezo wawe wanatoa taarifa kwa waandishi wa habari ili kuwe na *balanced stories* kati ya upande mmoja na upande mwingine. Nitumie fursa hii pia kuwaomba Maafisa Habari wa Wizara zetu waendelee kutoa habari kwa waandishi wa habari kama ambavyo wamekuwa wakifanya. *(Makofi)*

Suala la kuwep kwa malalamiko kwamba kunakuwa na habari ambazo siiyo *balanced,* mwandishi anafikia hatua anakosa upande mmoja kwa hiyo anaamua kuandika ile habari ili ule upande mwingine uweze ku-*react,* lakini ni kitu ambacho tunaamini kwamba tutakapokuwa tumefuata utaratibu ambao umeelekezwa na Idara ya Habari Maelezo kwamba hata Wizara zetu zina muda maalum wa kwenda kutoa taarifa Idara ya Melezo, utaratibu ambao umepangwa. Kwa hiyo, naamini kwamba hili suala la kutokuwa na *balanced stories* halitakuwepo tena.

**SPIKA:** Ahsante, naomba tuendelee na Wizara nyingine, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Augustino Masele atauliza swali hilo.

Na. 195

**Mahitaji ya Zana za Kilimo na Nyumba Gereza la Kanegere**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Wilaya ya Mbogwe ina Gereza moja la Kanegere linalojishuhulisha na shughuli za kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipatia Gereza hilo zana za kilimo hasa trekta?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba mpya za askari na kukarabati zilizochakaa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza kwa kutumia bajeti inayotolewa na Serikali inajitahidi kuboresha mashamba ya kilimo kwa kuyapatia vitendea kazi mbalimbali zikiwemo zana za kilimo kama vile matrekta, *power tiller* na zana nyingine. Gereza la Kanegere linajishughulisha na kilimo cha mpunga, mahindi na mihogo. Kwa sasa gereza hili lina *power tiller* mpya iliyonunuliwa mwaka 2010 na pampu ya maji kwa ajili ya umwagiliaji. Zana zaidi za kilimo likiwemo trekta zitanunuliwa na kupelekwa katika gereza hili kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wake wa kujenga nyumba mpya za askari, kuzifanyia ukarabati na kukamilisha nyumba ambazo ujenzi wake haujakamilika kwa awamu kadri fedha zinavyopatikana kila mwaka. Lengo hasa ni kuwapa makazi bora askari nchi nzima wakiwemo askari kwenye Gereza la Kanegere.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masele swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba pale Kanegere kuna *power tiller* moja, *power tiller* kulima mihogo, mpunga na mahindi naona kwamba hawajawatendea haki. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kupeleka trekta katika Gereza hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu Wilaya ya Mbogwe ni Wilaya mpya, kuna matatizo mengi pia katika Jeshi la Polisi, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atatembelea Wilaya hii ili aweze kujionea matatizo ya vyombo hivi vya ulinzi na usalama ili aweze kuyapatia utatuzi matatizo yaliyopo huko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Masele kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba *power tiller* inapata taabu sana hasa kwa sababu udongo wa pale ni mfinyanzi, lakini tunaendelea kuitumia hivyo hivyo kwa sababu hatuna njia mbadala ya urahisi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, pia nimuhakikishie Mheshimiwa Masele kwamba katika utafutaji wa matrekta kwa ajili ya kilimo katika Jeshi la Magereza tutahakikisha kwamba tunatenga moja kwa ajili ya kituo hiki cha kilimo hali itakavyoruhusu.
Kuhusu kufanya ziara nipo tayari mimi na yeye tukikualiana siku muafaka.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sanya, swali la nyongeza.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa SUMA JKT kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kudhaminiwa na Hazina walipata mkopo wa matrekta kutoka India ya dola milioni 40 na kama nina kumbukumbu sahihi SUMA JKT kupitia Wizara ya Ulinzi walikubaliana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuwakopesha matrekta zaidi ya 100 ili yapelekwe katika magereza mbalimbali walau kulima na kukidhi haja kwa chakula chao wanachokitumia magerezani.

Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ilichukua hatua gani kukopa matrekta au kuuziwa matrekta wakati Wizara ya Ulinzi ilikuwa tayari kuwakopesha Wizara ya Mambo ya Ndani matrekta idadi wanayotaka ili kuyasambaza katika Magereza haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI A MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na *offer* ya mkopo wa matrekta ya SUMA wakati ule, lakini lazima niseme kwamba mashauriano kwa ajili ya kuwezesha kuyakopa matrekta hayakukamilika hasa katika tatizo la matrekta ndiyo yatapatikana 100 lakini bajeti ya Magereza haiwezi kupata mafuta. Kwa hiyo, kukawa na mzunguko ambao haukumalizika, lakini tunajiandaa tunasikia kwamba SUMA JKT wanaleta matrekta mengine na sisi tunapeleka maombi wa kwanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema, swali la nyongeza.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, katika magereza yetu nchini kuna wafungwa wengi sana ambao wamefungwa kwa makosa madogo madogo ya mwaka mmoja au miwili mpaka mitatu ambayo mahakamani kimsingi walikosa faini kati ya shilingi 20,000/= hadi 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa Serikali isione wajibu wa kuwalipia faini wafungwa wale na kuwapa kazi nyingine za maendeleo ya jamii kwa ajili ya fidia ya kifungo hicho cha ndani?

**SPIKA:** Ningejua nisingekupa nafasi maana hilo ni swali lingine kabisa. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDAN YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Waziri Kivuli kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna watu ambao walishindwa kulipa faini ndogo na wako magerezani, lakini kinyume na kufuata sheria za kukata rufaa tunachofanya ni kutazama sheria zetu kama za *community service* au za kifungo cha nje zinavyoweza kuruhusu. Lakini magereza ni chombo ambacho kinaamrishwa na mahakama kwamba hawa wawafunge na hawa wawaweke hapa mpaka itakapotoa agizo lingine.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yote yakimalizika basi wanaweza wakaachiliwa kwa urahisi, lakini urahisi wa kukusanya faini kwa Serikali siuoni kwa sababu faini au kifungo ni hukumu kwa mtu ambaye alifanya kosa kinyume cha taratibu pengine kaikosea jamii au vinginevyo. Kwa hiyo, Serikali ambayo ni sehemu ya jamii ikiwalipia ni sawasawa na kuwa hatutaweza kudhibiti tena uhalifu kwa sababu watajua Serikali itakuja tena.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed atauliza swali hilo.

Na. 196

**Mkakati wa Kuzuia Unyanyasaji kwa Wanawake**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Utafiti wa USAID mwaka 2013 unaonyesha kuwa 40% ya wanawake wote wamepata matatizo ya kutenzwa nguvu (kubakwa) au vipigo na katika hao 44% ya wanawake wote walioolewa wamepata yote ya kubakwa na vipigo:-

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti kwa kuzuia unanyaysaji wa wanawake ambao huwaathiri sana kisaikolojia?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na unyanyasaji wa wanawake na ukatili wa kijinsia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imesaini na kuridhia mikataba, itifaki, maazimio na matamko mbalimbali yanayohusu kupiga vita unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake katika ngazi za kimataifa, kitaifa na kikanda.

Pamoja na kusaini na kuridhia Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba, itifaki, maazimio na matamko hayo.

Mheshimiwa Spika, mfano, Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia wa mwaka 2001 – 2015, Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukeketaji 2001-2015, kutunga sheria ya makosa ya kujamiiana SOSPA ya mwaka 1998, Kampeni ya Sema Hapana kwa Ukatili Dhidi ya Wanawake yaani *Say No to Violence Against Women* iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Mei, 2008, Kampeni ya Kuondoa Ukatili wa Kingono na Kijinsia yaani *Zero Tolerance on Women* ambayo ni kampeni iliyoazimiwa na Marais wa Maziwa Makuu na kadhalika.

Aidha, Wizara yangu imewezesha uundaji wa Kamati ya Kitiafa ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Wajumbe wa Kamati hii wanatoka katika Wizara mbalimbali, Jeshi la Polisi, Taasisi za Kijamii, Taasisi za Kidini na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kamati hii huwa inakutana kila baada ya miezi mitatu na kufuatilia mipango mbalimbali ya kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikiwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kutokomeza ukatili na unyanyasaji wa wanawake kupitia kampeni mbalimbali za kikanda, programu mbalimbali za redio na televisheni, semina na warsha zitolewazo kwa nyakati mbalimbali.

Pia Serikali imeweka mazingira mazuri kwa taasisi na wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kupiga vita ukatili wa kijinsia. Taasisi hizo zinatoa ushauri wa kisheria na matunzo kwa waathirika wa ukatili. Jitihada za makusudi zimechukuliwa na Serikali kuanzisha Madawati ya

Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi ambavyo vinashughulikia kesi za ukatili wa kijinsia na watoto.

Hadi kufikia Disemba 2013 jumla ya Madawati ya 417 yameshaanzishwa nchini. Aidha, masuala yanayohusu ukatili wa kijinsia yameingiwa katika mitaala ya Vyuo vya Polisi.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Rukia Ahmed, swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa yapo makabila nchini ambayo mwanamke kupigwa ni kitu cha kawaida tamaduni zao zinaona kuwa mwanamke kupigwa ni kitu cha kawaida, mwanamke ambaye hajatahiriwa hana thamani katika jamii hizo.

Je, kwa kutambua nafasi ya mwanamke katika Taifa hili Serikali iko tayari sasa kupiga vita tamaduni hizi ambazo zinadhalilisha na kumtesa mwanamke?

Pili, kwa kuwa zipo sheria kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, zipo sheria, mikataba na itifaki mbalimbali zilizoridhiwa na Serikali ambazo zinapiga vita unyanyasaji wa wanawake, lakini sheria hizi hazitambuliki huko vijijini ambako matukio haya yanatokea.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha kuwa sheria hizi zinatafsiriwa kwa lugha nyepesi na kupelekwa vijijini ambapo wanawake wanateseka na tamaduni hizi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed kwa kujali masuala ya mila zilizopitwa na wakati yaani mila potofu ambazo zinajumuisha masuala ya kupiga wanawake na masuala ya ukeketaji kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka sheria madhubuti kabisa na kuhakikisha kwamba masuala ya kupiga vipigo vya aina yoyote ndani ya ndoa na nje ya ndoa ikiwa ni pamoja na masuala ya ukeketaji ni makosa ya jinai na hatua kali zinachukuliwa.

Pamoja na hatua hizo maeneo ambayo kumekuwa na ukeketaji wale waliokuwa wanafanya masuala ya ukeketaji wamekuwa wakitafutiwa shughuli mbadala za vikundi ili vipate kuwapa vipato maana baadhi ya maeneo walikuwa wanafanya shughuli hizo wakiamini wanapata kipato kwa kufanya lile tendo la ukeketaji. Kwa hiyo, shughuli mbadala wametafutiwa wale wazee waliokuwa wanafanya masuala ya ukeketaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya kuelimisha maeneo ambayo hawazijui sheria hizi, Wizara yangu imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kupitia redio lakini pia tuna Maafisa Maendeleo Jamii katika kila Halmashauri na katika kila kata ambao wamekuwa wakishiriki kikamilifu kutoa elimu ili maeneo mbalimbali wajue mila potofu hazipaswi kutendeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maida, swali la nyongeza.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitendo hivi ni vya kikatili na vimekuwa vikiendelea siku hadi siku nchini kwetu hadi kufikia kiwango hicho kwa sasa. Je, Serikali ya Tanzania ipo tayari kutoa tamko sasa kwa sababu suala la semina na elimu limeshapitwa na wakati kwa sasa, kutoa tamko maalum la kukomesha kabisa hali hii kama vile ilivyotokea nchini India na kukomeshwa kabisa kwa kutangaza kwamba baada ya kutokea kitendo hicho kutoa tamko na hukumu kwa atakayekamatwa kufungwa kifungo cha maisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida pacha wangu kama ifuatavyo:-

Kimsingi kuhusu matamko Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imekuwa ikitoa matamko mbalimbali dhidi ya ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali na tamko la mwisho lilikuwa ni lile tamko la kukemea unyanyasaji dhidi ya wanawake na hata kuwaweka watoto kwenye maboksi.

Kwa hiyo, Wizara yangu imekuwa makini sana na kukemea suala hili, lakini pia Sheria ya Makosa ya Kujamiiana inaeleza wazi kwamba, namna yoyote ya ukatili wa masuala ya kujamiiana kwa wanawake kifungo chake ni miaka 30 au kifungu cha maisha. Kwa hiyo, Wizara ipo makini sana na suala hili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa na mimi kuuliza swali moja la nyongeza.

**SPIKA:** Wanasema kule kwao ndiyo wanaopigwa ili…*(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kiujumla unyanyasaji wa wanawake siyo tu kupigwa na kukeketwa, lakini pia tumeshuhudia kuna aina mbalimbali za unyanyasaji kama vile unakuta akina baba wanawabaka watoto wao waliowazaa, unakuta wanawake huko vijijini wananyanyaswa kisaikolojia, maana yake wengine ni bora hata umpige kuliko kumsimanga na manyanyaso mengine mengi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo kubwa ni kwamba wanawake na watoto vijijini hawana elimu. Ningependa kujua ni jitihada zipi zinafanywa na Serikali kuweza kutoa elimu kwa hawa akinamama hasa maeneo ya vijijini ili waweze kujua haki zao kana kwamba wakitendewa ndivyo sivyo waweze kwenda kwenye hayo Madawati ya Kijinsia mliyoanzisha?

**SPIKA:** Ahsante na wanaume nao wapewe elimu lakini.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la unyanyasaji wa kijinsia lipo nchini na takwimu zinaonesha kwamba kupitia Madawati yetu ya Kijinsia Kitaifa takribani makosa 6,000 nchini yameripotiwa katika kipindi cha mwaka 2013 na kwa hapa Dodoma Kituo cha Polisi cha Manispaa ya Dodoma makosa ya ukatili hususan kubaka yameripotiwa makosa 71 katika kipindi cha mwaka 2013 nilipotembelea nilithibitisha hilo.

Kwa hiyo, vijijini kimsingi Watanzania wote tunatakiwa tuelewe kwamba masuala ya kubaka ni makosa ya jinai na tuna mikataba mbalimbali ambayo tumeisaini ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Kuzuia aina zote za Unyanyasaji dhidi ya Wanawake na Watoto unaitwa CEDAW ambao tumeusaini mwaka 1979 na nchi yetu imeridhia mwaka 1980.

Kwa hiyo, vijijini kule hadi katika kata wale Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii, wamekuwa ni sehemu ya kwanza ya kupokea changamoto hizo na baada ya hapo wanakwenda kutoa ripoti katika Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, makongamano na mikutano vimekuwa vikifanyika. Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka imekuwa ni sehemu pia ya kuelezea masuala ya ukatili wa kijinsia.

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wa maswali umepita sana, sana, sana. Kwa hiyo nitambue tu wageni tulionao.

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu ambao ni kutoka Kanisa la Kisabato Marekani wakiongozwa na Ndugu Douglas Sue Schoch, *can you rise wherever you are! The five others too should rise up*. *You are welcome and we are happy to see you here. Thank you very much*.

Tuna wageni sita kutoka Kanisa la Kisabato la Dodoma na Dar es Salaam wakiongozwa na Mwinjilisti Matola Lumbe na Bi. Suzan Ngusa, tunaomba msimame mlipo. *Okay,* ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine 10 wa Mheshimiwa Gaudence Kayombo ambao ni wanachuo wa Mkoa wa Ruvuma kutoka Vyuo vya St. John, Chuo cha Mipango na UDOM. Hawa wenyewe wako wapi, wasimame. Ahsante sana, tunashukuru na msome kwa bidii.

Tuna wageni wengine 67 wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambao ni wanafunzi wa vyuo mbalimbali vilivyopo Dodoma kutoka jimboni kwake. Basi msimame mlipo nyie wanafunzi wote wa kutoka huko. Ahsante sana, msome sana. Kule kwao wanamuita Mawe Matatu, kwa hiyo, mjue hivyo.

Pia tuna wageni wengine 27 wa Mheshimiwa John Mnyika ambao ni viongozi na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutoka Kata ya Nzuguni, hii nafikiri ni Dodoma. Wapo wapi hawa watu 27? Aah, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine wamepewa kazi ya kupiga makofi tu. *(Makofi)*

Jamani matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.30 mchana watakuwa na kikao chao chumba Na. 227.

Nina tangazo lingine la Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba leo saa 5.00 kutakuwa na kikao cha Kamati kujadili Azimio la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Fedha na Uwekezaji *(The SADC Protocol on Finance and Investment)* na Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hiki kikao chao ni saa 5.00 lakini kitakuwa Hazina Ndogo, chumba Na. 125. Naomba Wajumbe wa Kamati hii niwaruhusu waende caa 5.00 baada ya kuahirisha hapa kwa sababu kazi wanayotakiwa kuifanya ni ya kesho. Kwa hiyo, waende.

Mwenyekiti wa APNAC, huu ni Umoja wa Wabunge wanaopambana na mambo ya rushwa, Mwenyekiti wake ni Dkt. Mary Mwanjelwa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati

Kuu ya APNAC Tanzania kuwa leo tarehe 05 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo. Kwa hiyo, ni Wajumbe wa Kamati Kuu ya APNAC.

Halafu Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Marafiki wa Mazingira (TAPAFE) Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, anaomba niwatangazie Wajumbe wa chama hicho kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao ambacho kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Katibu tunaendelea.

**HOJA ZA SERIKALI**

**AZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Kubadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kuwa Taasisi Inayojitegemea Kiutendaji (Tengeru Institute of Community Development Establishment Order 2013)**

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo kuchangia ni dakika 10 kwa sababu ile nyingine ilihusu mambo ya Bajeti. Kwa hiyo, watakaoomba kuchangia wajue watachangia dakika 10. Haya mtoa hoja endelea.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshiniwa Spika, kwa niaba ya Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi naomba kuwasilisha Bungeni Azimio la kukibadili Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru *(Community Development Training Institute – Tengeru)* kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji yaani *Tengeru Institute of Community Development* kwa kutumia Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili lililopo mbele yako linapendekeza kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii *Tengeru (Community Development Training Institute -Tengeru)* kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili ni kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Sura ya 129 Kifungu cha 6(1) ambacho kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu kutangaza kuwa Chuo au Taasisi yoyote ya ufundi ambayo imepata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kuwa Chuo Kikuu au Taasisi inayojitegemea kiutendaji.

Aidha, kifungu cha 6(3) kinamtaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu kuwasilisha Azimio mbele ya Bunge ili kuridhia tamko *(Establishment Order)* la kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili ni matokeo ya jitihada za muda mrefu za Serikali kukiwezesha Chuo kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuzishukuru Kamati za Kudumu za Bunge za Huduma za Jamii na Maendeleo ya Jamii kwa maoni na mchango wao mkubwa ambao umechangia sana kuboresha tamko la kuanzisha taasisi hii na kuwezesha Azimio kuwa tayari kuwasilishwa

mbele ya Bunge kwa ajili ya kuridhiwa. Aidha, napenda kuwashukuru wadau mbalimbali na wataalam wetu walioshiriki katika mchakato wa kuandaa azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika harakati za kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania imeweka kipaumbele katika kuwajengea wananchi uwezo wa kuainisha matatizo yanayowakabili katika maeneo yao na kuwajengea uwezo wa kuyatatua wenyewe. Aidha, msisitizo umewekwa zaidi katika dhana ya jamii kuweza kubuni, kusimamia na kuendesha miradi na programu mbalimbali za maendeleo ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo kutokana na mabadiliko ya haraka ya kiuchumi, utandawazi na sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 na Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, Serikali imeendelea kuimarisha vyuo mbalimbali vya maendeleo ya jamii vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada na Astashahada kama vile Buhare, Monduli, Mabughai, Rungemba, Ruaha, Misungwi, Mlale na Uyole. Kuimarishwa na kuinua ubora wa vyuo hivi ni hatua za makusudi kabisa zenye lengo la kuwapata wahitimu watakaojiunga na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa mafunzo ya Shahada.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kutoa maelezo mafupi kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru *(Community Development Training Institute-Tengeru)*.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilianzishwa mwaka 1963 kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Mabwana na Mabibi Maendeleo kwa ajili ya kuhamasisha jamii na hivyo kujiletea maendeleo. Tangu wakati huo Chuo kimepitia hatua mbalimbali mpaka sasa ambapo kinatoa mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika fani za Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Maendeleo na Upangaji na Uendeshaji Shirikishi wa Miradi baada ya kupata ithibati kamili toka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika chuo hiki tangu kuanzishwa kwake, imekuwepo haja na ulazima wa kuangalia upya mfumo wa uendeshaji na utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii kwa kuzingatia ushindani uliopo katika utoaji wa mafunzo na mahitaji ya soko la wataalam.

Mheshimiwa Spika, katika kukiimarisha chuo hiki ili kiweze kujitegemea kiutendaji, Serikali kwa sasa imeelekeza nguvu zake katika kukarabati na kujenga majengo pamoja na miundombinu mingine ikiwemo upanuzi wa maktaba na mfumo wa teknolojia ya mawasiliano.

Aidha, Serikali inagharamia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa chuo. Mathalani, walimu watatu wapo katika mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na walimu watano katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu ambapo wawili wapo katika hatua za mwisho za kumalizia mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 na matakwa ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ya mwaka 1997 inayoelekeza bayana kuanzishwa kwa taasisi zinazojitegemea kiutendaji, ni wakati sasa wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kupewa uwezo wa kubuni na kutoa maamuzi ya haraka ya utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo. Kwa kujitegemea kiutendaji, chuo kitakuwa na nafasi kubwa ya kupanua na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na programu ya sasa ya Serikali ya kuwa na shule ya sekondari kila kata, kumekuwepo ongezeko kubwa la mahitaji ya nafasi za kujiunga na vyuo.

Hivyo basi, inapendekezwa kuwa muundo wa sasa wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ubadilishwe na kuwa Taasisi inayojitegemea ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yanayozingatia mahitaji halisi ya sasa na kuendelea kutoa mafunzo yanayozingatia umahiri katika ngazi za shahada.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Chuo hiki kinachojitegemea kutaongeza changamoto kwa vyuo na taasisi nyingine hivyo kuchochea ushindani wa vyuo.

Pia chuo kitaimarisha uhuru na uwajibikaji kiutendaji katika kuamua, kutekeleza na kusimamia majukumu yake. Hii itakwenda sanjari na chuo kuweza kubuni mipango mbalimbali ya maendeleo inayolenga kukiongezea mapato na kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kusoma Azimio lenyewe la kuridhia kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kada ya watumishi wa maendeleo ya jamii ni muhimu katika kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya Serikali katika kuondoa umaskini kwa wananchi;

NA KWA KUWA katika Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129 Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu amepewa mamlaka ya kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Chuo chochote kinachotoa Elimu ya Ufundi kuwa chuo kinachojitegemea baada ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kuzingatia mambo muhimu kuhusu chuo hicho;

NA KWA KUWA Baraza limethibitisha kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru kinafaa kujitegemea kiutendaji na limemshauri Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu kutangaza chuo hicho kujitegemea kiutendaji, na kwa kuzingatia misingi hiyo chuo kimetangazwa katika Gazeti la Serikali Namba 9 la tarehe 25/01/2013;

NA KWA KUWA Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 inatamka bayana kwamba ili kuviwezesha Vyuo vya Ufundi na Taasisi za Ufundi kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, ni vyema vikajitegemea kiutendaji;

NA KWA KUWA Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru ili hatimaye kiweze kujitegemea kiutendaji, imeelekeza nguvu zake katika kuboresha miundombinu na mazingira ya kutoa mafunzo kwa kujenga na kukarabati majengo ikiwemo maktaba ya kisasa na kumbi za mihadhara. Aidha, Wizara imeendelea kugharamia mafunzo ya walimu wa Chuo hicho katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na wengine katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu;

NA KWA KUWA watumishi wengine wasio walimu wamepelekwa katika mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wao kwa lengo la kukiwezesha chuo kutoa mafunzo na elimu ya ufundi yaliyo bora;

NA KWA KUWA bado kuna hitaji la wataalamu wa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kuunganisha wananchi, Serikali na wadau wengine wa maendeleo;

NA KWA KUWA uimarishaji wa utoaji wa mafunzo utazalisha wataalamu wa maendeleo ya jamii wenye mwelekeo na vitendo zaidi kuliko nadharia na wenye kukidhi matakwa na mahitaji ya soko la ajira;

HIVYO BASI kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129, ninaomba sasa Bunge liridhie na kukubali Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru *(Community Development Training Institute - Tengeru)* kiwe Taasisi inayojitegemea kiutendaji na kupewa jina la Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru *(Tengeru Institute of Community Development)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Ninyi watu wa *front* mmekaa chini wakati hoja inatolewa? Watu wa *front desk* yaani mmekaa chini wakati hoja inatolewa.

**WABUNGE FULANI:** Wametimia.

**SPIKA:** Kutimia siyo hoja, wame–*share* watu wengi hawa. Hoja imeungwa mkono, sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika.

**MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa taarifa kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, natumia nafasi hii kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kujitegemea kiutendaji, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuiletea Kamati yangu jukumu la kujadili Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji tarehe 24 Oktoba 2013, Kamati ilikutana Dar es Salaam na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikiongozwa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Philipo Mulugo (Mb) ili kupata maelezo na ufafanuzi kuhusu hoja hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Kamati ilielezwa kwamba Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ambacho ni mojawapo ya Vyuo vya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kilianzishwa mwaka 1963 ili kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii *(Community Development Officers)* ya kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo.

Aidha, mwaka 1983 Chuo kilianza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu *(Advance Diploma)* katika fani ya Maendeleo ya Jamii na kimeendelea kupanua wigo wa utoaji mafunzo katika fani mbalimbali zikiwemo za jinsia na maendeleo na upangaji na uendeshaji shirikishi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Chuo kilisajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(The National Council for Technical Education - NACTE)* ili kutoa mafunzo ya Shahada (*Bachelor*

*Degree*) ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, mwaka 2012 Chuo kilianza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili *(Post Graduate Diploma)* katika fani ya maendeleo ya jamii. Hivyo Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa sasa kinatoa mafunzo ya Shahada na Stashahada ya Uzamili katika fani ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la shule za sekondari nchini linaloambatana na uwepo wa wahitimu wengi wa elimu ya sekondari, kumekuwa na ongezeko kubwa la uhitaji wa mafunzo yanayohitaji utendaji kazi kwa ufanisi *(competence based)* ili kumwezesha mhitimu kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia na utandawazi. Muundo wa Chuo uliopo haukidhi ongezeko la wanafunzi wanaomaliza elimu ya sekondari na hata wahitimu wa vyuo vikuu wanaohitaji fani zinazohusiana na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 inaelekeza kuanzishwa kwa taasisi zinazojitegemea kiutendaji ili kuharakisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taasisi ikiwemo kupanua na kuboresha elimu itolewayo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani za maendeleo ya jamii zenye uhitaji mkubwa kwa jamii, ni muhimu kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji ili kuwa na uwezo wa kuboresha mazingira ya utoaji elimu katika mafunzo husika.

Mheshimiwa Spika, lengo la Azimio hili ni kubadili Chuo ili kukiwezesha kujitegemea kiutendaji na kukipa uwezo zaidi wa kujisimamia katika kupanga na kufanya maamuzi yake katika azma ya kupanua na kuboresha utolewaji wa mafunzo katika fani za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, iwapo Bunge litaridhia Azimio hili, Chuo kitapata manufaa yafuatayo:-

Kwanza, kitaweza kubuni mipango na miradi mbalimbali itakayolenga kuongeza mapato ya Chuo, hali itakayosaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia uendeshaji wake.

Pili, kitaweza kuongeza udahili wa wanafunzi kwa kuanzisha programu mbalimbali zinazohusiana na mafunzo katika fani za Maendeleo ya Jamii kulingana na mahitaji ya jamii. Aidha, Chuo kitaweza kuanzisha matawi mengine ya utoaji mafunzo katika fani za Maendeleo ya Jamii nchini.

Tatu, kuwa na mamlaka kamili ya kuingia mikataba na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuboresha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Chuo ikiwemo kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu.

Nne, kitaweza kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya Chuo kulingana na uhitaji.

Tano, ni kuwa katika nafasi nzuri ya kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kutoa huduma mbalimbali kwa jamii hususan katika kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu *(consultancy)*.

Sita, kuweza kujitangaza zaidi ndani na nje ya nchi hususan katika Nchi za Afrika Mashariki na Kati kama Chuo pekee kinachotoa taaluma katika fani za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya aliyekuwa Naibu Waziri, Kamati iliona umuhimu wa kufanya ziara ya kikazi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ili kujiridhisha na mazingira ya utoaji elimu.

Aidha, Kamati ilifanya kazi yake kwa kuzingatia mambo muhimu katika uendeshaji wa Chuo kinachotoa mafunzo katika ngazi ya Shahada na Stashahada ya Uzamili. Mambo hayo muhimu ni pamoja na:-

Kwanza kupata taarifa ya Ikama na Taaluma za Wakufunzi *(Academic Staff)* na Idara ya Utawala *(Administrative Staff)*.

Mheshmiwa Spika, pili, kupitia Mitaala ya Mafunzo *(Training Curriculum)* iliyothibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)*.

Tatu, kupata taarifa za aina za mafunzo yatolewayo *(Training Programmes)*.

Mheshimiwa Spika, nne, kupitia miongozo ya ufundishaji na utahini.

Tano, kupata taarifa za taaluma za watahini wa nje *(external examiners)*.

Sita, kukagua miundombinu (*facilities)* ya Chuo ikiwemo maktaba, maabara, madarasa, kumbi za kufundisha *(theatre halls)*, nyumba za wakufunzi, na mabweni ya wanafunzi.

Saba, kupata taarifa ya sera ya Chuo kuhusu tafiti na mipango ya kuendeleza watafiti na nane, kupata taarifa ya huduma za ushauri *(consultancy)*.

Mheshimiwa Spika, katika ziara husika, Kamati pamoja na mambo mengine ilibaini changamoto mbalimbali zinazohitaji kutafutiwa ufumbuzi mapema iwezekanavyo, ili kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu.

Kwanza, ni kutokamilika kwa ujenzi wa jengo la maktaba yenye uwezo wa kutoa huduma kwa wanafunzi 200 kwa mara moja.

Pili, mradi wa ujenzi wa jengo hili ulianza mwaka 2008 na kutokamilika kwake kunatokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo pamoja na mambo mengine inahudumia vyuo 64 kikiwemo hiki Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Tatu, ni uhitaji wa ongezeko la ardhi kuwezesha Chuo kupanua utekelezaji wa shughuli zake. Kwa sasa Chuo kinamiliki ardhi yenye ukubwa wa hekta 20, na kina uhitaji wa jumla ya hekta 40 kutekeleza majukumu yake. Aidha, miliki ya ardhi ya Chuo pia ni changamoto kwa sababu ardhi hiyo iko chini ya Umiliki wa Jumla wa Chuo cha Mifugo cha Wizara ya Kilimo na Ushirika.

Nne, miundombinu chakavu ikiwemo nyumba za wafanyakazi, baadhi ya madarasa na jengo la utawala ambayo imejengwa tangu mwaka 1963.

Tano, ni ufinyu wa bajeti kutokana na kiasi kidogo cha fedha za ruzuku kutoka Serikalini kulingana na mahitaji. Aidha, chanzo kikuu cha mapato ya Chuo kinatokana na ada za wanafunzi.

Sita, sifa za kitaaluma za uongozi wa chuo pamoja na wakufunzi kutokidhi vigezo vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwani hakuna mtumishi wa Chuo hicho mwenye elimu ngazi ya Shahada ya Uzamivu yaani *Ph.D.*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maandalizi ya awali ya kukiwezesha Chuo kujitegemea kiutendaji pamoja na changamoto zilizopo kwani hatua hii itakiwezesha Chuo kukabiliana na changamoto zinazoambatana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Kamati kwamba utekelezaji wa Azimio hili utakuwa wa ufanisi katika kuboresha mazingira ya utoaji elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi wa hoja zote muhimu kuhusu utekelezaji wa Azimio uliotolewa, Kamati inakubaliana na Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji, hoja ambayo faida zake zimebainishwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ni kuwa kwanza Serikali iandae mkakati mahususi wa kuajiri na kuwatumia Maofisa maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata ili kuharakisha maendeleo katika makundi mbalimbali ikiwemo ya vijana, wanawake, wakulima, wafugaji na wajasiriamali kwani kwa hali iliyopo Maafisa Maendeleo ya Jamii hufanya kazi katika ngazi za Wilaya.

Pili, Serikali ikamilishe ujenzi wa maktaba ya chuo mapema iwezekanavyo kwa kutenga takribani kiasi cha shilingi bilioni moja kukamilisha ujezi huo na tatu, hatua hii itawezesha wanafunzi 200 kupata huduma hiyo kwa wakati moja.

Nne, juhudi za makusudi zichukuliwe kuwezesha upatikanaji wa hatimiliki ya ardhi ya chuo ikiwemo kugawa eneo hilo lenye jumla ya hekta 387 linalomilikiwa na Chuo cha Mifugo cha Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, ugawaji wa eneo uzingatie uhitaji wa Chuo hiki cha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Tano, Serikali ikarabati miundombinu ya chuo iliyojengwa tangu mwaka 1963. Aidha, Chuo kijenge jengo la utawala na kuongeza mabweni na madarasa kwa ajili ya wanafunzi ikiwemo wa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili.

Sita, sifa za kitaaluma za uongozi wa juu wa chuo na wakufunzi kwa mujibu wa Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kizingatiwe. Kwa mujibu wa NACTE sifa za kitaaluma za Mkuu wa Chuo ni Profesa au Profesa Mshiriki *(Associate Professor)* na sifa za Makamu Mkuu wa Chuo ni Mhadhiri Mwandamizi mwenye elimu ngazi ya Shahada ya Uzamivu.

Saba, ni kutokana na sifa za kitaaluma za uongozi wa chuo na wakufunzi kutokidhi vigezo vya NACTE vya kutoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili, ni vyema Serikali itoe muongozo wa kubadili utoaji wa mafunzo katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili na hivyo kwa sasa Chuo kibaki na utoaji mafunzo katika ngazi ya Shahada.

Nane, chuo kitangaze shughuli zake kwa umma ikiwemo fani mbalimbali zitolewazo kama vile utafiti pamoja na huduma ya ushauri. Hatua hii itawezesha kusajili wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na kutoa huduma stahiki kwa mujibu wa majukumu ya msingi ya chuo.

Tisa, chuo kibuni miradi mbalimbali itakayoongeza pato la chuo kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali, ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, na kumi, Sheria ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) iangaliwe upya ili kubainisha vigezo vinavyotumika katika usajili wa vyuo nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nakushukuru kwa kuipa heshima Kamati yangu kujadili, kufanya ziara ya kikazi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilichopo mkoani Arusha na hatimaye kuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe mwenyewe binafsi, namshukuru kwanza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa (Mb) na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Jenista Joachimu Mhagama (Mb) kwa ushirikiano waliotupa katika kujadili Azimio hili.

Aidha namshukuru Katibu Mkuu Profesa Sifuni Mchome na wataalam wote wa Wizara kwa ufafanuzi wa kina wa hoja za Kamati. Aidha, nawashukuru Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ushirikiano wao waliotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa umakini wao mkubwa na ushirikiano walioutoa katika kufanikisha kazi hii. Naomba niwatambue lakini najua huwezi kukubali kw ahiyo siwatambui Mheshimiwa Spika, wote wanajifahamu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe mwenyewe kwa jinsi unavyoshirikiana na Kamati yetu unatushauri vizuri. Namshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji *(Tengeru Institute of Community Development)*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwite Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii Mheshimiwa Rajab Mbarouk. Rajab *busy* kweli. *(Kicheko)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED – K.N.Y. MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Sana Mama.

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani anayeshughulikia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Susan Lyimo, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Tanzania ina upungufu mkubwa wa wataalam wa maendeleo ya jamii, hivyo katika mkakati wa kuhakikisha jamii ya Watanzania inafikia malengo yaliyowekwa katika Dira ya 2025 ni lazima wataalam wa kada hii wawepo, kinyume cha hapo tutaendelea kupanga mipango ambayo utekelezaji wake ni wa ubabaishaji tu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo miaka yote Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisisitiza kuwa na Taifa linalowajibika, vivyo hivyo ni lazima kuwa na jamii inayowajibika na jamii

inayowajibika ni lazima iandaliwe na iongozwe na wataalam waliopikwa vizuri kutoka katika vyuo vitakavyotoa taaluma ya maendeleo jamii kwa familia zetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Spika, sijapata hicho anachokisoma.

**SPIKA:** Nendeni ofisini mka-*find out*. Endelea nadhani zipo mtagaiwa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED – K.N.Y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Kwa sababu tumeshawasilisha sisi muda mrefu.

**SPIKA:** Naomba mgawe, naomba endelea Mheshimiwa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED – K.N.Y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa haraka haraka mtu atauliza kuwa ni kwa nini Waziri wa Elimu ndiyo alete Azimio hili la kuliomba Bunge kuridhia Chuo hicho kuwa na madaraka ya kujitegemea badala ya Waziri Mwenye dhamana na Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na Azimio hili, ila kutokana na hali ya chuo ilivyokuwa kwa miaka mingi inauliza ni kwa nini Azimio hili limechelewa kwani Chuo hiki tayari kingelikuwa kinatoa wataalam wengi na hivyo mpango mkakati wa kufikia Dira 2025 usingekuwa unasumbua kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hayo kutokana na hali halisi ya mgao wa bajeti kwa Wizara hii ambao kwa kuweli haujawahi kutosheleza kwa idara na taasisi zilizo chini yake. Kwani ni mara nyingi kumekuwa kukijitokeza migomo baridi ya wanafunzi kwa kukosa kwenda kwenye mafunzo kwa vitendo kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu huo wa bajeti, athari zake zimekuwa zikiathiri hata utendaji wa Chuo katika kuzalisha wataalam waliopikwa na kuiva vyema. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini Azimio hili ni dhahiri kuwa utendaji wa chuo hicho utakuwa ni wa kiwango kinachohitajika na malalamiko toka kwa watoa na wapatiwa taaluma hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, imani ya Kambi Rasmi inatokana na ukweli kwamba chuo hicho kitakuwa na Bodi, hivyo kupitia Bodi kitakuwa na uwezo wa kukopa na kuingia katika mikataba mbalimbali ya nje na ndani kwa manufaa ya chuo katika mustakabali mzima wa kutoa mafunzo yaliyotukuka. Aidha, kile kidogo kilichokuwa kikikusanywa na chuo badala ya kurudishwa Wizara na kusubiri kupewa mgao kitakuwa kinatumika kwa maendeleo ya chuo chenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kujitegemea kiutendaji maana yake ni uimarishaji wa utoaji wa mafunzo na mwisho kuzalisha wataalam wengi kwa mustakabali mwema kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa tukirudi kwenye ile hoja ya kwanza ya kwa nini Azimio hili halikuletwa na Waziri mwenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii kwani Chuo cha Tengeru kipo chini ya Idara mojawapo katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Tengeru kilianzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Sura ya 129 kifungu cha 6(1). Kifungu hicho kinampatia mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu kutangaza kwenye Gazeti la Serikali chuo chochote kinachotoa elimu ya ufundi kuwa chuo kinachojitegemea baada ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kuzingatia mambo muhimu kuhusu chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ya kuzingatiwa na Baraza katika kukifanya chuo kijitegemee na kupendekeza kwa Waziri mwenye dhamana ni pamoja na kuangalia miundombinu ya chuo kwa maana ya madarasa, mabweni, karakana za kujifunzia, uwezo wa chuo kudahili wanafunzi, uwezo wa kitaaluma kwa timu nzima ya wakufunzi kwa maana (idadi ya walimu wenye shahada za uzamili na uzamivu).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani kuunga mkono Azimio hili la kikifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kujitegemea, tunaitaka Serikali kuleta Maazimio mengine ya kuvifanya vyuo vingine vilivyokidhi vigezo vya kujitegemea kiutendaji ili navyo viweze kujitegemea na kushughulikia mambo yanayovihusu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Buhare kilichopo Musoma tayari kimeshaomba kujitegemea kiutendaji. Sasa labda tunajiuliza je, ni lini Serikali italeta Maazimio ya vyuo kama hivyo ili yaridhiwe na Bunge hili?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuwa haina tatizo la kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kujitegemea kiutendaji kama ambavyo Azimio linavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu na kwa msisitizo kidogo napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo sasa inaundwa na vyama hivi vitatu CUF, NCCR na CHADEMA kwa ushirikiano mkubwa katika kushughulikia masuala ya kitaifa. *(Makofi)*

Aidha, napongeza juhudi za Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ndani na nje ya Bunge za kuelimisha wananchi juu ya mchakato wa Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, napenda kuchukua fursa hii pia kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuupongeza uongozi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa jitihada zao za kukiongoza chuo kwa umahiri mkubwa hadi kukifikisha katika hatua ya kujitegemea.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawatakia uongozi wa chuo, wahadhiri na wanafunzi kila la kheri na mafanikio wanapofungua ukurasa mpya wa kuitafuta elimu katika hali ya kujitegemea kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa namna ambavyo unaendesha Bunge letu lakini pia nimshukuru na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa yake nzuri ambayo ameweza kuitoa kuhusiana na Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. UKAWA unafanya kazi nje ya Bunge siyo humu, halafu Kambi Rasmi ya Upinzani ni Wabunge wote ambao siyo Chama Tawala. Kwa hiyo, ninakushukuru kwa taarifa yako. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, kwa sasa atakayeitwa kuchangia ni dakika kumi kwa sababu ule utaratibu wa dakika saba ulikuwa kwa ajili ya zile siku 26, ambazo mmezifanya vizuri sana. Mimi ninawaambia dakika saba zilikuwa zina *productivity* kubwa sana kuliko kumi na mmefanya kazi nzuri sana, lakini kwa sasa tunarudia utaratibu wetu wa Kanuni. Kwa hiyo, nitakaowataja ni dakika kumi.

Nianze Mheshimiwa Said Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Ester Bulaya kama atapata nafasi. Nianze na hawa kwanza dakika kumi. Mheshimiwa Mtanda hayupo? Nimwite nani sasa? Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze vilevile na mimi kwa kuunga mkono hoja kwa mara ya kwanza, ni wazo zuri ambalo Serikali imeleta na ni jambo la msingi, kwa sababu tunahitaji maendeleo ya jamii zetu. Tupo hapa kama Viongozi kwa sababu ya maendeleo na ustawi wa jamii.

Nikubaliane na hoja iliyoletwa Mezani kwamba, kwa kuwa na chuo ambacho kinajitegemea, tutatoa fursa ya chuo kupanga mipango yao na kuweka uwanja mpana wa kuwafunza hawa wanafunzi. Pamoja na hayo, mimi ni-*challenge* kidogo dhana nzima ya *community development,* kwa sababu mpaka sasa tuna vyuo vingi ambavyo vinafundisha maendeleo ya jamii lakini kwa masikitiko yangu makubwa wale ambao wanahitimu kwenye vyuo hivi, wengine wamemaliza elimu za chini; *certificate, diploma* mpaka *degree,* wao wenyewe waliomaliza elimu hii unaona wanahitaji kuendelezwa wenyewe.

Sasa tunapowatoa kuwapeleka kwenye jamii wakaziendeleze jamii wao wenyewe hawajaendelezwa kifikra, inaleta mkanganyiko kidogo. Kwa hiyo, ninashauri kwa Wizara pamoja na Serikali, ni vizuri pamoja na mtaala ambao upo, tukaongeza na mambo mengine ya *attitude change*. Wapo watu wengine wanasoma masomo ya darasani, lakini hawajabadilika kimtazamo. Kuna msemo mmoja wa kizungu unasema, *change what you see by changing how you see*. Kwa hiyo, tusipobadilika mitazamo ya kifikra, pamoja na elimu tunayoipata, hatuwezi kukabiliana na *challenges* ambazo tunazipata. Kama Taifa tuna changamoto nyingi sana ambazo zinatukabili; kwa hiyo, tukiwa na mfumo wa elimu ambao ni *traditional,* wa kimazowea, hatuwezi kukabiliana nao kutokana na changamoto tulizonazo.

Ukimwona mtu ambaye amemaliza Digrii ya *Community Development* au *Diploma*, ukamlinganisha na mtu ambaye amesoma Kitabu cha *Rich Dad, Poor Dad,* unaweza ukakuta huyu aliyesoma hiki kitabu amebadilika kimtazamo kuliko aliyekaa darasani kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali na Wizara kwa ujumla kwamba, ni vizuri sasa wakati umefika hebu tujitahidi kuwafundisha watu kubadili *attitude,* wawe na mtazamo; pale panapoonekana pana ugumu, waone kuna uwezekano wa kupenya.

Mtu mwenye mawazo ya mtazamo ulio *positive*, anaona fursa katika kila magumu. Mtu mwenye mtazamo ambao ni *negative* anaona magumu kila kwenye fursa. Kwa hiyo, wakati umefika kwa Taifa letu sasa pamoja na mitaala, pamoja na mtakaowapata, pamoja na kwamba hiki chuo kitaenda mbele, ni vizuri tukaanza kujijenga wenyewe. Mtazamo huu unaanza kwenye *family,* tunapokuwa tumetengeneza *strong family* ambazo zina akina baba ambao wako *responsible* kwa watoto wao, wanaowajibika na wanaojali familia zao, tunapokuwa na akina baba na akina mama bora, wanakuwa na watoto bora. Hawa watoto

bora watajenga *community* bora. Kwa hiyo, *Community Development* ni mtambuka, inaelekea maeneo mengi ili tuwe na *community* zilizo nzuri, lakini ni lazima kuwe na *attitude change* ambazo zitasababisha hawa watoto wawe wanawaza *positive* au wanafunzi wawe *positive* na uzalendo kwa ajili ya Taifa lao.

Maneno yangu ni hayo kwamba, ninaunga mkono hoja, lakini ni lazima tuwe na *attitude change*, tusiangalie ugumu katika maisha tu kuwa hii inawezekana. Mitaala hii tubadilishe watu namna ya kufikiri na kuona kwamba kuna fursa; mfano mzuri, watu wa Singida wanapoona kuna jangwa, kuna upepo mkali, vibao barabarani vinasema kuna upepo mkali, lakini mtu mwenye *positive change* anaona anaweza akaweka *wind mill.* Mtu mwenye *positive change* anaweza akaona kuwa kutatokea umeme kutokana na upepo ule. Mtu wa Makambako anapoona ule upepo ni matatizo, mtu mwenye *positive change* anaona anaweza kupata fursa kwenye maeneo hayo. Ili kuweza tuzi-*develop* hizi *community* hawa watu wabadilike wawe wafikiri *positive.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli leo umesema kama Mchungaji, kama hawakukuelewa basi bahati mbaya, lakini umesema vizuri. *(Kicheko)*

Nilisema anayefuata ni Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na ninashuhudia Wabunge tukifanya kazi yetu vizuri bila ya kujali itikadi za Chama katika mambo ya msingi. Hili ndiyo Bunge ambalo linatakiwa, Bunge moja, kuonesha ushirikiano katika mambo ya msingi yanayohusu Taifa letu. Isiishie katika Azimio na hata katika mambo mengine yanayojali masilahi ya Taifa, tunatakiwa kuungana kama viongozi, kuhakikisha mambo ya msingi yanayohusu Taifa letu, tunashirikiana pamoja na kuweka itikadi zetu pembeni.

Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii pia kuwapongeza Wizara kwa kuleta Azimio hili na mimi ninaliunga mkono, kwa sababu tunakitegemea sana Chuo cha Tengeru. Nimesoma taarifa hii vizuri, moja ya sababu ya kukifanya kijitegemee kiweze kujiendesha mambo yake chenyewe. Tumeshuhudia vyuo vingi vya maendeleo ya jamii vikiwa hohehahe. Sasa ninaamini kabisa, kuweka chuo hiki kujitegemea chenyewe pia kitapata fursa ya kutanua wigo kwa mambo mbalimbali na pia kuweza kupata fursa ya kutafuta fedha wenyewe bila ya kuitegemea Serikali peke yake na kuhakikisha kinajiendesha vizuri.

Kwa kupata fursa hiyo, tumeona Shule zetu za Kata zinatoa wanafunzi wengi, lakini pia wanakosa fursa ya kupata nafasi mbalimbali. Tuna changamoto ya Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, fursa hii itasaidia vijana wengi ambao wameshindwa kuendelea katika maeneo mengine, kupata furasa na kujiunga na Chuo hiki kwa wingi.

Nimesoma Taarifa ya Kamati, tumeona mbali na Serikali kuleta azimio hili, bado kuna changamoto kubwa sana. Changamoto hizi mbali na kwamba, tunaridhia kitajitegemea, ninaiomba Serikali isikitelekeze kwa kisingizio kwamba, kimepewa fursa ya kujitegemea. Bado mna jukumu la kuhakikisha mnakarabati miundombinu na kuhakikisha mahitaji ya msingi ambayo yanahitajika mbali kukipa fursa ya kujitegemea, mnashirikiana nacho na kutatua matatizo hayo, kwa sababu yalikuwepo kabla ya hamjaipa fursa ya kujiendesha wao wenyewe. Kwa hiyo, ni jambo la msingi, mimi nimefika Tengeru, Chuo hiki kiko hohehahe.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye Taarifa ya Kamati pia wana tatizo la ardhi wanahitaji karibu heka arobaini na ni vyema Serikali mkashirikiana na Wizara husika, kuhakikisha wanapata hili eneo kwa ajili ya kutanua Chuo. Hili ni jambo la msingi kwa sababu wanahitaji kutanua Chuo waweze kudahiri wanafunzi wengi kujiunga na Chuo hicho. Nimeona pia kuna tatizo la suala zima la walimu wenye sifa ambao Kamati imeeleza kwamba, hakuna walimu wenye *Ph.D.* Jambo la msingi unapotaka kutoa wataalamu, lazima kuhakikisha hata hawa wanaowapa elimu wanakuwa na elimu ambayo inaendana na kukuza weledi wa kutosha kwa vijana wakaoenda pale kupata elimu. Tuna changamoto kubwa sana ya Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika maeneo yetu mbalimbali. Kwa hiyo, ninaamini kutoa fursa hii itasaidia sana kuhakikisha tunapata wataalamu wa kutosha. Hata katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona wamekiri kuwa, kuna tatizo hilo na wamesema watajitahidi kutoa mafunzo kwa walimu wa Chuo cha Tengeru.

Mheshimiwa Spika, bila ya kupoteza muda, nilikuwa ninasisitiza tu Serikali isikitelekeze hiki Chuo kwa kigezo kwamba wana uwezo wa kujitegemea. Changamoto zipo nyingi sana, mbali na Azimio hili kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi ninaunga mkono hoja, nina imani Mheshimiwa Jenista Mhagama atalifanyia kazi suala hili vizuri. Baada ya kushika usukani kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri, Azimio hili limekuja, sasa shughulikieni hizi changamoto. Msikiache hiki Chuo chenyewe, mbali na kwamba mmetuletea hili Azimio, changamoto ni nyingi sana. Ninaomba sana hilo mlizingatie Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moses Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Wasira!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Niseme kwamba, wazo ni zuri kimsingi, linastahili kuungwa mkono, lakini ni lazima tuweze kuishauri Serikali kuangalia ni namna gani ya kuweza kuangalia kuhakikisha kwamba, baada ya kuweza kuwa wazo hili limeungwa mkono na kupitishwa ni mambo gani yaweze kufanywa.

Nilikuwa ninajaribu kuangalia taarifa ambayo imesomwa na Kamati, ule ukurasa wa tatu, ukiangalia moja ya mambo yatakayoweza kukiwezesha hiki Chuo baada ya Azimio hili kuridhiwa ili kiweze kujitegemea, kwenye (i) pale wanasema, baada ya Azimio hili kupitishwa, Chuo kitaweza kubuni mipango na miradi mbalimbali itakayolenga kuongeza mapato ya chuo. Hali itakayosaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharimia uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyuo vingi hapa nchini, ambavyo kimsingi ukiangalia vinajitegemea, lakini bado vimeendelea kuwa tegemezi kwa Serikali. Sasa hapa kidogo mimi binafsi ninapata shida kuona ni kweli baada ya Chuo hiki kuwa kimefanywa kiweze kujitegemea kuwa huru ndiyo utakuwa mwarobaini wa matatizo ambayo yanakikabili leo hii?

Haya maswali inabidi pengine kama Bunge na Serikali kwa pamoja tujiulize kama itakuwa ni suluhisho.

Mimi ninafikiri tatizo lililopo hata katika vyuo vingine ambavyo viko hapa nchini, ni tatizo la *mindset* miongoni mwa watu ambao wamepewa dhamana ya kuvisimamia vyuo hivyo. Mtaalamu mmoja wa Saikolojia, Bwana Ivan Pavlov, katika nadharia yake ya uzoeshi, *conditioning theory,* anatuambia kwamba, ukizoea kufanya jambo lolote kwa namna fulani, maana yake ni kwamba, basi mazoea yanajenga tabia.

Ukijaribu kuangalia tatizo la msingi ambalo linaikabili nchi yetu, ukirejea nadharia hii ni kwamba, watu wetu hawajaandaliwa katika misingi ya kufanya mambo kwa misingi ya uzalendo. Tatizo la uzalendo na ndiyo maana utakuta hata rasilimali kidogo ambazo zinapatikana pengine zipelekwe mahali fulani kwa ajili ya jambo fulani, matokeo yake watu utakuta wanapiga dili, matokeo yake mambo hayaendi. Kwa hiyo, hata kama tutabadilisha taasisi hizi, lakini pasipo kuhakikisha tunaangalia mitaala yetu ambayo inatumika kuwafundisha watu ambao watatumika kwenda kufanya kazi ambazo zimekusudiwa na Serikali, itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu ukiangalia leo hii ukienda kwenye vyuo vingi, ukijaribu kufanya *simple study,* ukumwuliza mtu kwa nini unasoma kozi fulani? Atakwambia mimi ninasoma kozi fulani ninataka niende mahala fulani mambo yangu yaweze kuwa safi. Imefikia mahala sasa watu wengine wanabeza hata baadhi ya taaluma za watu. Sasa hili ni tatizo, ni janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali; moja, katika kuhakikisha hiki chuo ambacho kinashughulika na masuala ya maendeleo ya jamii wa-*introduce subject* moja ambayo ita-*deal* na suala la *critical thinking*. Katika *critical thinking* ndipo watu wanaweza kufikiri kwa namna ambayo inaweza kulitoa Taifa mahali tulipo. Hapa tumegota, leo tunabadilisha hiki chuo kitoke kwenye usimamizi wa Wizara, sidhani kama chuo ambacho kimekuwa kikisimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto kwamba imekuwa ndiyo tatizo.

Tatizo ni *mind set* miongoni mwa watu ambao wana dhamana ya kuweza kuvisimamia vyuo hivi. Tatizo siyo kwa sababu kipo chini ya Wiazara. Sasa tunaondoaje matatizo haya ya watu kukosa uzalendo wa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu. Lazima ku-*introduce* kuwepo na *subject* hiyo ambayo ni *critical thinking,* ndiyo ambayo inaweza ikatutoa hapa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia ninaangalia taarifa hii, ukienda ukurasa wa nane, inaonekana bado kuna tatizo, mwalimu mwenye Shahada ya Uzamili na yeye anamfundisha mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili. Haya ni maajabu! Sasa kama tunataka kutoka huko, lazima tuhakikishe tunawapatia watu *knowledge* na *skills* ambazo ni *appropriate* katika kuja kutatua matatizo haya. Hili tukiamua kama Taifa linawezekana. Litawezekana iwapo viongozi tutakuwa na utashi na dhamira ya kuona kila kitu kinafanywa kama kilivyokuwa kimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia changamoto hizi ambazo zinajitokeza; kwa nini matatizo haya yanajitokeza. Ni kwa sababu ya misingi mibovu ambayo imejengwa kuanzia huku chini. Leo ukichukua watu ambao wanasoma kwenye vyuo mbalimbali, kuna tofauti kubwa na watu ambao walisoma zamani.

Mheshimiwa Mkosamalia asubuhi aliuliza swali moja, inatia aibu sana unapokwenda katika Halmashauri moja, ametoa mfano wa vibao akasema imeandiwa Halmashauri ya Wilaya labda ya Dodoma. Unakwenda shule nyingine, Halmashauri ya Kijiji fulani, shule ya msingi Fulani! Lazima tuwe na *uniformity,* haya ni ukiyaangalia unakuta yanatokana na mfumo wetu wa elimu, yanatokana na kukosekana kwa *seriousness* miongoni mwa watu na ndiyo maana yanajitokeza. Wakati mwingine baadhi ya watu wamekuwa hawajali wanaruhusu watu ambao hawaja-*qualify* kufundisha kwenye *level* mbalimbali. Haya yanajulikana lakini Serikali imeyaacha.

Mheshimiwa Spika, sawasawa na kumchukua *University Graduate* umpeleke akufundishe *kindergarten* kule; hawezi kufanya kazi hii; ndiyo yuko *knowledgeable,* ana maarifa

makubwa lakini huyu mtu ana-*lack skills* za kuhakikisha anakaa na yule mtoto amfundishe. Kuna saikolojia ambayo ni sahihi katika kumfundisha yule mtoto wa elimu ya awali.

Unamtoa *University Graduate* hakusomea ualimu wa kufundisha elimu ya msingi aende kufundisha shule ya msingi, hatuwezi tukafikia malengo ambayo tumeyakusudia. Wapo watu na ndiyo maana hivi vitu vinakwenda kwa *levels.* Sasa haya matatizo kama yapo yamejitokeza Chuo cha Tengeru, mwalimu mwenye Shahada ya Uzamili *(Masters Degree)* na yeye anamfundisha mtu wa *Masters Degree;* hapa kuna tatizo na hili niseme kwamba ni janga.

Mheshimiwa Spika, haya na mengine mengi ninafikiri tuyaangalie. Lile swali la kwanza nitaomba Waziri anapokuja ku-*wind up* atusaidie; ni kweli Chuo hiki iwapo kitaruhusiwa kujitegemea ndiyo kitaweza ku-*solve* matatizo ya kiuchumi yaliyokuwa yanakikabili awali kwa sababu kimetoka kuwa chini ya Wizara?

Binafsi, ninaona ni hapana. Tatizo ni suala la utashi miongoni mwa watu ambao wamepewa mamlaka, kuhakikisha mipango ambayo imepangwa inasimamiwa na kutekelezwa vile ilivyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. WASIRA - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSINO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango kidogo kuhusu hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Suala tunalozungumza hapa ni la kukibadili Chuo cha Tengeru kiingie katika orodha ya vyuo vinavyotoa elimu ya juu. Ninadhani ndiyo sababu ya msingi ya kukihamisha kutoka *Community Development* kwenda kwenye Wizara inayosimamia elimu ya juu. Huo ndiyo msingi, kwa hiyo, hakuna uhusiano wowote wa kushindwa kukiendesha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, laini ambayo ningependa mimi kuisema hapa, siyo chuo chenyewe, lakini matumizi ya watu watakaotokana na chuo hicho na vyuo vingine vinavyotoa mafunzo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumepeleka madaraka kwa Wananchi, lakini hoja hapa Wananchi wayatumie madaraka kufanya nini. Wataalamu wa *Sociology* wanaamini kwamba, jamii zote zinaweza kubadilika, lakini zinabadilika hatua kwa hatua na kila jamii inahitaji msaada wa namna ya kubadilika.

Kwa hiyo, Idara ya Maendeleo ya Jamii wajibu wake mkubwa ni kuiandaa jamii kufanya mabadiliko kwa kutambua matatizo waliyonayo. Hiyo ndiyo fursa, kwamba, jamii tunasema tunataka maendeleo yaanzie chini kwa watu wenyewe. Wananchi wanaweza kuwa wapo, wanaishi, lakini hawajui *problem* inayowakabili. Wanahitaji msaada wa uchambuzi na elimu ili waweze kuamua, wajue matatizo yao hasa hasa ni nini na kwa nini hali iko hivyo ilivyo.

Hiyo nadhani ndiyo kazi ya kwanza ya hawa watu, ndiyo maana wanafundishwa *sociology*, watambue jamii wanayoishi nayo na matatizo yao. Waanze mahali walipo, waishauri jamii ili kupitia ushauri ule waweze kutambua na kuchambua matatizo yao kisha wakae chini na wapange namna wanavyoweza kujiondolea matatizo yao.

Sasa katika kutambua hivyo, yapo matatizo ambayo jamii yenyewe inaweza kuyajua, ikayatambua, iayachambua na kuyashughulikia bila msaada wa mtu mwingine yeyote. Yako matatizo ambayo jamii haiwezi kuyamaliza yenyewe mpaka kwanza wapate msaada wa

Halmashauri yao au Serikali Kuu. Uchambuzi huu ndiyo msingi wa kuwa na maendeleo yanayochipuka kutoka chini kwa jamii yenyewe. Hawa ndiyo wataalamu wanaofanya kazi hii.

Tatizo langu mimi ambalo nataka kulisema na ndiyo ushauri ninaotaka kuutoa hasa kwa watumiaji na wale wenye wajibu wa kusimamia maendeleo ya vijijini; ni kuitambua hii Kada na kuitumia. Kufundisha suala lingine, ila kutumia wale watu ndilo suala la msingi zaidi. Maana unaweza kuwa na Chuo, unaweza ukawafundisha, ukawapa utaalamu, lakini unatumika wapi kusaidia maendeleo ya watu wa nchi yetu. Kwa hiyo, kama tutawatumia, uwekezaji wetu katika Chuo hiki cha Tengeru na Vyuo vingine vyote pamoja na vile vya Buhare, vitakuwa vimefanya kazi ya maana zaidi, kwa sababu Wananchi watanufaika na suala hili. *(Makofi)*

Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ndiyo ingewasaidia Wananchi kuanzisha fursa ambazo zinafanana na kupelekewa madaraka. Madaraka ya Wananchi hayawezi kukomea kwenye Halmashauri ya Wilaya. Madaraka ya Wananchi lazima yaende kwa Wananchi chini kabisa na fursa na maendeleo yao lazima yapangwe kutokea chini na hawa watu ndiyo wanaweza kusaidia katika kazi hii. *(Makofi)*

Huko nyuma kwa sababu Idara hii imekuwa inabadilika sana, miaka ya 60 na kitu wakati tumepata Uhuru, Idara hii ilikuwa inafanya kazi nyingi na wakati ule ndiyo kulikuwa na kitu kinaitwa *self help*. Ile *self help* ilikuwa inasimamiwa na hawa. Vilevile kulikuwa na fursa nyingine ya kubadilisha makazi. Kulikuwa na vikosi chini ya Idara hii ambavyo vinatoa mafunzo namna ya kutengeneza uzalishaji wa vifaa vya ujenzi, ili kuwawezesha Wananchi waweze kubadilisha makazi yao.

Walikuwa na vifaa na *brigades* za kufanya kazi hii. Mimi nadhani Chuo cha Tengeru kinaweza kikafanya kazi nzuri kikirudisha fursa na elimu kwa Maofisa wake, ambao wanaweza wakarudisha kazi hii na ikawasaidia Wananchi katika kuleta ubora wa maisha yao. Kupanga mipango ya Wananchi ni fursa ya Wananchi. Yako mambo ambayo Wananchi wanaweza kumaliza wenyewe na mengine hawawezi; na kama tunaunga mkono hoja hii, basi tukubali kuachana na tabia ya kuwaambia Wananchi wao hawana cha kufanya isipokuwa Serikali; maana ndiyo msingi wa hii hoja, ndiyo msingi wa elimu ya hawa. Kwamba, kuna mambo wanaweza kufanya. Sasa hivi tumemwachia Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kata anaweza akatumia nguvu, hawa hawatumii nguvu wanatumia akili ya kufundisha na Wananchi wanaweza kuchangia kwa hiari yao baada ya kuelewa.

Mimi nikipita nikawaambia msichangie kwa sababu Serikali itafanya kila kitu, maana yake unawaambia cheleweni mpaka Serikali itakapowakumbuka. Mimi nadhani hiyo siyo sawa. *(Kicheko)*

Nimefurahi sana kwamba, Kambi ya Upinzani inaunga mkono. Matumaini yangu ni kwamba, wataunga mkono na mfumo huu wa kuwaacha Wananchi wawe wanafanya mambo ambayo wanaona wanayaweza na wachangie maendeleo yao, kwa sababu huo ndiyo msingi wenyewe wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Saidi Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia katika Azimio hili. Nianze kwa kusema ninaunga mkono Azimio la Bunge letu leo kuridhia na hatimaye Chuo hiki cha Tengeru kiweze kujiendesha kiutendaji.

Ninaunga mkono kwa sababu miongoni mwa mapendekezo ambayo Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii iliyatoa ndani ya Bunge hili juzi, wiki iliyopita wakati tunajadili hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ilikuwa ni kuiomba Serikali kuleta Azimio hili hapa Bungeni haraka iwezekanavyo ili liweze kuridhiwa.

Kwa hiyo, ninafurahi kwamba, maombi ya Kamati yangu yamezingatiwa na leo Azimio hili liko mezani kwetu. Kwa hiyo, ninawashawishi Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kauli moja tuunge mkono Azimio hili ili Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kijiendeshe kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo faida nyingi ambazo zimeshasemwa, lakini endapo tutaridhia leo, Chuo hiki kitakuwa ni Chuo miongoni mwa Vyuo vikubwa sana katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Chuo ambacho kinatoa taaluma hii ya Maendeleo ya Jamii. Nimepata fursa ya kwenda nchi mbalimbali za Afrika Mashariki, lakini hawana Vyuo vikubwa vyenye uwezo wa kutoa taaluma hii ya Maendeleo ya Jamii kama ambavyo Chuo chetu hiki kinatoa.

Kwa hiyo, ninawapongeza sana Serikali kwa kuleta Azimio hili, tunaliunga mkono kwa sababu tukifanya hivi mambo yetu yatakuwa mazuri sana. Ningependa kushauri sasa kwamba, mara baada ya kuridhiwa kwa Azimio hili na hatimaye Chuo hiki kujiendesha kiutendaji, ningeshauri sana, Chuo hiki kiwe na utaratibu kama Vyuo vingine, kuweka matawi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ili taaluma hii ya Maendeleo ya Jamii iweze kuwanufaisha na kuwafikia Watanzania walio wengi, badala ya hivi sasa Chuo hiki kipo mbali sana.

Kwa hiyo, ningetoa wito kwa Watendaji baadaye kuona haja; ukiangalia sasa hivi uchumi wa nchi unaelekea Mikoa ya Kusini; Lindi na Mtwara, kwa sababu ya uchumi wa gesi, uchumi wa kilimo, kilimo cha zao la ufuta, nimekieleza vizuri hapa leo asubuhi. Kwa hiyo, ningefurahi sana kuona Chuo hiki baadaye kinaweka mipango endelevu ili kuwa na matawi hasa katika Mkoa wa Lindi. Sisi Watu wa Lindi tupo tayari kutoa ardhi ili Chuo hiki kiweze kujengwa pale Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ambalo nimeona niliseme ni kuhusu changamoto. Wakati tunaridhia, lakini Kamati yangu tulipata fursa ya kukitembelea Chuo hiki na vyuo vingine kama Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. Kwa kweli vyuo hivi vinakabiliwa na changamoto kubwa sana.

Kwa hiyo, sasa Wizara kwa kushirikiana na vyuo hivi, waone haja ya kuimarisha miundombinu. Migogoro ya Ardhi katika maeneo ya vyuo hivi imekuwa mikubwa sana. Tunaomba Serikali ihakikishe inakisaidia Chuo hiki ili kuondokana na migogoro ya ardhi, waweze kupata eneo kubwa wapanue wigo wa Chuo chao kiweze kuwanufaisha vijana wetu walio wengi.

Tatizo la usafiri, tulizungumza sana kwenye Kamati, Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii vinakabiliwa na matatizo makubwa ya usafiri. Vyuo hivi hasa Tengeru, Rungemba na maeneo mengine, Bigwa tumekwenda tumejionea Chuo kina wanafunzi 2000 lakini hakuna usafiri; unajiuliza endapo wanafunzi watapata matatizo ya usiku, wanahitaji kupelekwa Hospitali, watatumia njia gani kufika Hospitali kwa urahisi?

Kwa hiyo, naishauri Serikali kuhakikisha wanashirikiana na vyuo hivi na kuvisaidia hivi. Kamati yangu iliwahi kutoa ushauri hapa ndani ya Bunge kwamba, *TRA* wameshika magari karibu 2500 pale Dar es Salaam, mali ya Kampuni ya *SBT Tanzania;* yametolewa Japani, hayana soko katika nchi yetu, hawakufuata utaratibu, Serikali imebinafsisha magari yale. Kwa nini Serikali isione haja ya kutoa baadhi ya magari hayo ili yaweze kusaidia usafiri kule Lungemba, Tengeru, Bigwa na Vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii ikiwemo Chuo cha Chilala kule Rutamba Mkoani Lindi katika Jimbo langu?

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo muhimu sana. Kwa hiyo, ninaendelea kusema, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ni wachache sana. Tulijadili na Kamati yangu ilitoa mapendekezo na maoni ndani ya Bunge hili kwamba, iko haja sasa ya kuwa na utaratibu maalumu, utakaowezesha wataalamu hawa wanapohitimu kwenye vyuo hivi, kupangiwa moja kwa moja maeneo ya kazi kama tunavyowapangia walimu. *(Makofi)*

Kamati yangu ilitoa ushauri huu, ni ushauri mzuri kwa sababu tuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii zaidi ya 2000. Kwa hiyo, nashauri chuo hiki kikianza kujiimarisha na kutoa wahitimu, basi ni vizuri sasa wahitimu hawa wapangiwe kazi moja kwa moja kama ambavyo inafanyika kwenye Kada nyingine hasa mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa baadhi ya maeneo ambayo nilisema ni vizuri leo hii nichangie. Naendelea kuunga mkono Azimio hili na kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge, kuona haja na umuhimu wa kuunga mkono Azimio hili ili hatimaye Chuo hiki na Vyuo vingine, viweze kupata hadhi ambayo inaweza kusaidia sana vijana wetu kuweza kupata elimu iliyo bora na katika mazingira mazuri.

Mwisho, nimalizie, tulitoa ushauri pia kuhusu *retention* kwamba, fedha zinazokusanywa kama maduhuli kwenye vyuo hivi, zikae pale, *retention at the source,* ziweze kusaidia kukabiliana na changamoto.

Mheshimiwa Machali, rafiki yangu, ni mkorofi kidogo *NCCR,* lakini alitoa ushauri mzuri kwamba, endapo Chuo hiki kitajitegemea matatizo haya yatakwisha, Kamati yangu ili shauri kwamba ili kumaliza matatizo haya ni vizuri fedha hizi za maduhuli zinazokusanywa zisiende Hazina Kuu kwa sababu hazirudishwi pale. Badala yake zikusanywe, zikae Hazina Ndogo ili Vyuo vya Maendeleo ya Jamii viweze kutumia fedha zile kuweza kutatua changamoto zilizoko kwenye vyuo. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Machali kwa ushauri wake na mimi ninamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, ninaomba kuunga mkono tena Azimio hili. ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Bibi Maendeleo, Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Yusufu Salim Hussein. Huyu Bibi Maendeleo *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, shikamoo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Unastahili heshima hiyo Mheshimiwa. *(Kicheko)*

Kwanza, niseme naunga mkono hoja na Azimio hili la Bunge la kuifanya Taasisi ya Tengeru kujitegemea. Mimi ni Mwanasheria kwa taaluma. Tunapofanya Taasisi ijitegemee, tunalenga kuimarisha ubora au huduma inayotolewa na Taasisi husika.

Kwa hiyo, kuifanya Tengeru iweze kujitegemea kiutendaji ni kukifanya chuo hicho kiweze kuzalisha Wataalamu wa kutosha katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Kweli tunaelewa umuhimu wa Kada hii ya Wataalamu hawa wa Maendeleo ya Jamii katika kuhamasisha jamii katika masuala mbalimbali ya maendeleo, lakini pia Wataalamu hawa wanasaidia sana katika Halmashauri mbalimbali nchini, kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya kimaendeleo; mfano, Miradi ya *TASAF* mingi inasimamiwa na Wataalamu katika Kada ya Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, tukikifanya chombo hiki kijitegemee, tunalenga kuimarisha utoaji wa huduma husika kwa maana ya Sekta hii ya Maendeleo ya Jamii.

Tunaposema Taasisi kujitegemea ni lazima tuangalie mambo mengine yanayohitajika katika Taasisi hiyo, ikiwemo suala la rasilimali watu wa kutosha. Hapa tunamaanisha wakufunzi na walimu wawe na sifa zinazotakiwa na wale watumishi wasiokuwa walimu wawepo wa kutosha na wenye sifa zinazotakiwa. Kingine pia ni uwepo wa miundombinu ya kutosha, kwa maana ya kwamba, kuwepo madarasa ya kutosha, mabweni ya kutosha, karakana za mafunzo, maktaba na mambo mengine yote ambayo ni muhimu na huduma nyingine zote ambazo zinahitajika kulingana na chuo hicho ziweze kupatikana kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, unaposema kuanzisha Taasisi ni sharti iwe na Bodi. Kwa hiyo, ni muhimu sana baada ya Azimio hili, Bodi ikaundwa mapema iwezekanavyo. Mara nyingi tumeona kunakuwa na urasimu wa uteuzi wa Bodi, lakini kunakuwa na ucheleweshaji sana katika uundaji wa Bodi.

Tumeona mifano katika Wizara mbalimbali, inachukua muda mrefu sana katika uteuzi wa Bodi, mwaka, miaka miwili na wakati mwingine mpaka miaka mitatu. Kwa hiyo, ni muhimu sana Bodi hii pia ikaundwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi kujitegemea au chombo hicho kujitegemea kiutendaji itahitaji fedha. Sijajua kama Wizara husika imeweza kutenga bajeti ya kutosha ya kuifanya Taasisi iweze kujitegemea au maandalizi ya fedha ya kuiwezesha Taasisi hii iweze kujitegemea inavyotakiwa yamefikia wapi. Tunaitaka Wizara itizame na Vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii ambavyo vimeshafikia hivi vigezo au inaonekana kabisa kwamba sasa vinaweza kujitegemea kama ambavyo Chuo cha Tengeru kilivyo, navyo viweze kuletwa hapa Bungeni tupitishe Azimio ili ziweze kujitegemea tuzalishe Wataalamu wengi sana katika Kada hii ya Maendeleo ya Jamii.

Pamoja na kwamba, pale Tengeru kuna changamoto mbalimbali kama Taarifa ya Kamati ilivyoeleza na mimi ni Mjumbe wa Kamati, bado kuna tatizo kubwa katika suala la umiliki wa ardhi; bado haijajulikana, kwa sababu kuna sehemu inamilikiwa na Chuo cha Kilimo na kuna sehemu ipo chini ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Kwa hiyo, ni muhimu sana hili suala sasa, tukiifanya Taasisi hii ijitegemee, ni vyema Wizara zinazohusika zikashughulikia suala hili la umiliki wa ardhi. Kuna miundombinu chakavu sana, madarasa, nyumba za wafanyakazi ni chakavu, kwa hiyo, ni vyema sana hizi changamoto Wizara ikaona namna ya kuzishughulikia na kuondoa upungufu huo.

Lipo tatizo la kutokukamilika kwa ujenzi wa Maktaba. Kama Kamati tumeona zinahitajika karibu shilingi bilioni moja kuweza kukamilisha suala hilo la ukarabati na ujenzi wa Maktaba ya Chuo. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara mkaangalia suala hili na Makataba ya Chuo ikakamilika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nitoe wito kwa Wakazi wote wa Mkoa wa Arusha na Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Karatu, Longido, Ngorongoro na Monduli, kutumia fursa hii ya

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kujitegemea. Vilevile kutoa ushirikiano kwa Chuo hiki ili kiendelee kuzalisha Wataalamu wa kutosha na kitoe mafunzo yanayotakiwa kwa kukidhi vigezo tupate Wataalamu watakaoingia katika soko la ajira kwa wingi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Yusufu Salim Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha asubuhi ya leo, kusimama katika Bunge lako Tukufu na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba, Chuo hiki kitatoa Wataalamu ambao watalisaidia Taifa hili kuendelea mbele katika masuala mazima ya kiuchumi. Pia ni ukweli usiopingika kwamba, Wataalamu hawa wataisaidia jamii kujipatia vipato katika maisha yao na pia watalisaidia Taifa letu au Serikali yetu kuondokana na mzigo wa lawama wa Vijana, Akina Mama na Wananchi wengine kukosa ajira. Kwa hiyo, mimi niungane na wenzangu kuishukuru Wizara na Serikali kwa ujumla, kwa kuleta Muswada huu wa kuridhia Chuo hiki kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, nina hofu kidogo na ninaomba nitoe mchango wangu hapa ili hiki Chuo kilete tija na dhamira ambayo imekusudiwa. Nina hofu kwamba; je, tumefanya utafiti wa kutosha kwamba hiki Chuo kinaweza kweli kujiendesha? Kwa sababu nimeangalia katika Ripoti ya Kamati, ukurasa wa saba, Kamati imetoa mapendekezo mengi sana hapa kwamba, kuna changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ikiwemo suala la ardhi, maktaba na miundombinu pale chuoni. Je, haya yamefanyiwa utafiti wa kutosha au tayari yameshawekewa mikakati ya kutosha kuona hiki chuo kitakapoanzishwa basi moja kwa moja kinatupeleka katika lengo ambalo limekusudiwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, tunajifunika shuka kumeshakucha, lakini bado muda upo na tunahitajika kutoa kipaumbele kwa Chuo hiki ili kiweze kutoa matunda ambayo yanakusudiwa. Jamii yetu, ni ukweli usiopingika kwamba, inahitaji msukumo wa uelewa, ni jamii ambayo inafanya kazi. Watanzania wanapenda kufanya kazi sana, lakini namna gani wataweza kutumia fursa katika rasilimali tulizonazo hili ndiyo tatizo. Chuo hiki kitakuwa mkombozi kwa jamii yetu, lakini je, tumewaandaa vipi Walimu na Vijana ambao watatoka pale kurudi katika jamii kwenda kutoa elimu hiyo kwa faida ya jamii na kwa faida ya Taifa kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka kukizungumzia hapa, hiki Chuo kinapewa mamlaka haya ya kujitegemea katika kutoa taaluma. Ninaomba Serikali bado iwe bega kwa bega na Chuo hiki, kwa sababu suala la elimu linahitaji fedha na kurudi ile fedha ikaonekana kwa mara moja inakuwa ni tabu kidogo, kwa sababu elimu siku zote inakula pesa, ni vipi ile pesa itarudi?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iendelee kukiangalia hiki chuo angalau kwa miaka mitano au zaidi ili kuhakikisha kweli sasa kinaweza kusimama chenyewe. Kama Ripoti ya Kamati inavyoeleza, changamoto hizi zinahitaji fedha kuweza kuzitatua na ili vijana watakaokwenda pale wasome na wapate elimu bora ambayo inatakiwa sasa wairejeshe kwa Wananchi na hiyo elimu ikirudi kwa Wananchi sasa izalishe ile fedha irudi kwa Serikali na Jamii, inahitaji mkakati wa kutosha. Tunaiomba Serikali, iendelee kukisimamia Chuo hiki na kukiangalia kwa jicho la huruma kuhakikisha kinafanya kazi vizuri na hakipati matatizo kama haya ambayo yameelezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, suala la vyanzo vya mapato; ni kweli Chuo hiki kitahitaji kuwa na fedha ya kutosha kuhakikisha kinakabiliana na changamoto hizi, kinatoa elimu ya kutosha na kinaondokana na mizozo ambayo itatokea chuoni. Siku zote tunaambiwa mwanzo ni mgumu. Kwa hiyo, mwanzo utakuwa mgumu sana katika Chuo hiki hususan katika suala la fedha ambapo kila siku bajeti zetu zinaonesha tuna upungufu wa upatikanaji wa fedha.

Je, ni mikakati gani ambayo Chuo hiki kimepanga au kimepangiwa kuhakikisha kina vyanzo vilivyo wazi vya mapato lakini vilivyo endelevu kuweza kujitegemea kweli kweli; maana isijekuwa tena ni paka mwizi, tumeshamtia kwenye gunia tunamtupa, Serikali imevua mzigo? Hapana, tuhakikishe kwamba, kuna vyanzo vya kutosha vya mapato na ni vyanzo endelevu ambavyo vitafanya hiki chuo kiweze kujitegemea kweli kweli na kuzalisha tija ambayo tunaikusudia.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ninaishauri Serikali kwamba, iwe imejipanga vya kutosha kuhakikisha bado inakishika mkono chuo hiki mpaka pale ambapo kitaweza kusimama chenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Philipo Mulugo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Azimio hili muhimu kwa uhai na uendelevu wa Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane sana na wachangiaji wengi waliozungumza tena nadhani wote, kwamba, jambo hili ni la muhimu sana na ninakubaliana nalo. Matatizo mengi ya Taasisi za Umma yanatokana na mfumo usio mzuri wa uwezeshaji katika ufanyaji wa shughuli zao. Mara nyingi Taasisi za Umma ambazo ni Idara za Serikali na hasa kwenye suala la mapato kama alivyosema Mheshimiwa Mtanda, zinakusanya fedha kama maduhuli na maduhuli hayo yanaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Matokeo yake ni kwamba, fedha zote zinazokwenda Hazina, zinaingia kwenye Bajeti ya Serikali na zinatumika kwenye bajeti ya jumla ya Serikali kwenye maeneo ambayo si lazima ziwe pale zilipotoka.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limekuwa halizisaidii sana Taasisi na ninakumbuka enzi zile tupo Serikalini, tulikuwa tunazungumzia sana suala hili hasa ukilinganisha kwa mfano ufanisi wa Idara ya Wanyamapori ukilinganisha na Taasisi zinazojitegemea kama *TANAPA* na Ngorongoro. Idara ya Wanyamapori ina uwezo mkubwa sana wa kuzalisha zaidi pengine kuliko hata *TANAPA*, lakini imekuwa haiwezi kwa sababu fedha zote zinazokusanywa zinakwenda Hazina na zikishaenda huko hazirudi. Matokeo yake sasa huu mfumo wa kwamba kiendacho kwa mganga hakirudi, kinawavunja moyo kabisa wafanyakazi, wanakuwa hawana motisha ya kufanya kazi na matokeo yake wanafanya kazi ili siku ziende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Elimu ninadhani hili tunalolifanya au tunalolikusudia kulifanya kwa Tengeru, tulifanye hata kwenye Taasisi zingine. Naishauri Serikali kwa ujumla wake kwamba, ijikite zaidi katika kutoa usimamizi wa ubora wa huduma na Taasisi zote za Huduma za Elimu ziruhusiwe kujitegemea. Serikali izisadie katika hatua za mwanzo tu, lakini baada ya hapo ziweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *performance* ya sekta binafsi kwenye huduma kama za elimu na afya, wanafanya vizuri zaidi kuliko Taasisi za Serikali. Angalia shule za *private*, *performance* yao na uendelevu wao ni mzuri zaidi. *(Makofi)*

Nikupe mfano mmoja ambao nadhani wenzangu katika CCM tunakubaliana; Shule za Sekondari za Wazazi, pale kwetu Kahama tuna Shule ya Sekondari inaitwa Wigehe. Shule ile ipo siku nyingi sana, zaidi ya miaka 30 iliyopita, lakini hadi leo hii huwa tunaichangia wakati mwingine chakula na magodoro wakati wanafunzi wanaosoma pale hawasomi bure. Kwa sababu tu fedha zote zinazoenda pale, zinaingizwa kwenye mfuko ambao hauhudumii shule ile peke yake unatumika pia kwenye shule zingine. Hali hiyo inafanya shule hizi zisiwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia shule nyingine mpya zimeanzishwa nyingi tu akina Mulugo wanazifahamu, kinaanzishwa kishule kimoja kidogo, baadaye viwili na baadaye vine, kwa sababu fedha yote wanayozalisha wanaitumia. Tatizo lingine ambalo tunalo kwenye hizi taasisi ni suala la urasimu katika maamuzi. Taasisi isiyojitegemea maana yake mpaka Ikama ya Watumishi ipitishwe na Ofisi ya Rais Utumishi. Matokeo yake katika mazingira haya ambayo tuna presha kubwa ya kuajiri wafanyakazi kwenye maeneo *sensitive* kama afya na elimu, wanakuwa wanapata mgawo mdogo sana wa Watumishi, matokeo yake mnaweza mkawa mnahitaji, nitoe tena mfano wa wanyamapori huko huko; wanaweza wakawa wanahitaji wafanyakazi na wanasoma kwenye Vyuo vya Mweka na Pasiansi, lakini wanapata kibali cha kuajiri asilimia 30 ya wanafunzi ambao wamehitimu, wengine wote inashindikana kwa sababu kipaumbele cha Serikali ni kuajiri Manesi na Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo kikiruhusiwa kujitegemea, kitaweza kuajiri bila urasimu wowote na pia kitaweza kutumia fedha zake zote ambazo wanazipata kwa ajili ya uendeshaji. Kubwa, Vyuo hivi vitapata *business mentality*, kwa sasa hivi kwa sababu wanafanya kazi kama Idara ya Serikali, ule uwezo wa kufikiria *strategically*, uwezo wa kubuni mikakati ya kufanya Chuo kizalishe zaidi na zaidi na wapate faida itakayowawezesha kupanuka, inakuwa haipo kwa sababu wanajua hata wakifanya hivyo juhudi zao hazitakuwa *immediately rewarded.* Fedha watakazokusanya na juhudi watakazofanya, zitakwenda kutumbukizwa, kwa maana ya mapato, yatatumbukizwa kwenye kapu kuu la Serikali na wao hawatanufaika moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pamoja na kukubaliana sana na hili Azimio, ipanue wigo, Vyuo kama *CBE* na *IFM* ambavyo kwa kiasi kikubwa vina sura kama hii, ada inayokusanywa inaenda Serikalini kama maduhuli na wanapata bajeti fulani ambayo wanapangiwa. Wakiruhusiwa waweze kutumia fedha zote wanazozi-*raise* wataweza kupanua huduma, kuboresha huduma na watafanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kupongeza sana Azimio hili na kuisisitiza Serikali ipanue wigo. Vilevile hata kwenye maeneo mengine kama nilivyotoa mfano kwenye Taasisi za Elimu kama Shule za Wazazi, nazo ziruhusiwe kujitegemea kila shule ilivyo kama *stand alone institutions* zitaweza kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, ilimradi ninyi msianze kulalamikia ada, mkilalamikia ada kubwa haiwezekani tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Philip Mulugo atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya pekee na mimi niweze kutoa mchango wangu wa mawazo, lakini hasa kuunga

hoja Azimio hili ambalo angalau ninalifahamu vizuri toka nikiwa pale Wizarani. Nami nimeshawahi kusafiri na Kamati mpaka kwenda kukiona Chuo hicho.

Ninataka kuwashawishi Wabunge, japo leo siyo ushawishi mkubwa sana kwa sababu hata pande zote mbili tumekubaliana kwamba wazo hili ni zuri. Naendelea kusema kwamba, nawashawishi tuunge mkono hoja, kwa sababu tayari watu wa viwango wanaoangalia masuala ya Vyuo hivi, Watu wa *NACTE,* tayari walishafika pale na walishakipa sifa hiki Chuo kwamba, kinaweza kikapata ithibati au *accreditation,* kwa ajili ya kutoa mafunzo haya ya Shahada ama kujitegemea kama ambavyo hoja imekuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuungana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Namwona Dada yangu Jenista yuko pale ameleta hoja hii. Nami nataka kusema kwamba, Mbunge wa Jimbo la Songwe, Chunya kule tuna chuo tunakiandaa kwa mifumo hii ili na sisi baadaye tuje tulete hoja ya kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Chuo hiki tayari kimeshapeleka Wahadhiri kwenda kusomea ili kuweza kupata Shahada za Uzamivu na Uzamili kiweze kuwa na sifa kamili ya kuwa Chuo kinachojitegemea. Vilevile kama ambavyo Kamati wamesema, hiki ni Chuo pekee katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati ambacho kinatoa fani za Maendeleo ya Jamii katika nchi hizi. Nadhani tukisharidhia hoja hii tutapata sifa kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania kuwa na chuo cha pekee kinachotoa fani hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama tunapongeza lakini ni lazima tutoe changamoto kidogo ambazo Kamati wamebaini na mimi mwenyewe tulipoenda Tengeru tulizibaini hasa kuhusu suala la eneo. Chuo hiki kina uhitaji wa hekta 40, lakini tayari hawana hati miliki. Naishauri Serikali na naona Naibu Mawaziri wote wawili wamekaa pale wanaungana, naomba hii hoja ipelekwe kwenye mjadala mkubwa Wizarani, muweze kujadili suala hili ili angalau Chuo kiweze kupata hati miliki, kiwe *autonomy* ya kumiliki ardhi yake na kiweze kujiendesha vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia upo upungufu wa jengo la maktaba, ambalo Serikali ikiweza kutoa bilioni moja kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii amesema hapa, wanaweza wakakidhi kujenga maabara ya kuchukua wanafunzi zaidi ya mia mbili kwa wakati mmoja. Sijajua kwa sababu bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na bajeti ya Maendeleo ya Jamii tayari zilishapita, sijui tunaongelea katika bajeti ambayo imeshapitishwa au tutaliongea mwaka 2015/2016?

Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha, aweze kuliangalia hili. Hii bilioni moja ambayo inatakiwa tunaiombea sasa kwa baadaye au tayari imo kwenye bajeti ya hizi Wizara zote mbili ambazo zilikuwa zimepitishwa wiki zilizopita?

Mheshimiwa Spika, tumepata changamoto vilevile ya Chuo hiki kukosa ruzuku Serikalini, inapata kidogo. Nataka niwahakikishie Wabunge kwamba, baada ya Chuo hiki sasa kujitegemea, tayari wale wanafunzi watapata sifa ya kusoma digrii, maana yake watasoma zile shahada ambazo wanafunzi watakuwa na sifa ya kukopeshwa mikopo na chombo chetu kikubwa cha Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo huwa hawakopeshi wanafunzi ambao hawasomi Shahada za Kwanza, wanakopesha wanafunzi wanaokuwa na sifa hizo, hawakopeshi kwa ngazi za *Diploma* na kitu kingine.

Wanafunzi hawa watakapokuwa wengi kutokana na zile programu ambazo Chuo kikishajitegemea zitaanzishwa, maana yake watakuwa na sifa ya kukopesheka. Kwa hiyo, ni wazi kama Mheshimiwa Machali alivyokuwa na wasiwasi labda Chuo kitaanza sasa kukosa

fedha na nini; nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Machali kwamba, Chuo kitakuwa na wanafunzi wengi, halafu watakuwa na sifa za kukopesheka na haya ndiyo yatakuwa mahuduri ya chuo kwa ajili ya kupata ada nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Chuo kikishakuwa na *autonomy,* kitaongeza udahiri mkubwa sana katika fani hizo na hivyo kuwa na wanafunzi wengi. Tulipoenda pale tuliona eneo linatosha na watu wa *NACTE* tayari walishaleta ithibati kwamba, Chuo kinaweza kikawa na sifa ya kuwa na uwezo wa kujiendesha chenyewe.

Mheshimiwa Spika, nilitaka angalau na mimi nitoe mchango huo kwa jambo hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nianze kwa kusema kwamba, mimi ni Mwanakamati na Ripoti yetu imewasilishwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Sitta, Magaret. Ninayo mambo machache tu ya kusisitiza.

Mheshimiwa Spika, kinachoongelewa hapa kinahusiana na changamoto kubwa ambayo imezishughulisha Serikali zote za Awamu Nne; changamoto hiyo ni maendeleo ya Jamii na hasa Maendeleo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wamekuwepo kwa Awamu zote hizo kama mimi, maendeleo vijijini yalimshughulisha sana Rais wa Kwanza wa nchi hii na ameandika sana kuhusu maendeleo vijijini. Yeye kwa wakati wake kwa Awamu ile alijitahidi sana, lakini hapa katikati kumetokea mambo ambayo yameturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni ya kuunga mkono na ndiyo maana Kamati tumeiunga mkono, Upinzani tumeiunga mkono na kila mtu ameiunga mkono. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kuna mambo ya kuangalia. Kwanza kabisa, ni Wizara na Chuo chenyewe kiangalie kwanza mitaala. Mitaala ya mwaka 1963 ni tofauti na mitaala ambayo inafaa kwa wakati huu. Kama tunavyofahamu, changamoto ambazo zinatukabili sasa hivi ni tofauti na zilizokuwa zinatukabili mwaka 1963. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko vijijini, ile misimu kwa mfano ya mvua haipo sawa tena. Kwa hiyo, masuala ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima yazingatiwe katika mitaala hiyo. Masuala ya nishati mbadala ni lazima yazingatiwe katika mitaala hiyo, sijui kama yanazingatiwa, lakini ni lazima yazingatiwe. Kuna matatizo mbalimbali ya kiafya ambayo yamezuka siku hizi ambayo huenda mwaka 1960 na kuendelea katika miaka hiyo ya 60 na 70 hayakuwepo. Ili kubadilisha hali huko vijijini, inabidi mtaala uwe wa kisasa na uhusike na sekta zote za maendeleo kama yanavyofahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mitaala nimelizungumzia hivyo. La pili, ambalo tumelizungumzia katika Taarifa ya Kamati ni sifa za kitaalam za uongozi na wakufunzi. Sisi Kamati hatukuwa na shida sana na jambo hili, ila tulisisitiza tu kwaba jambo hili lisimamiwe vizuri na Wizara.

Wale ambao wanasomea masomo ya Uzamivu ni watano nadhani, wamalize haraka na wale wanaosomea Shahada ya Umahiri wamalize haraka, nadhani ni watatu na wengine ambao hawajaanza kujisajili na masomo ya Umahiri, Umahiri ndiyo *Masters* na Uzamili ni *Postgraguate Studies*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na wengine ambao hawajajisajili wajisajili wasome. Hilo tunashauri tu kwamba Wizara ilisimamie na kwa sasa Shahada ambayo inaruhusiwa kufundishwa tu pale iwe ni Shahada ya Kwanza tu. Kwa sababu hawa ambao wanasoma, wote bado wanasoma, watawezaje kufundisha Shahada ya Pili au ya Tatu. Kwa hiyo, wafundishe tu Shahada ya Kwanza kwa miaka kama mitatu, minne hivi. Halafu baadaye wakishakuwa wengi ambao wana Shahada za Uzamivu, Shahada za Umahiri na nyinginezo zianze kufundishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo suala la kitaalam tuliwaachia Wizara walisimamie. La tatu, linahusu kiasi cha fedha ambacho kinahitajika kukamilisha jengo la Maktaba, jengo la Utawala na ukarabati wa miundombinu mingine katika Chuo hicho. Tunaiomba Serikali, tulishauri Serikali kwamba itoe hiyo fedha, kama hatua ya dharura kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hilo eneo. Eneo kwa kweli ni dogo, kama wenzangu walivyosema waliotangulia. Eneo kwa kweli la Chuo ni dogo, lishughulikiwe ili chuo kipate eneo la kutosha na la mwisho, tumependekeza kwamba Serikali iwe na mkakati mahususi na tulipendekeza hivyo tukifahamu kwamba Wataalam wa maendeleo ya jamii wamekuwepo kwa muda mrefu sana. Tunao katika Wilaya lakini hawafanyi kazi kwa sababu hatuna fedha. Kwa hiyo, tumependekeza kwamba Serikali iwe na mkakati mahususi wa kutoa fedha za kutosha ili Wataalam hawa waweze kufanya kazi ya kubadilisha hali katika Vijiji vyetu. Hali siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni suala tu la Serikali kuwa na mkakati mahususi. Sidhani kama ni suala la Wizara ya Elimu au Wizara ya Maendeleo lakini ni suala la Serikali kuwa na mkakati mahususi kabisa. Inabidi warejee huko nyuma miaka ya 1960 na 1970, Awamu ya Kwanza, nini kilifanyika kwa sababu yalikuwa yanakwenda Vijijini. Siku hizi hayaendi, kwa nini hayaendi? Wajiulize!

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache Mheshimiwa Spika, nakushukuru asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rebecca Mngodo!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Nianze kwa kusema kwamba, suala hili tumeanza kuliunga mkono mara baada ya Waziri aliposoma Azimio hili na vile vile tumemwunga mkono Mwenyekiti wa Kamati na hata Kambi ya Upinzani imeunga mkono suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa mantiki hiyo, Wabunge wote ambao wamechangia Azimio hili wameunga mkono na mie kwa upande wangu naunga mkono. Chuo ni ukombozi. Ni ukombozi wa Taifa lolote na kwa wananchi wote. Chuo ndicho kinachozalisha wataalam, wasomi na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki, kitatoa elimu na mafunzo mengi, yakiwemo mafunzo ya ufundi. Vile vile Chuo hiki kitaleta heshima kubwa kwa Taifa letu kwa wale watu ambao,

wasomi ambao, wataalam ambao, watatokana na Chuo hiki. Naamini mpaka kukubalika kuwekwa Chuo hiki, ambacho kitajitegemea, basi naamini kwamba utafiti mkubwa umeshafanyika na kwa sababu utafiti umeshafanyika naamini kwamba utekelezaji wake au utekelezwaji ndani ya Chuo hiki utakuwa na ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, vile vile, niseme kwamba ni kweli kwamba Serikali haiwezi kuajiri wataalam na wasomi wote. Sasa kupitia Chuo hiki naamini kwamba wataalam na wasomi ambao watapitia Chuo hiki wataweza kufungua mitaji ya ajira kwa kujiajiri wao wenyewe, lakini vile vile na kuajiri watu wengine ndani ya Taifa hili. Kwa hivyo, Chuo hiki kitasaidia mzigo mkubwa kwa Serikali hapo mbeleni na kutoa mwangaza mkubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, suala moja ambalo limelalamikiwa ni eneo la ardhi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba na ni muhimu eneo la ardhi liweze kupatikana ili Chuo kiweze kuwa na eneo, lakini vile vile kuwa na hati miliki ya ardhi hiyo ambayo watapewa. Vile vile niseme kwamba ujenzi wa Chuo hiki au uendeshaji wa Chuo hiki isiwe kikomo.

Mheshimiwa Spika, kuna haja na wajibu wa kufungua Vyuo vingine kama hivi ambavyo tunaweza tukasema kwamba ni matawi ya Chuo hiki ambayo yataweza kuiendeleza nchi yetu na ni vema suala hili likaangaliwa na upande wa pili wa Muungano ili kuweza kufunguliwa Chuo kama hiki ambacho kitaweza kuleta maendeleo na ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba hii ni nia njema na nia njema hii nina hakika kwamba italeta matunda. Vile vile niseme kwamba wenzangu wamezungumzia kuhusiana na suala la vyanzo vya mapato. Kukipa uhuru Chuo wa kuweza kujitegemea nasema kwamba kitaweza kupata fursa ya kutafuta misaada na mikopo nje na kwa hivyo kwa njia hiyo Chuo hiki kitajiendeleza kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali inapokuwa na uwezo, nayo isione ubaya wala hasara kukisaidia Chuo. Kwa hiyo, wale waliosema kwamba Serikali isije ikabweteka ikakiachia hiki Chuo mzigo wote, basi Serikali ina wajibu wa kukiangalia vile vile Chuo hiki ili kisije kikasita katika kujiendeleza kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba penye Vyuo vyovyote vile basi ajira zinakuwepo kwa wingi, ajira imara na naamini kwamba Chuo chetu hiki kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na Baraka za Mtume, basi kitakapoendelezwa katika misingi ambayo imekusudiwa, imedhamiriwa, basi tutafika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Rebecca Mngodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk. Ukiongea usiwaangalie wenzio utakosea maneno.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu katika Azimio hili la Bunge la kuridhia Chuo cha Maendeleo cha Tengeru kiweze kujitegemea kiutendaji. Katika maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri, alisema kwamba Serikali kwa muda mrefu imefanya jitihada ili kuweza kukifanya Chuo cha Tengeru kiweze kujitegemea kiutendaji, naona kwamba ni vema vyuo vingine vya maendeleo ya jamii pia vikapata nafasi kama hii ya Tengeru. Kwa sababu nakumbuka nilipokuwa katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii tulipata nafasi ya kwenda Mwanza kukitembelea Chuo kimojawapo cha maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali ya Chuo kile haikuwa na tofauti kama Chuo cha Tengeru. Matatizo yaliyoko Tengeru ya miundombinu, ya upungufu wa Walimu, upungufu wa maabara na maktaba tuliyaona pia katika vyuo vingine ambavyo tulikuwa tumevitembelea.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Tengeru nimekifahamu kwa muda mrefu, ni chuo ambacho kiko katika mandhari nzuri ya Mkoa wa Arusha. Kutoka Januari mpaka Desemba Chuo kile ni kijani. Kinaweza kuvutia wanafunzi wengi kutoka nchi washiriki wa Afrika Mashariki na hata katika nchi zingine za ulimwenguni kama kitapata ridhaa hii ya kuweza kujiendesha chenyewe kwa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, pia naamini kwamba bajeti iliyokuwa imetengwa ya bilioni 30 katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni pesa kidogo sana ambazo zisingeweza kutosha kwa Wizara kujiendeleza katika shughuli zake mbalimbali na pia kuweza kuendeleza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni vya muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka miaka ya nyuma, Mabibi Maendeleo, Mabwana Maendeleo, walikuwa wanaonekana mpaka kule vijijini, lakini siku za leo wamebaki katika Halmashauri. Ukiangalia Bwana Maendeleo wa Halmashauri ya Meru kwa mfano, ni mtu ambaye anakaa tu Ofisini, hana vitendea kazi. Anakaa Ofisini kwa sababu hana shughuli maalum ya kila siku kutokana na fedha kidogo ambayo inatengwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo ningependekeza basi kwamba, Tengeru itakapokuwa imeanza kujiendesha yenyewe kwa kujitegemea, *product* itakayokuwa inapatikana pale, wanafunzi watakaokuwa wanamaliza pale, nashauri kwamba Serikali iweke umuhimu mkubwa katika kuwapa ajira ili waweze kufika chini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasiishie tu katika ngazi ya Halmashauri, lakini napendekeza kwamba waende mpaka vijijini, ingawa naona pia Kamati ya Maendeleo imeshauri kwamba waishie kwenye Kata, lakini ni sawa, wakiwa kwenye Kata wataweza kufika pia katika Vijiji kwa maana watakuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasaidia wanawake, vijana na jamii mzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuzungumzia ardhi ya pale Meru kwamba Tengeru pale ile ardhi ni kidogo sana na mpaka sasa hakuna hati miliki. Naomba kwa umuhimu mkubwa Chuo hiki kiweze kupatiwa hati miliki ili kiweze kumiliki ardhi ile. Kwa sababu kitakapokuwa kimemiliki ile ardhi kitaweza kujiendeleza hata kwa kujenga maghorofa kwa sababu hekta 40 zile siyo nyingi, lakini Chuo kitaweza kujenga kwa kwenda juu badala ya kwenda kwa kujipanua zaidi kwa sababu ardhi ile haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba sana Serikali ilichukulie kwa umuhimu mkubwa jambo hili ili kile Chuo kiweze kuwa na hati miliki na hivyo kiweze kumiliki ardhi ile. Pia Maktaba ile ambayo kwa miaka nane sasa haifanyiwa kitu chochote kwa miaka nane jengo lile la Maktaba nikipita pale kila mara naliona liko vile vile.

Mheshimiwa Spika, naomba sana fedha hii ambayo Kamati ya Maendeleo ya Jamii imeomba ya shilingi bilioni moja iweze kutolewa, kwa sababu sijui kama pale katika zile bilioni 30 za Wizara sijui kama hii fedha pale ipo, sielewi. Naomba fedha hii itolewe kusudi Maktaba hii iweze kumalizika na miundombinu mingine ya pale Chuoni iweze kumalizika ili Chuo hiki kiweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, napenda kupendekeza kama Chuo hiki kitaanza kujitegemea kiutendaji, fedha yote itakayokuwa imepatikana baada ya wao kufanikiwa kibiashara, basi ile fedha iweze kubaki pale ili waweze kujiendeleza zaidi badala ya kusubiri tena fedha itoke

Hazina, lakini badala yake waweze sasa kujiendesha wao wenyewe kwa fedha ile ambayo watakuwa wanaipata pale. Naamini kwamba wataweza kuwa na *website* yao, wataweza kujitangaza ndani na nje ya nchi na wataweza kupata pia *exchange programmes* kutoka vyuo vingine duniani kwa sababu wataweza kuwa wamejitangaza vizuri katika *website* yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii ambayo ni ya muhimu sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema namwita Mheshimiwa Rajab Mohamed, *then* atafuatia Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilianza awali naunga mkono hoja. Naiunga mkono hoja hii kwa masikitiko makubwa hasa nikizingatia kwamba Serikali kwa kupitia Bunge ndiyo ambayo imeleta Azimio hili ili tuliridhie, lakini nikiangalia hali halisi ya safu ya Serikali haionekani. Walioko hapa ni Mawaziri wanawake watupu, enhe, samahani yupo Mheshimiwa Mzee Mwandyosa. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kwa kweli Mheshimiwa Spika, hali hii

**SPIKA:** Waombe radhi. *(Kicheko/Makofi)*
**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Nakuomba radhi Mheshimiwa Mwandosya.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kwa kweli kina historia kubwa, ni Chuo ambacho kimeanza au kimejengwa takribani miaka 50 iliyopita. Ni Chuo kikongwe kati ya Vyuo ambavyo vipo nchini kwetu. Ni wakati kwa kweli muafaka kwa Serikali kuweza kuleta Azimio hili Bunge liridhie sasa Chuo hiki kiweze kujitegemea. Naamini kwamba ndani ya miaka hiyo 50 wamekumbana na changamoto nyingi, lakini wameweza kujifunza mengi, kitu ambacho kitawasaidia katika kwenda mbele vizuri.

Mheshimiwa Spika, moja ya faida au baadhi ya faida ambazo kwa kweli Chuo hiki kinaweza kuzipata ni suala zima la kuingia ubia. Kuingia ubia ama na Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, lakini vile vile na Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi. Wanapoingia ubia hawa ambao wameingia ubia watakuwa na uwezo na nafasi ya kuwekeza katika Chuo hiki. Wanaweza kuwekeza katika miundombinu pamoja na mambo mengine ambayo kwa kweli yataweza kusaidia kuendeleza Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, vile vile mbali ya kuwekeza, lakini hata suala au matatizo ambayo yanajitokeza mara nyingi katika Chuo kile ya ukosefu wa mishahara au kuchelewa kupatikana kwa mishahara, naamini sasa kwa kutumia Bodi yao ambayo itaundwa kama ambavyo Mheshimiwa Paresso ameshauri kwamba, hii Bodi ni bora iharakishwe, naamini hata mishahara yao sasa hivi itakuwa inakwenda kwa wakati na haitaweza kuchelewa. Vile vile ni kuweza kuongeza *program* za masomo.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati nilimpongeza sana Mama yangu Mama Sitta, kwa taarifa yake nzuri imezungumzia Serikali kuandaa mikakati mahususi ya kuajiri na kuwatumia Maofisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ya *LAAC* mara nyingi tunapokwenda kukagua mahesabu katika Halmashauri tunakuwa tunapata matatizo sana na hawa Maofisa wa Maendeleo ya Jamii. Kwanza kwa kutokujua wajibu wao, lakini pia kwa kutokujua nini

ambacho kimewaweka pale ili waweze kufanyia kazi. Pia hata zile haki ambazo zinatakiwa zitolewe na Halmashauri kwenda kwa wananchi au kwenda kwa jamii pia inaonekana hawajui namna ya kuzifuatilia ama kuzidai katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, watu hawa wanatakiwa wawe wanadai zile pesa asilimia tano ambazo zinakusanywa na Halmashauri kwa ajili ya kuwapelekea akinamama na vijana, lakini sasa kutokana na kwamba hawaelewi basi wanakuwa wazito kuweza kuzifuatilia. Ni imani yangu sasa, Chuo hiki kitakapokuwa sasa kimeweza kujiendeleza au kuongeza *programmes* za masomo basi kitatoa watu wazuri ambao watasaidia sana katika kuendeleza Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ni kwamba, Chuo hiki kitaweza kuzalisha wataalam zaidi hasa wataalam ambao wataweza kukabiliana hasa na matatizo ambayo sasa hivi yanaikumba nchi yetu; suala la ubakaji, vitendo vya ukatili wa kijinsia na mambo mengine ambayo naamini mitaala ambayo itakuweko sasa hivi ambayo tutaachana na ile mitaala ya mwaka 1963 kwa kuanzisha mitaala mipya. Naamini kwamba haya na hapa Chuo hiki kinaweza kuzalisha wataalam ambao *seriously* sasa wataweza kupambana na suala hili zima la ukatili ambalo kwa kweli linaleta matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile niseme tu kwamba na niitake Serikali kwamba, hata mtoto unapomzaa hawezi kutembea kwa siku moja, lazima kwanza umlelee, ukae naye, umfundishe, unde naye vizuri. Tuiombe tu Wizara na tuiombe Serikali isiwe sababu ya Chuo hiki kukiacha mkono. Ni vyema sasa Serikali bado iendelee kukitazama Chuo hiki na indelee kwa kweli kukipa misaada yote inayohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Pamoja na Azimio alilosoma Mheshimiwa Waziri, lakini nadhani kuna *Tengeru Institute of Community Development Established Order 2013.* Nadhani mnapojadili mnacho hiki kitu, kwa sababu mengi mnayosema kama yamo humo. Sasa nimwite Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Azimio hili na moja kwa moja naunga mkono Azimio lililoletwa. Wakati huo huo nakubaliana na kila kitu kilichomo katika Taarifa ya Kamati kwa sababu mimi ni Mwenyekiti na yale yote yaliyoletwa humu ni uamuzi wa Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyomalizia Mheshimiwa Rajab, naomba niongezee pale pale. Suala kubwa alizolizungumzia Mheshimiwa Rajab ni suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kuwa Tengeru katika moja ya Mahafali ya Maafisa Maendeleo ya Jamii na kwa bahati nzuri siku yenyewe Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huyu huyu tuliye naye Mheshimiwa Pinda.

**SPIKA:** Na wewe ulikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii siyo?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Ahsante kwa kunitaja. Risala waliyotoa wanachuo waliokuwa wanamaliza, wahitimu, ilikuwa ni ombi la kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwa nini Serikali haiajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii. Wao kazi yao kubwa kama alivyokuwa amezungumzia Mheshimiwa Wasira, wamesomea *sociology* yaani kumwelewa binadamu, *psychology* wajua jinsi ya kuongea na binadamu, wanaweza kumhamasisha, wanaweza kumwelimisha, wanaweza na kumshawishi pia kwenye masuala ya kujiletea maendeleo wenyewe. Nashangaa kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwaajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Kata zipatazo 3,500 mpaka sasa hivi na utashangaa Kata zipatazo asilimia 39 tu kati ya hizo 3,500 ndiyo zina Maafisa Maendeleo wa ngazi ya Kata. Kwa hiyo, jambo kubwa hapa la kuzungumzia ni kwamba jinsi gani Serikali imejipanga ili kuwaajiri Maafisa Maendeleo waende hasa kwenye ngazi ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza tutakuwa tumepata ajira 3,000 kwa mfano wakichukua Kata zote, ajira 3,500 ni nyingi sana kwa vijana wetu wanaomaliza vyuo. Wakati huo huo ni muhimu sana, fikirieni nyie wakati wa ukoloni, hawa ndiyo waliokuwa wakitumika hasa katika zile *Community Centres* kama mtakumbuka, yale Majumba ya Maendeleo yale ambayo kwa sasa hivi bahati mbaya ndiyo yamegeuzwa *bar,* mengine wamegeuza sijui wanayafanye wenyewe. Lengo lake *the Community Centres* ilikuwa ni kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii kutumia zile *Centres* kuwaelimisha watu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kupongeza Wilaya ya Mufindi. Nilifika Wilaya ya Mufindi, nikafurahi sana na utaratibu wao, naamini bado wanaendelea. Wao wamechukua Maafisa Maendeleo katika nyanja tofauti. Yaani wamechukua Maafisa Maendeleo wanashughulikia suala la elimu tu. Kwa hiyo kipindi cha kuandikisha yeye ndiye anayezunguka kuhamasisha wazazi kupeleka watoto shuleni au mwingine ama anashughulikia masuala ya afya tu.

Kwa hiyo, panapokuja maradhi kama haya labda *dengue* na mengineyo, ndiyo wanapita kuelimisha jamii. Kwa hiyo, wamewachukua Maafisa Maendeleo kulingana na Sekta mbalimbali. Ningetoa wito kwa Serikali tuige mfano wa Mufindi, Afisa Maendeleo mmoja tu ndiye anashughulikia elimu, kilimo na maji na nini kuhamasisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mufindi wamefanya vizuri sana. Nawaomba waendelee hivyo hivyo na Wilaya zingine ziige mfano huo na nashukuru Mheshimiwa Celina Kombani yupo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi aangalie suala hilo la ajira ili Kata zote nchini ziajiri Maafisa Maendeleo Kata, lakini wakati huo huo kwa kuwa tulitoa ombi wakati huo na naamini bado Waziri Mkuu analikumbuka, aagize TAMISEMI wawaajiri hawa Mafisa Maendeleo ya Jamii ili wafanye kazi kama nilivyosema ya kuhamasisha, kushauri na kuelimisha, yaani wanashauri, wanahamasisha, wanaelimisha pia katika watu kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, la pili, siyo kuwaajiri tu, kwa mfano, kwenye ngazi ya Wilaya, wale Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Wilaya walikuwa hawapati hata senti moja, lakini Serikali ikasikia kilio chao, wakaanza nadhani mwaka wa kwanza nadhani wakaanza kuwapa milioni tatu kwa mwaka, baadaye wakaongeza kidogo milioni saba.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kutokana na umuhimu wa kazi zao, kuna umuhimu sana wa Maafisa Maendeleo ya Wilaya kupewa fedha katika Idara zao ili wawawezeshwe, wale walioko kwenye ngazi ya Kata wafanye kazi zao. Nasikitika mnaweza kufikiri pengine hawajui kazi zao, wanaweza kuwa wanazifahamu kazi zao, lakini kama hawakuwezeshwa, hawakupewa vyombo vya usafiri, hawapewi hata baiskeli hawapewi hata pikipiki watafanye kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kata zetu, labda wenzetu wanaotoka Zanzibar, karibuni tena muone Kata zetu za Urambo na kadhalika mtashangaa  Kata ni siku nzima unatembea hujaimaliza. Sasa atakwendaje kama hakupata chombo cha usafiri?  Kwa hiyo, nafikiria wapewe fedha, lakini pia wawezeshwe wapewe vyombo vya usafiri.  Mmoja nadhani kama sikosei nilimkuta Butiama anatembea na baiskeli, anasema nimetoka kutembelea vijiji na kadhalika kuwahamasisha mambo ya surua na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo yanayotakiwa.  Kwa hiyo, wapewe fedha, lakini pia wawezeshwe.  Kwa hiyo, kwa kweli nafurahi sana na hili Azimio la leo, naona ni ukombozi mkubwa sana.  Kwanza napongeza uongozi wa Tengeru uliopo sasa hivi, Walimu wote wanafanya kazi nzuri, lakini haisaidii kuongeza wanafunzi kama hatutawachukua na kuwaajiri.

Mheshimiwa Spika, naamini Serikali imenisikia na naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimiza hili suala naomba tulitilie maanani na hata Mawaziri wengine wanaohusika wakizungumzia juu ya kuwaajiri vijana ambao tutawaongeza zaidi kule, itakuwa vizuri, hata kwa sasa hivi, wamo Maafisa Maendeleo ya Jamii wapo wengine wameajiriwa na *NGO's*, lakini wako wengi ambao wamemaliza mafunzo wako mitaani.  Kwa nini wakati tuna Kata 3,500?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuwaajiri hawa.  Kwa hiyo, nafurahi kwamba leo tutapitisha Azimio hili.  Nakubali naona wote pande mbili tumekubaliana kwamba tunaazimia, lakini tuwatumie watakaopata mafunzo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.  *(Makofi)*

**SPIKA:**  Waheshimiwa na mimi niseme niliwahi kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.  Suala hili ni kubwa, ingawa tunaliona kama ni dogo, lakini ni kubwa.  Kwa sababu kama mlivyosema *population* yetu kubwa inahitaji kabisa kabisa kuamshwa katika vitu fulani fulani.

Kazi hii ilikuwa ni ya hawa wa Maendeleo ya Jamii.  Kwa hiyo, ilianza kupungua kasi yake moja kwanza iliyosaidia ni hii miradi ya Kimataifa, maana wale wanawalipa hela kubwa, wanawapa *facilities,* wakiondoka hao sisi huku tunashindwa kufanya, lakini hiyo siyo sababu, ya kutufanya sisi tusiweze kufufua kada hii katika maeneo yetu ya vijijini.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo, napenda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wafoto pamoja na mtoa hoja wakakae wakajipange vizuri siyo suala la *Institute* hii tunayozungumza, I*nstitute* hii itatoa wataalam kweli, lakini kuna bado kada ya Maendeleo ya Jamii na hii ni shughuli ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii.  Kwa hiyo, nataka nitoe muda wa kutosha mkajiandae vizuri, mtujibu siyo kama mnajibu darasani hapa, mtujibu vizuri kisera, kisera hivi.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.  Mmeelewa hapo saa 11 siyo saa 10, saa 11 haya.  *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 6.30 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.  Katibu!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba niunge mkono Hoja ya Azimio hili moja kwa moja. Naomba nichangie suala moja tu ambalo Waheshimiwa wengi Wabunge wame-*raise concern* kuhusu ajira za Maafisa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo tunalitambua sana kwamba, ni tatizo, lakini mkakati wa Wizara yangu kwa miaka karibu saba iliyopita tuli-*concentrate* sana kwenye kada za afya pamoja na elimu, kilimo pamoja na mifugo. Baada ya kuangalia kwa undani tukaona tuna tatizo kubwa la kada nyingine. Matokeo yake kuna *gape* kubwa sana kati nya vijana na wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ule mkakati wetu wa *succession plan* tukaona kwamba, tutakwama huko mbele ya safari, hilo *gape* tutaliona kwa wale ambao walikuwepo miaka ya 90, 80, wakati ule tulifanya *retrenchment gape* likawa kubwa sana. Hatukuajiri kwa miaka 10 watumishi. Kwa hiyo, utaona hilo *gape* tunaliona sasa hivi, wakati ule tulikuwa hatulioni kwa hiyo, hilo nalo tumeliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeanza mkakati wa kuajiri kada mbalimbali. Kwa mwaka huu kwa upande wa maendeleo ya jamii tume-*concentrate* zaidi na Vyuo vya *FDC,* kwa sababu ndiko tunakofundisha vijana wetu kazi mbalimbali za kuweza kwenda kujitegemea. Kwa hiyo, kwa upande wa *FDC* tumewapa kibali cha watumishi kama 260, ili tuwatawanye katika hizo *FDC*.

Mheshimiwa Spika, kada nyingine kwa mfano Mipango tukakuta kabisa kwamba, tuna *gape* tutaajiri *economists* karibu 100, tutaajiri *HRs* karibu 200, tutaajiri watu wa ardhi ni kwa sababu tumeona kwamba, huko mbele ya safari kama kweli tuna nia ya mkakati wa *succession plan* tumeona kwamba, tutakwama. Kwa hiyo, tumeanza kuajiri hizo kada. Sasa tunaziangalia kada kwa kada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuahidi kwamba, hili la watumishi wa maendeleo ya jamii ni kweli, watumishi wa maendeleo ya jamii ni *multipurpose,* hata nalifahamu hilo. Hata enzi za zamani ukiangalia *DCs* wengi ni wale waliokuwa na *qualifications* za maendeleo ya jamii. Maendeleo ya jamii ndio wenye uwezo wa kuhamasisha watu wetu katika maendeleo kwa sababu ya ile *sociology* ambayo wamesomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tu, miradi yetu mikubwa mikubwa hii, *PADEP, ASDP, TASAF,* usipokuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii kuhamasisha watu, mradi huo hauendi. Kwa sababu gani, wale wana vipaji vyao na kama nilivyosema wamesoma ile *Sociology* kwa hiyo, wana uwezo wa kumshawishi mtu, lakini Afisa Kilimo atoke hapa aende kijijini, ataongea tu mambo yake *technical,* lakini hasa kuhamasisha wananchi ni kazi ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeutambua huo umuhimu na kuanzia mwaka ujao tutaanza kuajiri hao Maafisa Maendeleo ya Jamii, ili waweze kukidhi mahitaji ya maendeleo katika Kata zetu, hasa tutaanzia katika *level* ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa hilo agizo akasema kwamba, tuwatumie hao Maafisa Maendeleo ya Jamii, kama alivyosema Mheshimiwa Sitta, tulikuwa wote kwenye hiyo ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aliagiza akasema kwamba, tuwaajiri hao Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini tuliona kwamba, tuanze kwanza na hii kada ambayo inawafundisha watu wetu kule vijijini hasa kwenye *focal development,* kwenye Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa hiyo, hili linafanyika, mwaka ujao tuta-*make sure* kwamba, tunaweka Maafisa Maendeleo ya Jamii wengi, ili waweze kukidhi mahitaji ya kuhamasisha wananchi katika miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nami tu nitoe wito kwa wenye miradi mbalimbali, hasa kwenye Halmashauri; miradi ile ya *PADEP,* miradi ya *ASDP, TASAF,* miradi ya maji, wasimwache Afisa Maendeleo ya Jamii wakati wanakwenda kuhamasisha wananchi. Wale ndio wenye uwezo wa kuwahamasisha hao wananchi na hela zinatoka wapi? Kila mradi una hela za *supervision.* Kwa hiyo, wasile peke yao zile hela za *supervision,* wawachukue na hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii, ili waende wakawasaidie katika kuhamasisha wananchi katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lile alilosema Mama Sitta kule Mufindi kwa kweli, ni wazo zuri. Naomba tulichukue tulifanyie kazi, ili Afisa Maendeleo anaye-*deal* na mambo ya afya a-*deal* na mambo ya afya; anaye-*deal* na mambo ya kilimo a-*deal* na mambo ya kilimo na Maafisa Maendeleo ya Jamii wengine ni *multipurpose* kwa sababu, wamesomea *Project Planning,* kwa hiyo, hata kwenye mipango pia, kama tunavyosema kwamba, mara nyingi tunataka mipango yetu iwe *gender sensitive,* kwa hiyo, wale nao pia watatusaidia hata katika kupanga mipnago yetu ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia Hoja iliyowasilishwa leo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, nianze kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Naibu Waziri, mwanangu Jenista Mhagama, kwa jinsi alivyoiwasilisha hii hoja pamoja na timu ya Wataalam wa Wizara hii kwa ushirikiano na maandalizi mazuri ya Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji. Shukrani hizi pia ziende kwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wataalam wa Wizara yangu, kwa kuwezesha mchakato huu kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa michango na ushauri na maoni yaliyowezesha kukamilisha Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyekiti kwa sababu, yeye alilianza hili jambo na akaliacha pale Wizarani, Mama Sitta, na mimi naendelea nalo. Bahati nyingine ni kwamba, Mheshimiwa Jenista akiwa Mwenyekiti amekuwa siku zote akilipigia debe Azumio hili na leo hayawi hayawi, yamekuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda niwashukuru sana Watani zetu Kambi ya Upinzani, kwa jinsi walivyoli-*support* Azimio hili. Kweli, katika masuala ya Elimu hakuna ugomvi, nawashukuruni sana na hasa elimu ya maendeleo ya jamii, najua mnaihitaji sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia, Mheshimiwa Mtoa Hoja atakuja kuwataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nitamke kwamba, nami naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu nichangie hoja kwanza kwa kutoa ufafanuzi kuhusu dhana ya mendeleo ya jamii. Najua unaifahamu vizuri sana kwa sababu, ukiwa bado mdogo kabisa ulikuwa Waziri wa Wizara hii na uliacha kulikuwa na moto unachemka pale, kwa hiyo, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana ya Maendeleo ya Jamii ni dhana kongwe katika nchi yetu. Toka tumepata uhuru jambo ambalo wote walilijua mwanzo kabisa ni masuala ya maendeleo na Rais wetu wa kwanza, Hayati Baba wa Taifa, aliliwekea kipaumbele cha aina ya pekee na ndio wakati huo kulikuwa na akina Baba Maendeleo na Mama Maendeleo. Baba Maendeleo akiita wananchi wa Mtaa au wa Kata au wa nini, hakuna ambaye anabaki nyumbani, ilisaidia sana na walifanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchakato huu unahusisha wadau mbalimbali wa maendeleo. Mdau mkubwa ni mwananchi mwenyewe, unahusisha pia Wataalam, lakini pia unahusisha Serikali na *NGO* katika kujiletea maendeleo kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchakato huo Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wao ni Wahamasishaji, Waraghibishaji, wanaobadilisha *mindset* za wananchi kukubali kupokea mabadiliko mbalimbali katika maisha yao. Serikali kwa upande wake inawezesha na kuiwekea mazingira mazuri, ili Maafisa Maendeleo ya Jamii wakishirikiana na wananchi watekeleza miradi yao kwa kujitolea au kwa kuletewa, lakini zaidi Maafisa Maendeleo ya Jamii wako mstari wa mbele kuhamasisha mwananchi mpaka aone umuhimu wa kujitolea na hilo ni zito sana. Wanapojitolea wananchi kufyatua matofali, wanaona ile shule ni yao, wanakuwa na *sense* ya *ownership* na watahakikisha watoto wao wanawapeleka katika ile shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta hii ni mtambuka inahusisha sekta zote, iwe elimu. Tulisoma sisi kwa sababu, Maafisa Maendeleo ya Jamii, walikuja majumbani kwa bibi zetu, kwa mama zetu kusema watoeni watoto wakasome, lakini mpaka leo inahitajika. Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaweza wakahamasisha wananchi kuchangia madawati, Mwalimu ana kazi ya kufundisha, tunampa mzigo mkubwa wakati Afisa wa Maendeleo ya Jamii kama yupo pale, hiyo ni kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kilimo, kubadilisha *mindset* kwamba, sasa tumieni mbolea hii. Yule mkulima anaweza akaelekezwa vya kufanya, lakini atakayembadilisha yule mwananchi mpaka aone ni kweli ni Afisa Maendeleo ya Jamii. Afisa Maendeleo ya Jamii huyu ndiye ambaye anahamasisha akinamama kuhakikisha watoto wanakwenda kupewa chanjo, akinamama wanakwenda *clinic,* mambo makubwa sana ambayo wanafanya, lakini pia hata ujenzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, kuna mmoja amezungumzia kuhusu ujenzi wa nyumba bora, ni kweli. Katika Vyuo vyetu tuna chuo kimoja kinafundisha vikosi vya ujenzi wa nyumba bora, ufyatuaji matofali na mambo mengine ya kitaalam ambayo yanaweza yakafika kwenye Halmashauri. Zamani huko Halmashauri zilikuwa na vikosi vyake vya kusaidia mambo kama haya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa sasa kwa hali ilivyo, Afisa Maendeleo ya Jamii tunawahitaji sana katika kutunza mazingira yetu, si usafi tu, lakini hata katika kuhakikisha nchi yetu mazingira yake hayaharibiki. Kwa hiyo, dhana yetu ya Maendeleo ya Jamii ni dhana mtambuka na ni dhana kongwe ambayo nimefurahi kwamba, leo imeletwa hapa kwa njia nyingine, lakini mimi naona ni vyema watu wakaitambua.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuna sehemu nyingine wanaona kama Maafisa Maendeleo ya Jamii kama ma-*MC,* leo kuna hiki, nenda kafanye hiki, hapana na wao wana mipango yao ambayo wanaweza wakafanya.

Mheshimiwa Spika, kuna Kitabu kimeandikwa *Freedom and Development* cha Mwalimu Nyerere. Alisema, mtu unaweza ukamjengea mtu mwingine nyumba, lakini ile nyumba

hatoionea fahari, yaani umempa; ukitengeneza mwenyewe kitu unakuwa na fahari nacho zaidi kwa sababu, una *sense* ya *ownership.* Maafisa Maendeleo ya Jamii wanajitahidi kuifanya jamii ione shule ni zao, hospitali ni zao, hata ule uharibifu unapungua.

Mheshimiwa Spika, siku hizi wanatengeneza, wanajitolea, Serikali inakuja inachimba kisima; kwa vile wananchi hawakujitolea pale, mmoja anakwenda anaharibu au anaiba kwa sababu, sio chao, ile *ownership* haipo. Afisa wa Maendeleo ya Jamii angetumiwa pale kusaidia, nadhani hali ingebadilika.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyotokea Mtwara juzi, sisi Ofisi yetu ya Maendeleo ya Jamii, Katibu Mkuu wangu tuliongea, kule Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wako wapi? Wangeweza kabisa wakawaelimisha wale wananchi wa Mtwara na Lindi wakaelewa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo zuri ni kwamba, Katibu Mkuu wangu alikwenda akaonana na Katibu Mkuu wa *Energy,* Maswi, wakashuka kule chini na mambo naamini sasa kidogo yanakwenda vizuri. Tulivyofanya tunajua wenyewe jinsi walivyojaribu kubadilisha zile *mindset. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona niseme hayo ya ujumla. Sasa naomba nijibu yale machache ambayo yanahusu Wizara yangu na Mtoa Hoja akija, atajibu yale yanayohusu Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala limetolewa na Kamati kuhusu eneo ni dogo. Ni kweli kweli, Wizara ya Maendeleo ya Jamii inafanya juhudi ya kuzikutanisha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mifugo ambazo ni Asasi zilizopo pale na zinalo eneo la hekta 387. Kwa hiyo, tumepeleka mapendekezo yetu kwa sababu, sisi wote ni Serikali; tugawane tuwekeane, ili tuweze na sisi kupima tuwe na eneo letu. Mazungumzo yako katika *stage* ya Makatibu Wakuu na yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa ni uchakavu wa Majengo na Miundombinu ya Chuo. Ni kweli, lakini toka mwaka 2005 Serikali imekuwa ikikarabati majengo kidogo kidogo, lakini tunaamini sasa ikiwa inajitegemea mambo yatakuwa mazuri zaidi na itatengenezwa kama vile ambavyo Bodi itakuwa ikishauri mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa na Kamati ya Huduma za Jamii ni ufinyu wa bajeti ya chuo ukilinganisha na mahitaji. Ni kweli, ufinyu wa bajeti unatokana na ufinyu wabajeti nzima ya Maendeleo ya Jamii; nyote hapa mmekuwa mkisema bajeti mbona ndogo? Sasa angalau tunaamini kwa kuwa ni Taasisi ambayo inajitegemea, inaweza ikapata ruzuku ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kulikuwa na mjadala wa sifa za wakufunzi. Chuo kina Wakufunzi 30, kati ya hawa Wakufunzi watano wanachukua mafunzo ya Shahada ya Uzamili *(Ph.D.),* Wakufunzi 22 wa Shahada ya Uzamili, Wakufunzi wawili wanachukua mafunzo ya Shahada ya Uzamili, Mkufunzi mmoja ana Shahada ya kwanza, lakini lile suala kwamba, kuna waliopata masomo ya *Masters* na Walimu hawana *Masters,* ile si kweli. Bado hatujaanza kutoa *Degree* ya *Masters,* kwa hiyo, sasa tunao hawa ambao wanachukua *Ph.D.* watano, nadhani hivi karibuni watamaliza wata-*fit* mle, lakini bado Chuo kitaendelea kutafuta Wakufunzi wengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa chanzo cha mapato kwa sasa ni ada. Ni kweli, lakini tunaamini baada ya kuwa kinajitegemea wataweza kuwa wanatoa huduma za *consultancy,* watafanya *research,* lakini pia wanaweza kukopesheka. Kwa hiyo, yote haya tumeyataka ili kukiboresha hiki chuo. Tumeona kikiwa chenyewe badala ya kuwa na sisi Wizara, ambao kila siku tunalialia, nadhani inawezekana kabisa kikaweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa ajira ya Wataalam; ameizungumzia vizuri sana, lakini nami ningependa niizungumzie kama nilivyozungumza, lakini nimeshaizungumza kwenye dhana kwamba, jamani ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Celina Kombani akiwa *TAMISEMI,* tulihangaika sana; watumishi wa Maendeleo ya Jamii walikuwa hata ruzuku hawapati, lakini kwa jitihada zake ameweza kuwa-*convince* Wakurugenzi sasa wanapata ruzuku nadhani ya milioni 12, angalau inawasaidia. Wakati huo walikuwa hawapati kwa hiyo, walikuwa wanaonekana kama ma-*MC,* walikuwa hawawezi kutengeneza mipango yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, umuhimu bado upo kwa sababu asilimia 39 tu ya Kata zote nchini ndiyo zina Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Jamani Maafisa wengi kwenye Kata wako *misplaced,* pale unamkuta huwezi ukamuajiri *engineer* unampeleka kijijini kule Uzaramoni. Kwanza anajifikiria hata ku-*deal* na wale wananchi hawezi. Afisa Maendeleo ya Jamii yuko *trained* ku-*deal*, kujihusisha, kuzungumza na wananchi wa aina yoyote. Kwa hiyo, wengi sana wameajiriwa katika nafasi hizi lakini hawapendi mara nyingi wapo pale wanatafuta kazi nyingine.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Wakurugenzi, naomba wawatumie vizuri, lakini lingine warudishe yale majengo. Natumia nafasi hii kuwaomba Wakurugenzi warudishe yale majengo ambayo yalikuwa yanaitwa *Community Centres* yale yawe chini ya Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kwingine majengo yale mpaka leo yapo yanaitwa *Welfare, Olofair* wanaita, lakini hasa ilikuwa *welfare centre*. Kwa hiyo kule *welfare* kule siyo mahali pa kuuza pombe, ni mahali pa *Community Development Officers* wakutanishe makundi mbalimbali wafanye mambo yao.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni hili la mwisho ambalo mlilizungumza kwamba, fedha zinazokusanywa kwenye hiki chuo zisipelekwe Hazina. Ningependa niwafahamishe kwamba Chuo hiki fedha zake hazimo katika *retention,* kwa hiyo zilikuwa haziendi. Hata hivyo tuna vyuo kama Buhare, Misungwi, Monduli, Rungemba, Mabugai, Uyole, Ruaha na Mlale hawa ada zao zinakwenda Hazina na tunapata matatizo kurudishwa, lakini tumeshafanya mazungumzo na Hazina kuwaomba basi zibaki pale Hazina ndogo iwe rahisi kuzipata, kuliko zikifika *treasury* inakuwa vigumu sana.

Mheshimiwa Spika, vyuo vingine mmesema vipandishwe. Nasema kwamba vyuo vitapandishwa vikikidhi vigezo. Tengeru imekidhi vigezo na tumehangaika miaka mingi mpaka tumefikia hapa na ndiyo maana leo tumeleta hili azimio kukifanya kiwe kinajitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi hii.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtoa Hoja!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipa tena nafasi hii nyingine ili niweze kuja kuhitimisha hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia hoja hii niliyoiwasilisha hapa Bungeni leo tarehe 5 Juni, 2014. Kuna waliosema kwa maandishi na kuna wengine waliochangia kwa kauli. Kwa kweli kwa namna ya pekee kabisa na hasa kwa niaba ya…

Mheshimiwa Spika, samahani naona watu wanaongea kwa sauti.

**SPIKA:** Ngoja tuwatoe nje, naomba uendelee Mheshimiwa! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sababu niliposikia sauti ya *Chief Whip* wangu nilifikiri kuna kitu ananikumbusha hapa.

Kwa hiyo, niseme tu napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kwa kweli kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu Dkt. Shukuru Kawambwa Waziri mwenye dhamana ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tunatoa shukurani za dhati kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, lakini naipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ikiongozwa na Mama Margaret Sitta Mbunge na kaka yangu Mheshimiwa Ngonyani Profesa ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe kwa ujumla kwa ushauri wao na maoni makubwa waliyotupatia katika kuboresha azimio hili na kulifanya leo liweze kufika mbele yako.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa nafasi ya pekee niishukuru kambi ya Upinzani na nimshukuru sana msomaji wa Kambi ya Upinzani leo Mheshimiwa Rajabu kaka yangu. Kambi ya Upinzani leo imetuonyesha uzalendo wa hali ya juu kwa kuthamini sana hoja iliyoletwa mbele. Kwa mujibu wa Sheria hoja hii imeletwa na Wizara yetu ya Elimu na mwanzo ilikuwa kidogo kama inaleta utatanishi kwa nini tumeileta sisi na siyo Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeieleza sana katika taarifa ya Wizara vile vile Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba ameeleza sana. Hii tu ni kwa sababu ya dhamana tuliyopewa kama Wizara ya Elimu ya suala zima la ithibati na udhibiti kupitia Sheria ya *NACTE*, Sheria Namba (9) ya mwaka 1997 na hasa Sura ya 129 ndiyo iliyopelekea sisi sasa tuwe na dhamana ya kuleta mwelekeo mpya wa Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli naomba niishukuru sana Kambi ya Upinzani kwa kukubaliana na sisi na Wabunge wote kwa pamoja wa Kambi ya Upinzani, lakini Wabunge wa Chama Tawala tumekuwa kitu kimoja kuthamini mchango wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika nchi yetu. Nawashukuru sana Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue nafasi ya pekee kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii mama yangu, dada yangu Sophia Simba na Naibu wake ndugu yangu Pindi Chana, lakini vile vile niwashukuru wataalam wa Wizara yake na wataalam wa Wizara yangu tumefanya kazi kwa pamoja na kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia hii hoja ambayo niliiweka mezani kwako leo asubuhi walikuwa 14 ambao walichangia kwa kuzungumza humu ndani, lakini Waheshimiwa Wabunge watatu walichangia kwa maandishi. Kwa kweli nawashukuruni sana, Watanzania wamethaminiu mchango wenu katika kuboresha maendeleo ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba, kweli kabisa wote kwa pamoja kabla sijaanza kujibu baadhi ya hoja ambazo nadhani zinahusu kabisa Wizara yetu zilizoachwa na

Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mama yangu Sophia Simba. Dhana hii ya maendeleo ni kitu cha msingi sana katika kupiga hatua za kimaendeleo, kiuchumi, kiutamaduni na kadhalika katika nchi yetu, lakini watu wengine wamekuwa wakifikiri kwamba tunapozungumza haya maendeleo kwa ujumla wake labda tunazungumza tu kitu ambacho kinaelea hewani.

Mheshimiwa Spika, liko suala la kuangalia kwa undani tunajipanga namna gani na Serikali inasimamia namna gani dhana hii ya maendeleo ya jamii na ndiyo maana leo unaona Serikali imeleta Azimio hili, lakini lengo ni kuboresha tu mwelekeo wa maendeleo katika jamii yetu ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa kufanya wenyewe kazi kwa bidii, lakini pia tusitegemee sana kama fedha ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo na wako wataalam wanaosema kwamba mara nyingi fedha inakuwa ni tunda la maendeleo na siyo msingi wa maendeleo. Kwa hiyo, msingi mkubwa wa maendeleo ni kutengeneza rasilimali mbalimbali ambazo ndizo zitakwenda kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kutengeneza rasilimali hizo ndiyo maana leo sisi tumekuja na azimio hili litakalokwenda kutengeneza rasilimali watu. Tunahitaji sana rasilimali watu katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, naomba sasa nijibu hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge mbele yako katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo ilizungumzwa na Kambi ya Upinzani lakini ilizungumzwa na Kamati ya Huduma za Jamii na Mheshimiwa Mwenyekiti aliisema hapa, lakini vile vile Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa kaka yangu Profesa Kahigi, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, hawa walizungumza sana kutokamilika kwa ujenzi wa jengo la maktaba ambalo lilikuwa limeanza kujengwa katika taasisi hiyo tarajiwa na wakashauri sana kama miundombinu hiyo haitakuwa imekaa vizuri basi wanahofu kama kweli elimu ambayo itatolewa katika taasisi hiyo itakuwa inakidhi viwango ambavyo vinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tulipopokea maombi haya ya kupandisha hadhi, ama ya kuleta mabadiliko ya kimtazamo ya kiuendeshaji ya taasisi hii tulikuta pia liko tatizo hilo la ujenzi wa maktaba. Kamati ya Huduma ya Jamii ilitembelea kule lakini nawashukuru sana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii tena naomba nishukuru sana na ni-*declare interest* tu kwamba, kipindi hicho hata mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii tulitembelea chuo hicho kuona ni namna gani tatizo hili litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Wabunge katika Sheria yetu ya *NACTE* tusingeweza kutoa ruhusa ya kuanzishwa kwa taasisi hii kama Serikali ingekuwa haijajipanga vizuri, lakini naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge katika bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Sophia Simba mwaka huu wa fedha, taasisi hiyo imetengewa jumla ya shilingi milioni 939, ambayo itakwenda kumalizia jengo hilo la maktaba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba msiwe na wasiwasi, mliagiza hapa na mlisema sana kwamba ni lazima jengo hilo likamilike. Jengo hilo sasa litakamilika na kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba na ameahidi kulisimamia kwa nguvu zake zote na fedha imeshatengwa, kwa hiyo hilo tena si tatizo kwa sababu Serikali imefanya kazi ya kulitazama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Profesa Kahigi tena, wao pia walizungumza sana sifa za kitaaluma za uongozi wa

Chuo kutokidhi vigezo vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Hawa Waheshimiwa watatu walizungumza sana suala hili. Sasa tulichofanya wakati tunakwenda kukagua ili kutoa hiyo ithibati na tuweze kudhibiti mfumo wa elimu katika chuo hicho, tulichoshauri na tunashukuru wamekitekeleza.

Mheshimiwa Spika, pia utaona kwamba, tunapolipitisha Azimio hili leo tayari Chuo na kupitia Wizara husika na Serikali kwa ujumla, wameshawapeleka wakufunzi watano wakiwemo viongozi watakaochukua mafunzo katika ngazi ya uzamivu yaani *Ph.D* na viongozi wengine wawili watahitimu mafunzo yao mwaka huu yaani mwaka huu ambao sasa tunapitisha Azimio hili watakuwa wameshahitimu mafunzo hayo ya ngazi ya Uzamivu kwa maana ya *Ph.D*.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa sasa chuo baada ya kuwaelekeza haya tunayotaka wayafanyie kazi, wameendesha sasa na mafunzo mengine ya shahada ya kwanza ambayo wakufunzi waliopo kwa sasa, kuna wengine wanashahada hizo, lakini naomba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba kulingana na miongozo ya Baraza la Taifa ya Elimu ya Ufundi, Mkufunzi anatakiwa awe na angalau ya ngazi ya juu ya yule anayemfundisha, wasilingane ngazi. Hiki Waheshimiwa Wabunge mmekizungumza na Profesa amelikizungumza sana na sisi tunakubaliana kwa sababu ni Sheria inasema hamuwezi mkawa wote labda mna-*degree* halafu mnafundishana, mmoja anakuwa Mwalimu anakufundisha wewe mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa miongozo ambayo ipo Kisheria kwenye *NACTE* ni lazima anayemfundisha mwenzake awe na ngazi iliyomzidi yule anayefundishwa. Kwa hiyo, basi tulipokwenda kukagua kitu hicho tulikuta kwamba kigezo hicho kwa kweli kimezingatiwa na kwa mujibu wa *NACTE* hatuna tatizo, tumeona kwamba ufundishaji huo na hasa kwenye shahada ya kwanza unaweza kuendelea kwa sababu kigezo hicho kimetimizwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja kutoka kwenye Kamati, nafasi ya juu ya Uongozi lazima ishikwe na Profesa au Profesa Mshiriki. Kamati ililiona hilo na sisi tumesema kwamba Bunge hili lifanye kwanza hii kazi ya kuridhia hili Azimio. Baada ya kuridhia hili Azimio, basi utaratibu huo sasa utafuata Sheria ambayo ndiyo inayoongoza mienendo na taratibu za uongozi katika taasisi zilizoweza kupandishwa hadhi kama taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa viongozi wa chuo hiki wanamalizia mafunzo yao ya *Ph.D* na tunaamini kabisa kwamba baada ya Azimio hili kupitishwa hilo tena halitakuwa ni tatizo kwa sababu miongozo itafuatwa, Sheria itasimamia na kiongozi wa Chuo hiki atapatikana kwa mujibu wa Sheria na taratibu ambazo zinasimamiwa na *NACTE*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine la ajira kwa watumishi wa Chuo na hili lilichangiwa sana na Mheshimiwa Ezekiel Maige lakini vile vile na Mheshimiwa Said Mtanda. Kuhusu ajira ya watumishi wa kawaida na wakufunzi wa taasisi hiyo, sisi labda naomba niwape maelezo yafuatayo Waheshimiwa Wabunge ni namna gani suala hili tutakwenda kulisimamia.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi wa kada mbalimbali kwanza yataandaliwa kwa kuzingatia muundo mpya wa kiutendaji katika taasisi hii kwa sababu baada ya Azimio hili kupitishwa ni lazima sasa taasisi hii itafanya kazi kwa muundo mwingine mpya. Hiyo tunakubali kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa na muundo mpya ni lazima sasa kupitia upya muundo wa utumishi na ajira za watumishi ambao watakuwa wana sifa na vigezo vinavyotakiwa katika kufanya kazi kwenye taasisi hiyo. Mahitaji hayo yoote yatakwenda

kuwasilishwa kwenye Bodi na Bodi ile itaundwa kwa kuzingatia pia Sheria ya *NACTE* na kwa kuzingatia pia kanuni ambazo zimetoa tangazo la kuanzishwa kwa taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wala msiwe na wasiwasi, mahitaji yatatambuliwa kwa kufuata muundo mpya wa taasisi ambao sasa ndiyo utakwenda kufanya kazi, lakini baada ya muundo huo kueleweka mahitaji ya watumishi wote wawe wakufunzi, wawe watumishi waendeshaji, wawe watumishi wa aina yoyote ile itatakiwa sasa wao mahitaji hayo yote yapelekwe kwenye Bodi na Bodi itakuwa na kazi sasa ya kuona ni namna gani inatathmini mahitaji hayo na kuweza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mchakato mzima wa ajira utazingatia viwango na vigezo vinavyokubaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)*. Aidha, Sura ya Tatu, kifungu cha 12 cha Tamko hilo la Unzishaji wa Taasisi hiyo, *(Establishment Order)* kinatoa mamlaka kwa Bodi ya Chuo kwa ajili ya wataalam na watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa kuzingatia Sheria ya *NACTE*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na jambo lingine ambalo lilichangiwa sana na Mchungaji Peter Msigwa, baba Mchungaji kutoka Iringa Mjini. Kwa kweli baba Mchungaji leo amechangiwa mchango huu kwa kuonesha weledi wa hali ya juu sana na huku akionesha kabisa ile *profession* yake ya uchungaji, ametoa maelezo ambayo yalikuwa na mantiki ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, suala hili pia limechangiwa na Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed na suala lenyewe lilikuwa mitaala kupitwa na wakati na Profesa Kahigi pia amelizungumza sana suala hili.

Mheshimiwa Spika, sasa mitaala ya mafunzo ya shahada ya kwanza ya Maendeleo ya Jamii katika chuo hiki ilipitishwa na Baraza la Elimu ya Ufundi Stadi mwaka 2008. Wakati tunapitisha mwaka 2008 na tuliruhusu kozi zifuatazo zifundishwe pale. Tuliruhusu kozi ya Maendeleo ya Jamii, lakini pia tuliruhusu kozi ya jinsia na maendeleo na kozi nyingine tuliyoruhusu hapo ilikuwa ni upangaji na uendelezaji shirikishi wa miradi. Tumesema kwamba mitaala hii inaweza kubadilishwa na inaweza kubadilishwa kulingana tu na mahitaji halisi ya wakati ambao tunao sasa na hali halisi ya taasisi jinsi itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumza jambo la msingi sana, wakati mwingine wamesema mitaala hii sasa iwe *demand driven,* iendane na mahitaji halisi ya sasa katika maeneo yetu ya nchi yetu ya Tanzania, tusiendelee kufundisha kozi kimazoea. Kwa sababu tunapozungumzia suala la maendeleo ya jamii tusifikirie ni suala la jinsia tu na watoto, jinsia na nini ama masuala haya ya upangaji na uendelezaji shirikishi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge hapa wamesema sasa hivi tumegundua gesi, je, hatuwezi kutengeneza mitaala itakayowasaidia Watanzania kuendelea na kuendeleza maeneo yao labda kwa kupitia rasilimali walizonazo katika maeneo husika?

Mheshimiwa Spika, sasa hayo yote ndiyo masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetushauri sana na nimesema kwamba kwa kweli ni masuala ya msingi sana. Tunachoweza kuwaambia sisi kama Serikali na hasa Wizara yetu ya Elimu kama wasimamizi wakubwa wa suala zima la ubora wa elimu katika taasisi hii tumesema kwamba, tutakachowaagiza Taasisi waangalie wanafanye *review* ya mitaala waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, wakishafanya hiyo *review* sisi ndiyo wenye mamlaka sasa ya kutoa kibali cha matumizi ya hiyo mitaala mipya kwa kuzingatia hali halisi na umuhimu wa mitaala hiyo kwa wakati tulionao sasa na kwa dhana halisi ya maendeleo katika jamii yetu ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaunga mkono Waheshimiwa Wabunge, katika hili mmezungumza jambo la msingi sana na mnajitahidi kutuambia kwamba ni lazima sasa mitaala yetu tunayoifundisha katika taasisi zetu iendane na mahitaji ya soko tulilonalo kwa sasa, mahitaji ya Watanzania yaliyoko sasa na tusiendelee tu na mazoea ya kila siku. Kwa hiyo, zoezi hili litafanyika na kuna utaratibu wa kisheria na wa kikanuni wa kufanya *review* kila baada ya miaka mitano. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi tuko pamoja. Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rajabu inasikia itasimamia tu na mambo haya yote yatakwenda vizuri wala hakuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Yussuf Hussein, wao pia walisema Serikali isikitelekeze chuo baada ya kupata hadhi ya kujitegemea kiutendaji na walikuwa wakali kweli wakasema hii tabia ya kukiacha tu chuo sasa kinajitegemea nyie mnaachana nacho siyo vema na muone namna gani mtaendelea kukilea.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hatufanyi hivyo, sisi ni wazazi bora, tena ni wazazi ambao tumekua katika maadili mema, Serikali yetu inaelewa umuhimu wa kuendelea kuvilea vyuo ama taasisi hizi kwa namna moja ama nyingine. Kwa hiyo, tunavyo vyuo vingine vingi tu vya elimu ya juu nchini ambavyo vinajitegemea kiutendaji. Mfano, ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini Chuo Kikuu cha Sokoine, Mzumbe. Vyuo hivi vyote bado vinaendelea kupata ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mishahara ya watumishi, Serikali ndiyo inalipia mishahara hiyo yote ya watumishi. Kwa hiyo, unaona kwamba bado Serikali hata ikikipandisha hadhi Chuo ama taasisi, ni lazima bado inaendelea kukilea kwa hali moja ama nyingine. Wakati mwingine hata miradi ya maendeleo bado Serikali imeendelea kuchukua jukumu hilo na kufanya kazi hiyo kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, labda nina mfano hapa halisi kabisa, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, chenyewe peke yake kinakusanya maduhuli, kwa mfano ,kwa bajeti ya makadirio ya mwaka 2014/2015 kinatarajia kukusanya maduhuli ya takribani shilingi bilioni 31.1 na hiyo itatokana na ada. Pia itatokana pia na malipo ya mambo ya *consultancy* na vilevile wana miradi yao hawa ambayo wanaruhusu. Tuliposema kwamba tunataka tukiache kijitanue kijitegemee, kitakuwa na uwezo pia wa kuingia mikataba na vyombo vingine na kutengeneza miradi mikubwa ya kuwasaidia kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niwape mfano mzuri pia ni kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wote tunaona ule uwekezaji wa Mlimani *City*, sasa ule uwekezaji wa Mlima *City* ni kati ya ile mipango ambayo tumewaruhusu wajitanue ili waweze kujiingiza mapato wenyewe. Kuna uwekezaji mkubwa sana pale na fedha ile inapoingia kwenye chuo inawasaidia pia kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata Serikali bado inatoa ruzuku kwa mfano, tuna Bodi ya Mikopo, Bodi ya Mikopo bado inapotoa pesa kwenda kwa wanafunzi chuoni, iko asilimia ya fedha ambayo wanaipata wanafunzi, kwa mfano, hela za vitabu, sijui malazi, *tuition fees* sijui na vitu gani, lakini kuna fedha ya ada ambayo bado inakwenda chuoni. Kwa hiyo, unaona kabisa

jamani hatuviachi hivi vyuo wala hizi taasisi Serikali haiziachi, tunaendelea kuzilea, tunaendelea kuzipa pesa kwa namna moja ama namna nyingine.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kwa sababu sasa taasisi hii tunaipa nguvu ya kujiendesha yenyewe, inaweza kufanya uwekezaji wa namna moja nyingine ama nyingine, *hostel* za mabibo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimewekeza na Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba, tuko pamoja na wala hakuna tatizo kabisa, tutaendelea kuilea taasisi yetu na itaendelea tu kufanya vizuri na itakuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati naendelea kuna hoja ilisemwa sana na Mheshimiwa Said Mtanda na Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Kombo. Hoja hiyo ilikuwa ni kuanzisha matawi ya chuo hiki katika maeneo mengine iwe ndani ama katika maeneo yote ambayo itaonekana inafaa. Wabunge wamesifu na wamekubaliana na sisi kwanza taasisi hii ni taasisi pekee katika Afrika Mashariki ambayo inatoa shahada hizi zinazohusiana na maendeleo ya jamii. Hilo peke yake ni sifa kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kwa kweli hata wenzetu wa vyombo vya habari watusaidie hata Azimio hili likipita leo, Afrika Mashariki ijue leo sisi tumeshapiga hatua kubwa kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa upande wa elimu na hasa kwenye kada hii ya maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunasema katika mfumo wetu wa *NACTE*, kabla ya kukipatia chuo uwezo wa kutoa mafunzo katika ngazi shahada ama zile *level* zetu ambazo tunatoa award ambazo tunaziita *NTA* ilikuwa lazima kueleza Chuo kwamba, wanafunzi watakaotoka katika vyuo vyenye *level* ya chini kutoka kwenye chuo hicho ama taasisi hiyo, hao kwanza ndiyo watakaokuwa wanaingia na kujiunga na chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa sasa tamko la taasisi ya maendeleo Tengeru, linaelekeza Waheshimiwa Wabunge mkifungua aya ya nne, kifungu kidogo cha kwanza, taasisi hiyo imeshapewa mamlaka na uwezo wa kuanzisha matawi yake. Sasa Mheshimiwa Kombo alikuwa anataka na kutuuliza haya matawi tutapeleka mpaka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu taasisi imepewa uwezo kwenye aya hiyo ya nne, kifungu hicho cha kwanza, wana uwezo wakiamua kupeleka matawi yake mpaka Zanzibar, wakiamua wana uwezo hakuna mipaka yoyote, kwa sababu wamesharuhusiwa kabisa kwa mujibu wa tamko la taasisi lililowapa mamlaka ya kufanya hivyo katika kifungu cha nne, kifungu kidogo cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, hata akitaka waende Pemba watafika Mheshimiwa Kombo ili mradi Sheria hii haiwabani inawapa ruhusu wakitaka kwenda Kilimanjaro, Arusha, hata kule Peramiho, wanakaribishwa tu. Kwa hiyo, hakuna tatizo lolote katika eneo, Mheshimiwa Margreth, Mheshimiwa Mtanda na wengine wote. Mheshimiwa Mtanda andaa tu kule mazingira yatasaidia, maana yake tunasema dhana ya maendeleo ni shirikishi tunafanya kwa pamoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kombo ukiwa kule na nyumba yako ile ya ghorofa uliyojenga basi unaweza ukawaalika tu wakaja wakafanya kazi huko. Kwa hiyo, tunasema kwamba hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya uundaji wa Bodi; Mheshimiwa Mtanda aliizungumza sana na Mheshimiwa Margaret Sitta, aliizungumza pia. Tunasema kwamba ili

kuwezesha taasisi hii sasa ya maendeleo ya Tengeru kuanza utekelezaji wa tamko la kuiwezesha kujitegemea kiutendaji, Wizara zetu zitafanya kazi kwa pamoja, kufanya uteuzi wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, lakini na Mheshimiwa mama yangu, Mama Sophia Simba wameshaanza kufanya hii kazi kwa pamoja, kwa sababu Tamko linaelekeza katika aya ya 19 ya Tamko, linatoa maelekezo ya uanzishaji wa Bodi hii. Kwa hiyo, hakutakuwa na mgogoro kwa sababu tamko limetoa maelekezo kwenye aya yake ya kumi na tisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na aya ya 19 ya tamko inatoa maelekezo, lakini maelekezo hayo pia yanasimamiwa na Sheria ya *NACTE*. Sheria ya *NACTE* pia inatoa usimamizi wa kutosha na maelezo ya kutosha sana ya uundwaji wa Bodi hiyo. Kwa hiyo, Bodi itaundwa tu, itasimamiwa, itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria na taratibu hizo ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine, ilikuwa inahusu usimamizi na uendeshaji wa taasisi na vyuo vyetu na Mheshimiwa Maige alizungumza sana suala la ada na Mheshimiwa Spika na wewe ulizungumza sana, ulisema furahieni tu hizo taasisi lakini ada mtaweza. Kwa hiyo, hiyo nayo ulituuliza hapa kwa namna fulani na sisi tunaona kwa kweli lazima tutoe maelezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu imefanya kazi kubwa sana kwenye tatizo la mgongano wa ada na hasa tatizo la mgongano wa ada katika kozi mbalimbali zinazotofautiana kwa namna moja ama nyingine ama kwenye kozi ama program zinazofanana kwa namna moja ama nyingine katika vyuo, lakini zinakuwa na ada tofauti.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaenda katika chuo kimoja ukakuta program hiyo hiyo inayofundishwa katika chuo hicho na kwenye chuo kingine ipo, lakini katika chuo hiki ada iko tofauti na chuo kile kingine. Kwa hiyo, unaweza ukakuta huku labda ni milioni moja na laki tano, chuo kingine milioni moja, chuo kingine milioni mbili na kadha wa kadha. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana na watoto wengi wa Kitanzania na wazazi wa Kitanzania wamesumbuliwa sana na tatizo la utofauti wa ada katika program zinazofanana, lakini katika vyuo tofauti.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu imefanya kazi kubwa, imefanya utafiti wa kina na imekuja na mpango mpya ambao tunauita *unit cost*. Kwenye mpango huu wa *unit cost* tunakwenda kutoa miongozo ya ada elekezi katika taasisi na vyuo vyetu vikuu nchini. Sasa mfumo huu unawataka wa miliki na *Managers* wa hivyo vyuo na taasisi hizo husika kwanza kabisa waangalie na kufanya mapitio ya gharama zao za uendeshaji ambazo ni za moja kwa moja katika vyuo vyao na gharama ambazo si za moja kwa moja kwenye vyuo vyao.

Mheshimiwa Spika, lakini tunataka kabisa kuwasaidia na tushirikiane nao kuwafanya wasitegemee sana ada kama ndicho chombo ama fedha ya kuendesha shughuli za chuo katika maeneo yao. Tunataka ku-*discourage* sana kitu hicho ili kuwafanya wamiliki wa taasisi na vyuo waweze kuwa na mpango maalum kabisa wa kutengeneza ada katika maeneo husika ya taasisi na katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumefanya kazi ya kutosha, tumeshakutana na wadau wote na tumeshatoa miongozo na sasa hivi tunaendelea na semina, lakini tunaendelea kuwapa maelekezo ya kina na tunategemea maelekezo ya semina yetu kila chuo kikishaelewa

vizuri, tumewaagiza waanze kupanga hizo ada zao kwa kuzingatia miongozo sasa iliyotolewa na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, wakishapanga watapeleka *TCU,* Tume yetu ya Vyuo Vikuu, wao sasa ndiyo watakuwa na kazi ya kufanya mapitio na kuona kama ada zile zinaendana na hali halisi ya mazingira halisi ya kila program na ya aina ya chuo ambacho kimependekeza ada hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatutakuwa na tatizo kubwa sana katika eneo hilo kwa sababu Serikali kupitia Wizara yetu ya elimu imetambua tatizo hilo na imemua kwa dhati kabisa kulichukulia hatua ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla masuala ambayo yalikuwa sasa ni ya ujumla, masuala ambayo yalibeba maana ya pamoja ilikuwa ni kuipongeza sana Serikali yetu kwa kuchukua maamuzi na kuleta Azimio hili leo ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge wengine walisema kwamba limechelewa, lakini Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba huko tunakokwenda sasa mtazamo huu wa maendeleo ya jamii, uende ukiwa ni mtazamo unaobadilika na hasa katika Taasisi hii ambayo tumeianzisha.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ni kongwe ina takribani miaka siyo chini ya 51. Sasa ukiona taasisi ambayo ina miaka si chini ya 51 halafu leo tunakuja kuipandisha hadhi katika mtazamo mpya, ujue kabisa kwamba tumedhamiria kuleta mageuzi makubwa katika sekta hii ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tumedhamiria kuleta mageuzi makubwa leo na ninyi Waheshimiwa Wabunge mmetuunga mkono kwa kiasi hiki cha kutosha, tunaomba kuwaahidi kwamba hatutawaangusha, tutaendelea kusimamia. Kama mlivyopendekeza tutazame na vyuo vikuu vingine vyuo vikuu vishiriki na taasisi nyingine na maeneo mengine ambayo tunafikiri kwamba tunaweza kuyapandisha hadhi ili yaweze kusaidia kutoa elimu ya kutosha na elimu inayotarajiwa katika soko kwa watoto wetu wa Tanzania, hasa kama nilivyosema katika hotuba yangu asubuhi, baada ya ongezeko kubwa sana la shule zetu za Sekondari kwenye ngazi ya Kata, watoto wengi wa Kitanzania sasa hivi wana kiu ya elimu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba sisi kama Serikali wenye jukumu la kusimamia maendeleo ya elimu, lakini maendeleo kwa ujumla kwenye nchi yetu, basi tutajitahidi kufanya tathmini ya namna moja ama nyingine na kila tutakapoona kwamba tumefanya tathmini na utafiti wa kutosha tutawaletea Waheshimiwa Wabunge Bungeni kama tulivyofanya leo. Tunaamini mtakuwa mnatuunga mkono mara zote tutakapofanya hili kwa nia njema ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nichukue nafasi hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, lakini nikushukuru sana wewe kwa kuipa Serikali nafasi ya kuja mbele ya Bunge lako Tukufu siku hii ya leo na kuleta Azimio hili muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ,sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 57 na 58 kama mtu angekuwa anataka kufanya mabadiliko katika Azimio hili angekuwa ametoa taarifa kwa Katibu, lakini sikuona mtu aliyefanya hivyo wala hakuna mabadiliko. Kwa hiyo nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Azimio la kuridhia Chuo cha maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi Inayojitegemea Kiutendaji (Tengeru Institute of Community Development (Establishment Order, 2013) ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nachukua nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuleta mabadiliko haya makubwa katika maendeleo ya jamii. Naamini kabisa kama mlivyosema tukitengeneza mitaala kufuatana na hali halisi ya maisha yetu, tunaweza kufika hatua.

Tangu tumeanza kujadili Wizara zote, kitu ambacho sikukipenda hata kidogo, kila mtu anasema Serikali, Serikali, sasa bajeti yenyewe ndiyo hii hapa, hakuna kitakachofanyika kwa mtindo huu wa kwetu, *unless* tunarudi kwenye dhana ya maendeleo ya kujitegemea na Serikali ichangie pale, tutafika hatua kwa *style* hii yetu?

Leo nimefurahi sana kwamba ninyi wote mmeongea kitu kimoja, lakini kila kitu Serikali, mpaka kuchimba choo Serikali, basi tutafika kweli! Serikali ya namna duniani haipo.

Waheshimiwa Wabunge, kazi kubwa za Serikali ni ulinzi, ni haki na mambo kama ya kuendesha Bunge, hiyo ndiyo kazi kubwa za Serikali, zingine nyingi zinapaswa zifanywe na wananchi wenyewe. Kwa hiyo, tubadili *mindset* zetu za kuamini kila kitu hata kuchimba choo kilichotumbukia kule kwako Serikali, hii itakuwa balaa sana.

Kwa hiyo, naomba niwapongeze na wataalam wetu na tuendelee kuonesha hiyo kwamba, maendeleo yoyote yataletwa na sisi wenyewe. Kwa hiyo, nawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutaendelea na Azimio lingine la *SADC*, la Afrika Mashariki bado Kamati inalifanyia kazi kwa sababu wamepewa juzi, kwa hiyo, tutaendelea kesho kama kawaida. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.56 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 6 Juni, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*